**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TISA**

**Kikao cha Saba – Tarehe 7 Novemba, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kwa Mwaka 2006.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 86

**Ufanisi wa Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali**

**MHE. ESTHERINA J. KILASI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, imekuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na ufanisi unaonekana kuwa si mzuri sana:-

Je, ni lini ofisi hiyo itakuwa wakala ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa idhini yako kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Estherina Kilasi naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Chama cha Mapinduzi, kwa kukamilisha chaguzi zake. Nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika, kwa kuongoza vizuri Kamati ile ya usimamizi kwa kufanyakazi kwa kasi na viwango inavyotakiwa. Nawapongeza wote waliopita katika sekretarieti na wajumbe wa Kamati.Kwa niaba ya

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, ina dhamana ya kuchapa Nyaraka muhimu zote za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali. Idara hiyo bado haijawa Wakala wa Serikali kwa kuwa ushauri huo ulikuwa bado tunaufanyia kazi.

Kwa hivi sasa Serikali imekamilisha uchambuzi wake na kukubalika kwamba Idara ya Mpigachapa wa Serikali, haiwezi kuingia kwenye mfumo wa uwakala mpaka ukamilike mpango wa kuipatia mitambo na vitendea kazi ambavyo vitawezesha kukifanya kifanye kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuboresha Idara yetu hiyo, Serikali katika mwaka wa fedha 2007/2008 inatekeleza yafuatayo:-

(i) Inaboresha majengo na Ofisi ya Viwanda vya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kwa kufanya ukarabati ambao kwa sasa unaendelea.

(ii) Inafanya uchambuzi wa kitaalamu wa mahitaji halisi ya Idara kwa maana ya Mitambo na vitendea kazi vingine vinavyoendana na teknolojia ya kisasa, ambao taratibu zake zimeanza.

(iii)Inaendelea na taratibu za ununuzi wa mitambo mipya ya kisasa na pia vitendea kazi. Aidha, kwa mwaka huu, Serikali itanunua mtambo mmoja wa kisasa wa kuchapa nyaraka zianzohitaji usalama wa hali ya juu.

(iv) Itawezesha kutolewa mafunzo yanayoona na teknolojia ya kisasa ya uchapaji kwa watumishi wa Idara.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge hili Tukufu, kuwa Serikali imeweka kipaumbele katika kuona ufanisi wa chombo hiki muhimu kwa taifa unapatikana. Pamoja na hatua hizo mbalimbali za kufanikisha azma hiyo nzuri, Serikali itaendelea kutafakari upya kisera, suala zima la uwakala kwa kuamini kwamba majukumu ya Mpigachapa mkuu wa Serikali pengine bado yanafaa yatekelezwe na chombo cha Serikali ambacho kinakidhi usalama wa dhamana ya kuchapa nyaraka muhimu au maalum za Serikali.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi karibuni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala tulitembelea Ofisi ya Mpigachapa Mkuu na kwa taarifa tu tulizopata pale kwamba hizi sheria ndogo za Halmashauri za Wilaya walikuwa hawachapishi pale. Je, sasa Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba sheria ndogo za Halmashauri za Wilaya zianze kuchapishwa kwenye Ofisi za Mpigachapa Mkuu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali zuri sana la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa taratibu zote na nyaraka zote muhimu zote za Serikali zinahitajika kuchapwa kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, kwa kutumia Bunge hili Tukufu napenda kutoa agizo kwa viongozi wote wa Halmashauri kuhakikisha kwamba nyaraka zote za sheria ndogo ndogo na nyaraka zingine zote muhimu za Serikali zinachapwa kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Na. 87

**Msaidizi wa Mbunge – Viti Maalum**

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI (K.n.y. MHE. PINDI H. CHANA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano imeeleza majukumu ya Wabunge wote bila kubagua Wabunge wa Majimbo na wa Viti Maalum; na kwa kuwa, Wabunge wa Viti Maalum wana majukumu makubwa sana ya kuhudumia Mkoa wote:-

Je, Serikali haioni kuwa Mbunge wa Viti Maalum anapaswa kuwa na Msaidizi kama ilivyo kwa Mbunge wa Jimbo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu linajumuisha Wabunge wa aina mbalimbali waliopatikana kwa mujibu wa Ibara ya 66(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Mara baada ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005, tuliweza kupata Wabunge waliochaguliwa kuwawakilisha wananchi kupitia Majimbo ya Uchaguzi, waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi, Mwanasheria Mkuu, Wabunge walioteuliwa na Rais na Wabunge Wanawake wa idadi isiyopungua asilimia 30 ya Wabunge wote waliochaguliwa na Vyama vya Siasa kwa mujibu wa Ibara ya 78 na kwa kuzingatia masharti ya uwiano wa kura. Utaratibu wa kuwapata Wabunge wa Viti Maalum kupitia Mikoa ni Sera ya CCM na ndiyo Chama pekee kinachotekeleza utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Wabunge wa Bunge hili Tukufu, wanashika nafasi zao za uongozi kwa mujibu wa Katiba ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na mabadiliko yaliyofanywa kwa Sheria iliyotungwa na Bunge. Masharti ya kazi ya Mbunge yanajumuisha Wajibu na Haki/Stahili kwa mhusika.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali inatambua majukumu waliyonayo Waheshimiwa Wabunge katika makundi yao na ndiyo maana inaheshimu na kuhakikisha inatekeleza kikamilifu Ibara ya 73 ya Katiba ya Nchi na sheria mbalimbali zinazotungwa na Bunge.

Suala la Mbunge wa Viti Maalum kuwa na Msaidizi kama ilivyo kwa Mbunge wa Jimbo ni suala linalohitaji kuwasilishwa rasmi Ofisi yako Mheshimiwa Spika, ambayo kwa kutumia Kamati inayohusika linaweza kuchambuliwa na hatimaye mapendekezo yake yakawasilishwa Serikalini. (*Makofi*)

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wabunge wengi wa Viti Maalum wameonekana hawana Ofisi na kwa kuwa imekuwa ni vigumu sana kuwapata Wabunge wa Viti Maalum, wanapokuwa kwenye Mikoa yao. Je, Wizara haioni kwamba sasa hivi ni wakati muhimu wa kuharakisha ofisi hizo kwa ajili ya Wabunge wa Viti Maalum? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Waheshimiwa Wabunge wote wanahitaji kuwa na ofisi na sasa hivi Kamati inakamilisha taratibu zote za kuanza kujenga ofisi za Waheshimiwa Wabunge, kwa awamu. Lakini pia suala la Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum, bado tunaliangalia kwa maana ya utekelezaji, hasa tukizingatia kwamba Wabunge hawa wametawanyika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, suala hili tunalifanyia kazi pale itakapokamilika basi shughuli hiyo itatekelezwa.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba Wabunge wa Viti Maalum, sasa hivi hawana wasaidizi. Nilikuwa napenda kujua kazi za wasaidizi wa Wabunge ni nini na kwa sasa hivi Wabunge wa Viti Maalum wanafanyiwa na nani kazi hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo wana wasaidizi ambao wanawasaidia katika shughuli zao katika majimbo yao. Wote tunafahamu kwamba Waheshimiwa Wabunge waliopo katika majimbo wana eneo mahususi na wana shughuli zinazoeleweka. Lakini pia tunajua kwamba Wabunge wa Viti Maalum ambapo na mimi ni mmojawao tuna shughuli mahususi japokuwa tunawakilisha eneo ambalo siyo la kijiografia. Tunawakilisha watu na makundi mbalimbali. Kwa utaratibu huo basi najua wote tunafanyakazi hizi bila kuwa wasaidizi. Lakini kama nilivyokwishasema, taratibu za kuingiza Wabunge wa Viti Maalum hapa Bungeni zinatofautiana sana kutokana na chama hadi chama kingine. Chama cha Mapinduzi kama nilivyosema kina utaratibu wa kuwaingiza Wabunge kupitia Mikoa. Vyama vingine vina utaratibu wao ambavyo vinaelewa. Sasa tunataka tuwe na uwiano wa pamoja ili tunapoweza kutoa msaada huo

ukaweza kuwasaidia wananchi na ikaleta tija inayokusudiwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Viti Maalum naomba tuvute subira tunajua tuna tatizo hili na tunalifanyia kazi. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER K. NYAWAZA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunapofikia masuala ya viti maalum ndani ya Bunge na Serikali inatambua kabisa Viti Maalum kazi yao ni sawa sawa na Wabunge wa Majimbo. Sasa tunapofikia masuala ya majukumu na haki za Wabunge wa Viti Maalum, Serikali inaanza kusema wanaangalia, hebu naomba leo Serikali ituambie Wabunge wa Viti Maalum, tunatofautiana namna gani na Wabunge wa Majimbo? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa tunatambua utaratibu wa kuwa na Wabunge kutoka katika Majimbo. Utaratibu huu tuliojiwekea ya kuwa na Wabunge kutoka makundi mengine ni utaratibu ambao tumejiwekea wenyewe na unaweza ukarekebishwa kutokana na michakato mbalimbali inayoendelea. Najua kabisa kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum ambapo na mimi ni mmojawao tuna kazi nzito na muhimu sana kwa Taifa.

Lakini pia kama nilivyosema kutokana na tofauti zilizopo za kuingiza Wabunge wa Viti Maalum kutokana na Chama ipo Mikoa ambayo kuna Wabunge wa Viti Maalum zaidi ya 7, kuna Mikoa ina Wabunge wa Viti Maalum 2. Kutokana na uwiano huo ambao haulingani tunaona muda na tutapata ushauri wenu ili tuweze kuona ni jinsi gani tutaweka rasilimali na Wabunge wote wakapata tija inayokusudiwa. (*Makofi*)

Na. 88

**Hadhi ya Stendi ya Mabasi Dodoma**

**MHE. MOHAMED HABIB J. MNYAA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali ya Tanzania, ambapo kuna mzunguko mkubwa wa watu wanaoingia na wanaotoka katika Mji huo kwa kutumia mabasi ya abiria, na kwa kuwa, stendi ya mabasi ya Dodoma hailingani na hadhi ya Makao Makuu kutokana na uchafuzi mkubwa wa mazingira kama vile vumbi wakati wa jua na tope mithili ya lambo wakati wa mvua, hali inayosababisha usumbufu mkubwa wa abiria, wafanyakazi waliopo hapo na watu mbalimbali wanaoitumia stendi hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha hali ya mazingira katika stendi hiyo ya mabasi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Stendi ya Mabasi ya Dodoma, haikidhi hadhi ya Makao Mkuu kwani stendi hiyo ni ya muda siyo ya kudumu kwa maana ya kwamba itahamishwa. Kuhusu barabara zinazoingia stendi hiyo, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma imeweka mikakati ya matengenezo ya Barabara zilizomo ndani ya eneo la stendi ikiwa ni pamoja na kuimarisha huduma za ulinzi na usafi. Kwa mwaka wa fedha 2007/2008 jumla ya shilingi 14,000,000 zimetengwa kwa ajili hiyo na matengenezo ya barabara hizo na yataanza mwezi Desemba, 2007.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa na stendi ya kudumu, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (*CDA*) kwa mujibu wa mpango wake kabambe wa mwaka 1976 ilitenga eneo lenye ukubwa wa ekari kumi (10) katika eneo la Tambukareli. Hata hivyo, kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na ya baadaye eneo hili limeongezwa na kufikia kiasi cha ekari arobaini (40). Eneo hili liko umbali upatao kilomita tatu, Kusini – Mashariki mwa Mji wa Dodoma, njia iendayo Chuo Kikuu cha Dodoma. Sehemu hii pia imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Mkuu (*CDA*) inafanya utaratibu wa kupima eneo hili kwa sasa na litamilikishwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma mwishoni mwa mwezi huu wa Novemba, 2007 kwa ajili ya kulifanyia usanifu. Manispaa ya Dodoma ndiyo yenye wajibu wa kujenga stendi hii. Ujenzi unategemea upatikanaji wa fedha kutoka Serikali Kuu, wadau mbalimbali watakaojitokeza na mashirika ya fedha.

**MHE. MOHAMED HABIB J. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la uchafuzi wa mazingira ni suala mtambuka na kunatokea uchafuzi wa mazingira kwa mabasi yanayoingia na yanayotoka katika Mji wa Dodoma kupitia abiria wanaopanda magari hayo na wakati wanapokula chakula hutupa mifuko ya *plastic*, maganda ya machungwa na ndizi barabarani ovyo:-

(a) Je, *SUMATRA* na Ofisi yako itafanya vitu kulazimisha wamiliki wa mabasi haya kuweka sehemu maalum ya kutupia taka kwenye mabasi kama *dustbin*?

(b) Kwa kuwa eneo la Tambukareli lililopangwa kujengwa stendi ya kudumu ya baadaye fedha hazijapatikana. Na kwa kuwa hazijulikani zitapatikana lini. Lakini eneo la stendi iliyoko lina hali mbaya, kuna vioski vilivyojengwa ambavyo hazina thamani kulingana na hadhi ya Makao Makuu. Je, Halmashauri ya Mji wa Dodoma, itachukua hatua gani za dharura kujenga mabanda yenye mwelekeo mzuri ya kuwakodisha wajasiriamali ili mandhari ionekane nzuri? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Kuhusu suala la uchafuzi wa mazingira ni kweli abiria

hutupa takataka sehemu yoyote hata barabarani bila kuchagua kwamba ni sehemu gani. Lakini kwa Manispaa ya Dodoma pale stendi kuna utaratibu maalum, kuna *dustbin* ambazo zipo kwa ajili ya kutupa takataka hizo. Kuna kampuni maalum ambayo inashughulikia uzoaji wa taka katika stendi hiyo. Kwa hiyo, hilo ni jukumu la Manispaa ya Dodoma na wanatimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria.

Kuhusu hatua za dharura kwa stendi iliyopo sasa hivi sisi kama Serikali tuliona si vema kuziba viraka kwenye iliyoko sasa hivi. Tunachotilia mkazo zaidi ni kuhakikisha kwamba eneo la stendi mpya linapatikana na kuanzia mwaka ujao, *feasibility study* itafanyika, baada ya kufanyika tutajua kwamba ni kiasi gani cha fedha kinatakiwa katika kujenga stendi mpya ambayo itakuwa na miundombinu mpya na itakuwa stendi ya kisasa.

Kwa hiyo, tutajenga kwa awamu lakini kubwa zaidi ni upatikanaji wa eneo, mmilikaji wa eneo hili na baadaye kujua kwamba inahitaji kiasi gani ndipo Serikali itapanga katika Bajeti zake za kila mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha. (*Makofi*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imekuwa ni mazoea kwa usemi unaosema kwamba mgeni njoo, mwenyeji apone mara anapoalikwa au kiongozi yeyote mkuu wa nchi anapotembelea sehemu ile hukarabatiwa. Je, Naibu Waziri anaweza na Ofisi yake kumwalika aidha, Waziri Mkuu au Rais, kutembelea eneo lile ili liweze kukarabatiwa kwa dharura? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ratiba ya Rais, ratiba za Mheshimiwa Waziri Mkuu, zinakuwa zimeshapangwa kwa mwaka mzima. Sasa siyo rahisi kumpangia tena ratiba upya kwa ajili ya kuangalia hiyo stendi. Mimi naomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira hilo tunaloongea lipo na hiyo stendi ya sasa tunahakikisha kwamba angalau inakuwa safi na inakuwa katika hali nzuri ili kukidhi mahitaji ya sasa. Lakini suala la stendi mpya ndilo hilo ambalo tunatilia mkazo zaidi. Kuhusu kwamba wageni wakija ndipo sehemu zinatengenezwa si kweli, Kwa mfano kwa taa za Dodoma, kwa mwaka huu nilijibu swali hapa Bungeni, Bunge lililopita kwamba Dodoma taa zitawekwa. Siyo kwa ajili ya ugeni lakini tulijibu na mipango thabiti ya Serikali ilishawekwa kwamba taa zitawekwa katika Manispaa ya Dodoma, siyo kwa ajili ya ugeni.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri nyingi sana hapa nchini zina sheria ndogo ndogo za usimamizi wa mazingira. Lakini ni Halmashauri chache sana ambazo zinatekeleza sheria zake na kuzisimamia ipasavyo. Matokeo yake miji mingi sana hapa nchini ni michafu sana. Je, Serikali itachukua hatua gani dhidi ya Halmashauri hizo ambazo hazisimamii kabisa sheria ndogo ndogo za hifadhi ya mazingira? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kila Halmashauri imejiwekea

sheria ndogo ndogo ya uhifadhi wa mazingira na hata sera yetu inasema wazi kuhusu uhifadhi wa mazingira. Sisi kama Serikali tunachukua hatua mbalimbali.

Kwa mfano, kila mwaka kuna mashindano ya usafi wa miji, majiji na Halmashauri katika sehemu zote nchini. Hii ni hatua mojawapo ya Serikali ya kuhakikisha kwamba mazingira yanawekwa katika hali ya usafi. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge, mtakuwa mashahidi kwamba kila mwaka tunatangaza Manispaa au Jiji, Mji ambao umefanya vizuri katika mambo ya usafi na uhifadhi wa mazingira.

Kwa hiyo, ni wito wangu kwamba kila Halmashauri ihakikishe kwamba mazingira yao yanakuwa masafi. Hiyo ndiyo azma ya Serikali na huu ndiyo msimamo wa Serikali.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mwuliza swali linalofuata, nilikuwa napenda niseme tu kwamba mwenzetu mmoja aliyekuwa anatamkwa kwamba katika wadhifa wake mguu mmoja uko nje mwingine ndani, jana amethibitishwa tena na nimeshindwa kujizuia. Hivyo naomba Mheshimiwa Yusuf R. Makamba, aweze kusimama ili tuweze kumpongeza. Ahsante sana. Mambo ya vyeo vikubwa hivi ni hatari sana ukimwona mtu anasemwa atadondoka na hivi. Basi, asipodondoka ni vizuri kuwa tunapongezana. (*Makofi*)

Na. 89

**Fidia kwa Wananchi wa Manga**

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Mpanda unapata maji kutoka katika bwawa la Milala na Maji ya Mtaro Manga na kwa kuwa nakubaliana na hatua za kulinda, kuhifadhi na kuendeleza maeneo hayo ambayo wananchi wakiyatumia kabla ya kuweka vituo vya kusukuma maji na kuchimba bwawa:-

(a) Je, kwa nini Serikali haitambui mipaka iliyokuwepo wakati bwawa linachimbwa mwaka 1956 na kuwaondosha wakulima, kuharibu mazao yao na kuweka mipaka mipya bila ya kuwalipa fidia wananchi hao?

(b) Je, Serikali imechukua hatua gani juu ya maafisa wake waliofanya uharibifu kule Manga na waliochoma moto nyumba za wananchi?

(c) Je, kwa nini Serikali iliwaondosha kwa nguvu wananchi wa Manga barabarani na kuchoma moto nyumba na mashamba yao bila ya kuwalipa fidia wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** aljibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Kati, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mji wa Mpanda unapata maji kutoka katika vyanzo vya aina tatu, bwawa la Milala lililojengwa mwaka 1956 maji ya mtiririko kutoka Manga na visima virefu na vifupi vilivyoko Mjini Mpanda. Mazingira ya vyanzo vya bwawa la Milala na kile cha mtiririko cha Manga yanaharibika sana kutokana na shughuli za kilimo na ufugaji. Baada ya kuona hali ya uharibifu wa vyanzo vya maji inaendelea kwa kasi, Halmashauri ya Wilaya ilituma sheria Na. 42 ya 1974 na sheria ndogo ya mwaka 2001 ya kulinda vyanzo vya maji kwa kulitangaza eneo hilo kuwa ni hifadhi ya vyanzo vya maji. Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaitambua mipaka yote iliyokuwepo wakati wa kujenga bwawa mwaka 1956, kilichofanywa na Halmashauri ya Wilaya ni kutekeleza sheria Na. 42 ya mwaka 1974 na sheria ndogo ya Halmashauri ya Wilaya ya Hifadhi ya vyanzo vya maji ya mwaka 2001 inayozuia shughuli za kilimo au ufugaji katika eneo la mita 500 kutoka kwenye kingo za chanzo. Wakati wa utekelezaji wa sheria hii wananchi waliruhusiwa kuvuna mazao yao kwanza kabla ya kutakiwa kuhamia maeneo mengine. Hata hivyo, baadhi ya wananchi waligoma kuhama na Halmashauri imewafungulia mashtaka Mahakamani kwa kesi Na. 2/2005 na 18/2006. Suala la fidia kwa walioondolewa linasubiri maamuzi ya Mahakama kuthibitisha kama wanastahili.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la sehemu (a) wananchi waliokuwa wanaishi ndani ya eneo la hifadhi walitakiwa wahame kulingana na sheria Na. 42 ya mwaka 1974 na sheria ndogo ya Halmashauri ya Hifadhi ya vyanzo vya maji ya mwaka 2001. Katika kutekeleza sheria hiyo, elimu ilitolewa kwa wananchi kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji na hatimaye walipewa notisi ya kuhamia maeneo mengine baada ya kuvuna mazao yao.

Baada ya hapo, Kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya kwa kushirikiana na Serikali ya Kijiji cha Manga, iliweka ulinzi wa sungusungu kuhakikisha kuwa wahusika wote wanaondoka na mabaki ya makazi yao yanasafishwa. Baadhi ya wananchi waliokaidi na wenyewe walifungulia kesi sungusungu ya kuwachomea nyumba zao. Kesi hiyo, ipo mahakamani.

(c)Mheshimiwa Spika, suala la fidia kwa wananchi waliohamishwa litajadiliwa kati ya uongozi wa Halmashauri na wahusika mara baada ya mahakama kutoa maamuzi yake.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kama Waziri alivyoeleza katika

utangulizi wake mipaka ya hifadhi ya vyanzo vya maji imeongezwa imepanuliwa bila kuwashirikisha wananchi waliokuwa wakiishi katika maeneo yanayozunguka vyanzo hivyo na kwa sababu elimu ya kutosha haikutolewa ikalazimika wananchi hao wachomewe nyumba zao na kesi iko Mahakamani.

Je, Waziri anasema nini au anafahamu kwamba hao waliofanya kitendo cha kuchoma moto wame-*abscond* dhamana na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na kesi hiyo inaendelea kuzungushwa mpaka leo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba sheria tunazitunga sisi wenyewe humu Bungeni. Kwa hiyo, wananchi huwa wanashirikishwa wadau mbalimbali katika hatua za awali. Kwa hali hiyo basi sheria hii ya kuongeza hiyo mipaka ilifanyiwa humu Bungeni na ilikuwa ni wajibu wetu baada ya kupita sisi wenyewe kama wawakilishi wao pia tuweze kuwafahamisha na kuwapa elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala la pili ni kwamba kama nilivyosema kesi hii iko Mahakamani na ni Mahakama ambayo ndiyo yenye uwezo wa kuamua haki iko upande gani. Naomba hilo tuliache tusubiri Mahakama watupe ufafanuzi wa mambo yataendaje. Ahsante.

Na. 90

***T.I. B.* Kuwa Benki ya Maendeleo**

**MHE. MOSSY S. MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, *T.I.B.* ni Benki inayofikiriwa kufanywa Benki ya Maendeleo:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani za kuboresha zoezi hilo?

(b) Je, hadi sasa Serikali imeshalipatia T.I.B. kiasi gani cha fedha za mtaji ili kuboresha zoezi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa mnamo mwaka 2005, Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) iligeuzwa kuwa Benki ya Maendeleo kwa ajili ya kutoa mikopo ya muda wa kati na muda mrefu kwa sekta ya uzalishaji hapa

nchini, ambapo ilikubalika kwamba mtaji wa benki hii uwe Tshs. 50.0 bilioni. Katika hatua za awali mnamo mwaka 2006 Serikali iliidhinisha *TIB* kutumia kiasi cha Tshs. 12.7 bilioni kutokana na mradi wa kukarabati vituo vya petroli (*Petroleum Sector Rehabilitation Project (PSRP)* kuwa mtaji.

Mheshimiwa Spika, hatua hii imeongeza mtaji wa *TIB* kutoka Shs. 7.721 bilioni hadi Shs. 24.9 bilioni. Hatua inayofuata ni Serikali kuuza hisa zake katika *Tanzania Development Finance Limited (TDFL)* ambapo mapato yake pia yataongeza mtaji wa Serikali katika *TIB*. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha katika Bajeti ya Serikali kwa awamu kwa awamu ili kuhakikisha kuwa kiwango cha mtaji cha Tshs. 50.0 bilioni kilichokubaliwa kinafikiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hii Serikali imeiruhusu *TIB* kukopa kiasi cha *USD 5.0* milioni kutoka nje ya nchi kwa lengo la kupata fedha za kutoa mikopo kwa wawekezaji wa kati (*SMEs*) ikiwa ni njia mojawapo ya kuwawezesha wawekezaji wa ndani.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Je, Serikali haioni kwamba ingekuwa ni jambo zuri kuanza kujiandaa na kuweka utaratibu ambao utaiwezesha Benki hii kufanya shughuli zinazofanywa na Benki Kuu sasa kuhusu dhamana ili kupunguza usumbufu kwa watu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, *TIB* haiwezi kufanya kazi za dhamana kama inavyofanywa na Benki Kuu kwa sababu kazi inayofanywa na Benki Kuu kwa dhamana hii ni kwa mujibu wa Sheria tuliyoiweka hapa Bungeni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hapo tutakaporekebisha baadhi ya vipengele vya sheria hiyo kama tukihisi kwamba itakuwa ni sawa tunaweza tukafanya hivyo.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM kuna eneo mahsusi linalozungumzia kwamba Serikali ya awamu ya Nne itaweka mkazo katika kuanzisha benki ya wakulima kwa maana ya Benki ya Maendeleo.

Majibu aliyotoa Naibu Waziri hayaonyeshi kama kweli huo mkazo upo kwa sababu bila Benki ya Maendeleo katika neno halisi ya benki ya Maendeleo mambo yote tunayotaka yaende mbele kwa maana ya Maendeleo hayawezi.

Swali, Mheshimiwa Naibu Waziri anatuambia kwamba Serikali itakuwa inaongeza mtaji kila Bajeti taratibu kwa kipindi hiki tutakuwa tumekwishafikisha huo mtaji wa shilingi bilioni 50 Serikali haiwezi kuwekeza bilioni 50 kwa mara moja? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ni kweli imesema hivyo.

Lakini bado hatujatoka kwenye Ilani, lakini kupanga ni kuchagua. Ni Bunge lako Tukufu na Kamati mbalimbali lililopendekeza umuhimu wa kutumia fedha zetu kwa siku mbalimbali kwa mahitaji kwamba ni *prioritities* zetu.

Kwa hivyo kama nilivyosema kwa sasa tumewaambia *TIB* tumewaruhusu wakope kutoka nje pengine katika Bajeti ijayo tutahakikisha kabla ya miaka mitano haijamalizika hii benki ya maendeleo itakuwepo. Tumechagua yale kwanza ya kuyafanya mwanzo na hayo mengine yatakuja baadaye kama hali itavyoruhusu.

Na. 91

**Ulipaji wa mafao ya wastaafu**

**MHE. FATMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 Serikali ilifanya marekebisho katika Sheria ya wastaafu ya mwaka 1999 na sehemu ya kwanza ya marekebisho hayo yanawahusu wastaafu waliokuwa wamechukua pensheni yao kwa mkupuo kurejeshwa kwenye daftari la malipo ya pensheni.Pamoja na vima vipya vya pensheni ambavyo wastaafu walitakiwa kulipwa tangu tarehe 01/01/2005 kufuatana na ngazi za vyeo walivyoachia wakati wanastaafu, yaani vyeo vya maafisa na shs.21,600/= kwa maafisa wa vyeo vya chini:-

(a) Kwa kuwa wastaafu waliolipwa kwa mkupuo wamerudishwa kwenye daftari la pensheni. Je, Serikali itatekeleza lini sehemu ya pili ya kutoa viwango vipya vya pensheni ambavyo hata hivyo vimepitwa na wakati?

(b) Kwa kuwa utaratibu wa malipo ya pensheni kwa sasa ni kila baada ya miezi sita, malipo ambayo humsaidia mstaafu kujikimu maisha yake. Je, Serikali haioni umuhimu wa kulipa pensheni hiyo kila mwezi kufuatana na mkataba wa ajira?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, swali lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kuwarudisha wastaafu waliochukua pensheni kwa mkupuo kuanzia mwezi Julai, 2004. Kazi ya kurekebisha malipo hayo ili yawepo katika vima vipya vya pensheni ambavyo wastaafu walitakiwa kulipwa kufuatana na ngazi za vyeo walivyoachia wakati wanastaafu bado inaendelea, ikiwa tayari penseheni italipwa kwa kutumia vima vipya.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuboresha huduma ya pensheni kwa wastaafu wa Serikali kwa kuihamishia huduma hiyo katika mifuko ya pensheni.

Kuanzia mwezi Januari mwakani wastaafu waliopo katika daftari la wastaafu ambao wanalipwa pensheni kila baada ya miezi sita watalipwa na mfuko wa pensheni kwa Mashirika ya Umma *(Pastatal Pensions Fund).* Wastaafu watakaohusika na utaratibu huo ni wale waliostaafu hadi Juni, 2004. Utaratibu wa mfuko huo ni kulipa pensheni za wastaafu kila mwezi, hivyo kuanzia Julai, 2008 wastaafu hao watapokea pensheni kila mwezi.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa Serikali inajaribu kuunda Taasisi moja itakayoshughulikia mambo ya pensheni lakini inasahau kitu kimoja kwamba wanapolipwa pensheni wanapensheni wanapata usumbufu sana sana mara njoo leo mara kesho, fuata hapa, fuata pale. Hivi kuna utaratibu gani kiserikali ambao utahakikisha kwamba malipo ya pensheni yanakuwa *smooth* bila usumbufu ambao hivi sasa wengi wanaupata? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kama tulivyokwishajibu hapo nyuma, kwamba utaratibu umefanywa kwamba ulipaji wa pensheni unapelekwa katika mifuko yetu mbalimbali ili kuondoa usumbufu huu. Na tunayasema haya kwamba kuanzia Januari watakuwa wanafanya hivyo na hasa kwa wale wastaafu ambao hawahusiani na mfuko wa *PSPF*, wale ambao wameanza mfuko wa *PSPF* ambao sheria yake inasema kuanzia mwaka 1999 mpaka 2004 wameanza kulipwa hakuna matatizo hayo hata kidogo.

Lakini hayo ya pensheni za nyuma kwa sasa hivi hayo hakuna matatizo. Kama tulivyojibu hapo nyuma wiki iliyopita kuhusu polisi, likitokea tatizo pale pale tayari ni rahisi kulitatua. Matatizo yaliyokuwepo ni wale wa nyuma kabisa, lakini nalo tumeshalitafutia dawa.

Na. 92

**Hifadhi ya Makazi na Huduma za Afya kwa Wazee**

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwa kutambua umuhimu wa wazee katika Taifa letu na hata Ilani ya Uchaguzi ya CCM inatambua mchango wao katika Taifa hili ndiyo maana imewahakikishia wazee wapewe hifadhi ya makazi, huduma ya afya na za kijamii:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kuwahudumia wazee hao katika huduma hizo muhimu?

(b) Kwa upande wa matibabu. Je, lini wazee hao watapewa vitambulisho maalum ili kuepuka usumbufu wanaoupata kwa sasa pamoja na kuwa na madaktari wao katika kila hospitali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali na hata Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) inatambua mchango mkubwa wa wazee wetu katika maendeleo ya Taifa letu kupitishwa kwa Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003 kunathibitisha kuwa Serikali yetu inatambua na kuthamini umuhimu wa wazee na imedhamiria kwa dhati kuwahudumia.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa huduma ya matunzo kwa wazee wasio na uwezo na ama wasio na ndugu wa kuwahudumia. Huduma hizo zinatolewa katika makazi 17 yanayoendeshwa na Serikali na makazi 24 yanayoendeshwa na wakala za hiari. Kadhalika Serikali kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii, hutoa misaada ya kimaisha kwa wazee walio nje ya makazi.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoliarifu Bunge lako Tukufu katika mkutano wa 5 tarehe 1/11/2006 wakati nikijibu swali na 17 lililoulizwa na Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, maelekezo ya Wizara yangu kuhusu suala la matibabu ya wazee yako wazi. Wazee wote wanaostahili kupata msamaha wanatakiwa kupata uthibitisho wa kutokuwa na uwezo kutoka kwa Afisa wa Ustawi wa Jamii au viongozi wa Serikali ya mtaa katika eneo analoishi mwombaji. Uthibitisho huo uwasilishwe kwa uongozi wa hospitali kwa ajili ya hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwataka watumishi wa Wizara yangu katika sehemu zote za kutolea huduma (zahanati, vituo vya afya na hospitali) nchini kuwajibika ipasavyo kwa wananchi wanaohitaji huduma za afya kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa katika taratibu za msamaha wa matibabu.

Mheshimiwa Spika, aidha hivi sasa, Wizara yangu inashughulikia mpango wa uwezekano wa kuwa na chumba na wataalam kwa ajili ya matibabu ya Wazee katika kila hospitali ya Wilaya ili kuboresha zaidi utoaji wa huduma za afya kwa Wazee.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hao wazee wengi ili waweze kutibiwa na kupata matibabu ya bure ni lazima waende kwa Afisa Mtendaji ili waweze kupewa barua ya utambulisho kwa sababu ya kukosekana kwa vitambulisho. Swali langu ningependa kufahamu hivi ni kwa kuwa vile vitambulisho vya kupigia ni vitambulisho halali ambacho kinaonyesha umri wa mzee huyo. Ni kwa nini kwa wakati huo Serikali isiviruhusu vitambulisho hivi viweze kutumika na wazee moja kwa moja waweze kwenda hospitalini kuliko kuwazungusha wakati wao ni wagonjwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba wazee wana vitambulisho vya mpiga kura, lakini vile vile ni busara wazee hawa wakatambulika kule sehemu wanakotoka kwa Maafisa Watendaji

kwa sababu siyo wazee wote ambao wana umri mkubwa wanahitajiwa kupata msamaha wa matibabu. Wapo wazee wanafikisha miaka 60 lakini wana uwezo mkubwa na hivyo haiwezekani kwa kupewa msamaha.

Mimi naomba tu ili kuwa na utaratibu nzuri na kwa kuwatambua wazee wetu sehemu tunazoishi wazee wanafahamika, uwezo wao tunaufahamu. Tutoe tu wito kwa Watendaji na wananchi na wafanyakazi wetu waliopo kule wawatambue wazee wanapofika sehemu za kutolea huduma ili wasipate usumbufu hata kama atakuwa hana kitambulisho. Mheshimiwa Spika, napenda nikuambie na niliambie Bunge lako Tukufu kutokuwa na kitambulisho na kuwa na kitambulisho, mzee anapofika pale na hata mtu ambaye hana uwezo hata hajafikia uzee haitamzuilia kupata huduma. *(Makofi)*

Na. 93

**Wazee waliopigana vita ya Pili ya Dunia**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Jimbo la Siha kuna Wazee waliopigana katika vita ya Pili ya Dunia mwaka 1939 – 1945 katika jeshi la *Kings African Rifles (KAR)* ambao wamekuwa wakifuatilia mafao yao kila mafanikio na kwa kuwa kila Serikali ilipojibu swali hili haikupata ufumbuzi wa kudumu hasa katika utelelezaji wake:-

Je, Serikai inawaambia nini wazee hao sasa, hasa tukizingatia kuwa tuna kauli mbiu ya Ari Mpya,Kasi Mpya na Nguvu Mpya chini ya Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango mkubwa wa askari waliopigana vita vya pili ya dunia mwaka 1939-1945 katika kutetea uhuru wa Uingereza, Serikali ya Uingereza iliamua kutoa posho ya kujikimu kwa askari wote waliopigana vita hiyo kutoka nchi mbalimbali ikiwepo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, posho hiyo imekuwa inapitia *Tanzania Legion* na uongozi wa chama hiki ndiyo ulikuwa na jukumu la kutambua askari waliostahiki na kuwapa posho hiyo. Kuanzia mwaka 2000 kumekuwepo na mgogoro wa uongozi na pia tuhuma za ubadhirifu ndani ya *Tanzania Legion* uliosababisha chama cha *British Commonwealth Ex-Service League* kufuta mahusiano na *Tanzania Legion* na hatimaye kusitisha posho hiyo. Ilikubaliwa kuwa posho hiyo itarejeshwa tena iwapo *Tanzania Legion* itakuwa na uongozi madhubuti utakaolinda na kuhakikisha kwamba posho inawafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba sharti hili linazingatiwa Wizara yangu iliipatia *Tanzania Legion and Clubs* fedha za uchaguzi mkuu ambao ulifanyika mwezi Machi 2002. Pamoja na kupatikana kwa uongozi mpya *Tanzania Legion* bado

imegubikwa na vurugu zinazosababishwa na makundi ya wazee hususani wa Dar es Salaam wanaoupinga uongozi mpya.

Hata hivyo, Wizara yangu imeendelea kuchukua hatua kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Usalama wa Raia kuhakikisha kwamba *Tanzania Legion* inakuwa na utulivu unaohitajika na hatimaye kurejesha ruzuku iliyofutwa na *British Ex-Services League.* Hii ni pamoja na kuanzishwa kwa uchunguzi wa kipolisi kwa baadhi ya watendaji wanaotuhumiwa kwa ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za kuirejesha posho ya wazee hao; kama nilivyoliarifu Bunge lako Tukufu katika mkutano wa nane tarehe 29/6/2007, nikijibu swali la Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, Wizara yangu inaandaa mfuko maalum wa Maendeleo ya wazee wakiwemo wazee waliopigana vita ya pili ya dunia ili kuwawezesha kupata mikopo kwa ajili ya shughuli ya uzalishaji mali. Vile vile, Wizara inashughulikia utaratibu wa kuanza kutoa fedha za kujikimu kwa wazee waliothibitika kuwa hawana uwezo wala ndugu na jamaa wa kuwasaidia. Hivi sasa Serikali kupitia *TASAF* inafanya majaribio ya utekelezaji wa mpango huu katika Wilaya ya Chamwino Dodoma na Bagamoyo Pwani.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa hapa lakini nilitaka kusema kwamba majibu haya tumekuwa tunayapokea kila wakati, mimi hii ni safari yangu pili kuwa Mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tunajua kabisa kwamba hawa tunaowazungumzia ni wazee ambao wamezeeka uwezo wao umepungua. Kama kuna matatizo katika *Tanzania Leagion* je ni kwa nini Serikali isichukue nafasi yake kama Serikali kuingilia kati katika mgogoro ule? Hilo la kwanza. *(Makofi)*

La pili, nimewahi kusoma kwenye gazeti na ningejua leo kwamba swali hili litajibiwa ningeleta *cutting* hapa ndani ambayo inaionyesha Serikali ya Uingereza kupitia Ubalozi wake kwamba anasema, „msaada unaokuja kwa Serikali ya Tanzania katika msaada huo huo Serikali ya Tanzania iutumie kwa ajili ya kuwasaidia wazee ambao wamepigana vita kuu ya pili KAR, je Serikali inasema nini katika hilo na je, Serikali ipo tayari kupokea hiyo *cutting* ili iifanyie kazi“? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kweli swali hili limechukua muda mrefu kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi na Serikali ndiyo maana nimesema kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mambo ya Ndani na Usalama wa Raia tunaliingilia kati ili kuweza kuona kwamba hili swali linaisha. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali italichukulia kwa uzito wake ili kuhakikisha kwamba hili tatizo linaisha.

Swali la pili, Mheshimiwa Spika kuhusu Ubalozi wa Uingereza na msaada ambao wameutoa kama kweli msaada ulitolewa na maelekezo yalitolewa nadhani Serikali inajua sisi kama Wizara yetu mimi sewezi nikasema kama hilo agizo tumelipata, lakini kwa

sababu Serikali iko hapa inasikia, kama kuna maelekezo yoyote kutokana na huo msaada uliokuja basi Serikali itaangalia ili kuweza kuhakikisha kwamba wazee wanasaidiwa.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa John Samwel Malecela, swali la nyongeza!!

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Aah!! Aah!!

**SPIKA:** Hapana ahsante sana. Mheshimiwa Maige, wewe ni kijana tu, sasa sijui.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza ili kuonyesha kwamba pamoja na kwamba ni kijana lakini wazee ndiyo wazee wetu ndiyo waliotulea tunawaenzi sana.

Katika majibu ya Naibu Waziri amesema Serikali inaandaa mpango wa kuangalia namna ya kuwahudumia wazee hao.

Kwa kuwa wazee hao wako nchi nzima wametapakaa. Je, ina mpango wowote ambao imeuweka wa kuratibu na kupata takwimu zao sahihi kwamba ni kina nani na wako wapi kwa kuwa mazingira ya *Tanzania Legion* sasa hivi sidhani kama wanaweza wakawa na hiyo takwimu ya kuwajua wazee hao. Je, Serikali ina mpango gani wa kujua idadi yao na wako wapi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, Serikali inawafahamu wazee hawa waliopigana vita katika vita ile ya mwaka 1939-1945 na inajua wako wapi kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge kama atataka kujua kwamba ni wangapi na wanakaa wapi basi Wizara itamwandalia na itampatia ili aweze kufahamu wanakopatikana.

Na. 94

**Wananchi waliojenga Ubungo Kisiwani**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza:-

Kwa kuwa zaidi ya miaka sita iliyopita wananchi waliojenga kwenye eneo la Ubungo Kisiwani waliagizwa kujiandaa kuondoka katika maeneo hayo na wasiendelee na ujenzi au ukarabati wa nyumba, na kwa kuwa wananchi hao waliahidiwa kulipwa fidia:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kutowapa wananchi hao maelezo juu ya hatua zinazochukuliwa na wakati huo huo kutotimiza ahadi yake ya kuwalipa fidia kunawasababishia mazingira magumu kimaisha?

(b) Je, ni lini sasa Serikali itawalipa fidia wananchi hao?

(c) Je, Serikali haioni kwamba kuwaacha wananchi hao kuendelea kuishi karibu na mitambo ya kuzalisha umeme wa *TANESCO* ni hatari sana kwa maisha yao na kwa nini hatua za haraka zisichukuliwe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mwezi Desemba 2003 Serikali iliona umuhimu wa kuwahamisha wakazi wa jirani na eneo la matenki ya kuhifadhia mafuta ya *TANESCO Power Station* yaliyoko Ubungo kutokana na sababu za kiusalama baada ya kutokea ajali ya moto katika matenki hayo.

Hatua za kuthamini nyumba na mali nyingine ilifanywa na Idara ya Uthamini ya Manispaa ya Kinondoni kati ya mwezi Juni – Agosti 2004. Lengo la tathmini hiyo ilikuwa ni kujua thamani ya mali ya wananchi hao kwa lengo la kuwahamisha kutoka katika eneo hilo ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea endapo ajali ya moto itatokea katika matenki hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Ndelyanaruwa Keenja, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kutokuwapa wananchi maelezo juu ya hatua zinazochukuliwa na kutotimiza ahadi ya kuwalipa fidia wananchi kunawaweka katika mazingira magumu kimaisha.

Hata hivyo kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya utangulizi, nia ya Serikali ilikuwa kuwalipa wananchi hao fidia mapema ili wahame eneo hilo ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea endapo ajali ya moto itatokea. Serikali inapenda kuwahakikishia wananchi hao kuwa jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya fidia zinafanyika na pindi fedha zitakapopatikana wananchi hao watalipwa fidia ili wahame eneo hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, wananchi wa Ubungo Kisiwani watalipwa fidia na kutakiwa kuondoka mara fedha za kulipa fidia zitakapopatikana na kulipwa fidia zao.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inajua wazi kwamba kuwaacha wananchi hao kuendelea kuishi karibu na mitambo ya kuzalisha umeme ya *TANESCO* ni hatari sana kwa maisha yao. Ndiyo maana jitihada zinafanywa kupata fedha za fidia ili waweze kuhama haraka iwezekanavyo.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri sana ya Naibu Waziri yanayoonyesha kwamba Serikali inakubali kuwalipa fidia. Lakini tangu swali hili litungwe mpaka sasa yametokea mabadiliko makubwa sana pale Ubungo, imejengwa mitambo mikubwa sana ya kuzalisha umeme unayotoa joto, kelele na ambayo ni hatari zaidi kuliko ilivyokuwa.

Je, Serikali haioni kwamba kuna ulazima wa kuchukua hatua za haraka sana kuwapatia wale wananchi viwanja ili waanza kuandaa makazi yao waondoke katika eneo lile?

Pili, swali ni lini sasa wananchi hawa watalipwa fidia maana ananiambia Naibu Waziri ni fedha zitakapopatikana, anatarajia zitapatikana lini na kutoka wapi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo :-

Mheshimiwa Spika, Kweli ni mabadailiko makubwa yametokea katika maeneo hayo baada ya mitambo ya kuzalisha umeme kuongezeka kuwekwa pale katika maeneo ya Ubungo Kisiwani. Lakini pia Mheshimiwa Spika kama nilivyosema katika jibu la msingi pia kasi ya Serikali kutafuta fedha kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje ya nchi imeongezeka kwa kuzingatia hayo ambayo yanaendelea katika maeneo ya Ubungo Kisiwani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ni lini wananchi hawa watlipwa, niseme kwa dhati kwamba inakuwa vigumu kusema hasa ni mwezi, tarehe na mda gani na mwaka gani, lakini ambacho naweza kusema kuwahakikishia wananchi wa Ubungo Kisiwani na Watanzania kwa ujumla kwamba Serikali inatambua umuhimu wa wananchi hawa kuhama maeneo hayo kwasababu ya kulinda afya zao kwa kulinda maisha yao.

Mheshimiwa Spika, namuwmba Mheshimiwa Mbunge, tuendelee kuwashawishi wananchi waamini kwamba Serikali inalichukulia jambo hili kwa uzito mkubwa na kwa kweli juhudi mahususi zinaendelea kuhakikisha kwamba tunapata fedha ambazo kwa tathmini iliyofanyika mwaka 2004 ni zaidi ya bilioni 2 nukta 2 ili ziwezeshe kulipa fidia kwa wananchi hawa na hatimae waondoke wahame maeneo haya. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, tunamhakikishia Mbunge kwamba Serikali tunatambua na tunafanyia kazi suala hili kwa kiwango kikubwa sana.

Na. 95

**Ukosefu wa Umeme – Churuku, Kinkima, Jinjo na Jangalo – Kondoa**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kijiji cha Hamai, Wilayani Kondoa kimepatiwa umeme kupitia mradi wa *Electricity IV*:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika vijiji jirani vya Churuku, Kinkima, Jinjo na Jangalo kwa kuanzia na kijiji cha Churuku?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Contantine Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa umeme katika vijiji vya Churuku, Kinkima, Jinjo na Jangalo upo kwenye mpango mahususi wa Serikali wa usambazaji umeme vijijini. Hata hivyo kwa kuwa miradi ya umeme vijijini ni mingi, utekelezaji wake unafanyika kwa awamu kutegemea upatikanaji wa fedha. Tathmini za awali za kupeleka umeme katika vijiji hivyo imeshafanyika ambapo gharama za kupeleka umeme katika vijiji vya Churuku, Kinkima, Jinjo na Jangalo zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 530.Serikali inafanya jitahada za kupata fedha nyingi zaidi kwa ajili ya miradi ya umeme vijijini katika mwaka wa fedha 2008/2009, ili kuwezesha utekelezaji wa miradi mingi zaidi ya umeme vijijini vikiwemo vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Aidha namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa, katika majibu yake Naibu Waziri, amesema gharama ya kupeleka umeme katika vijiji nilivyovitaja ni shilingi milioni 530, na kwa kuwa, kiwango hicho ni kikubwa sana. Lakini natambua kwamba kijiji cha Churuku kiko karibu sana na kijiji cha Maya ambako ndiko umeme sasahivi umefika. Je, atakubaliana nami kwamba badala ya kungoja mradi huu utekelezwe kwa vijiji vyote vinne angeanza kwanza na Churuku mwaka kesho?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Degera Mbunge, kama ifuatavyo:-

Awali wakati mpango unaandaliwa wa utekelezaji wa mradi huo ilikuwa ni kufikisha huduma ya umeme katika vijiji ambavyo nimevitaja katika jibu la msingi. Na utekelezaji wake ulikuwa uende kwa pamoja kwasababu ya kuwafikishia wananchi wengi zaidi huduma hiyo. Lakini niseme kwa niaba ya Serikali, wazo la Mheshimiwa Mbunge, tunalipokea na tutalirudisha kwa Wataalamu wetu kushirikiana na Mamlaka zinazohusika

kuona kama tunaweza kutekeleza kwa kuanzia na kijiji kimoja kwanza badala ya kutekeleza kama vile ambavyo mwanzoni ilikuwa imepangwa. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Nakushukuru Mheshimiwa spika, kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwanza nianze kwa kuipongeza serikali kwa kupeleka transfoma kijiji cha Tuguli kata ya Iguguno. Je, Serikali itakuwa tayari kumpa *Regional Manager* wa singida shilingi milioni 10 ili kuwezesha kuunganisha umeme kwa wananchi wa Tumuli ambao wengi wameshafunga nyaya kwenye nyumba zao na wanangoja kuunganishiwa tu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Msindai, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Serikali imefanyia kazi uwezeshaji wa kukamilisha mpango wa kutoa huduma katika kijiji cha Tumuli. Kuhusu ombi la Mheshimiwa Mbunge kwamba, serikali imuwezeshe Meneja wetu wa *TANESCO* wa Mkoa wa Singida kumpa milioni 10, hili suala ni la kufanyia kazi Mheshimiwa Mbunge, tunamuahidi tutarudi kuangalia kama kwanza mpaka sasahivi pesa hiyo haijatengwa, maana inawezekana tukaongea kitu ambacho Mheshimiwa spika, pengine tayari kimeshatengewa.

Lakini nimuahidi kwamba yeye na mimi tutashirikiana kwa niaba ya Serikali kuona ni jinsi gani mradi huu unaweza kukamilika hivi karibuni. *(Makofi)*

Na. 96

**Hifadhi ya Saadani**

**MHE. RAMADHANI A. MANENO** aliuliza:-

Kwa kuwa Saadani imekuwa Hifadhi ya Taifa na mbuga pekee iliyo kandokando ya Bahari ya Hindi, na kwa kuwa wanyama hawanywi maji ya bahari, hali inayosababisha wakati mwingine wanyama kutoka na kwenda kutafuta maji maeneo wanakoishi watu, hivyo kusababisha madhara na usumbufu wa watu :-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mabwawa ndani ya hifadhi ili wanyama wasiende maeneo waishiyo watu ?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mbunge wa Chalinze kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa baadhi ya wanyamapori walioko kwenye Hifadhi ya Taifa ya Saadani kuna kipindi wanatoka kwenda kwenye maeneo nje ya hifadhi na wakati mwingine kwenda maeneo ya wananchi. Wanyamapori hutoka nje ya maeneo ya Hifadhi kwasababu mbalimbali ambazo ni pamoja na kutafuta chakula na maficho kwaajili ya usalama.

Katika kukidhi haja hizi, baadhi ya wanyamapori huhama kwenda kwenye maeneo mengine kufuata mahitaji hayo kwa kutumia mapito yao ya asili ambayo mengi yako nje ya Hifadhi na yamechukuliwa kuwa makazi na kwa shughuli nyingine za binadamu.

Mheshimiwa Spika, Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa kwenye Hifadhi ya Saadani kuna mabwawa ya maji 25 ambayo siyo ya asili. Jumla ya mabwawa yaliyopo upande wa Mkwaja ni 21. kati ya haya mabwawa 11 yana maji kwa kipindi cha mwaka mzima na 10 yanakauka wakati wa kiangazi. Upande wa Saadani, kuna mabwawa 4 ambayo pia yanakauka wakati wa kiangazi.

Aidha mto Wami ambao una maji mwaka mzima utaendelea kuwa chanzo cha maji ya uhakika kwa wanyamapori wa Hifadhi ya Taifa ya Saadani. Hivyo basi Serikali haina mpango wa kujenga mabwawa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani kwa sababu maji yaliyomo kwenye mabwawa na mto Wami yanakidhi mahitaji ya wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara kupitia Kitengo cha Ujirani Mwema cha Hifadhi ya Taifa ya Saadani kitaendelea kushirikiana na wanavijiji kwenye maeneo ambayo kuna tatizo la wanyama kutoka nje ya Hifadhi, ili kuweka mikakati ya jinsi ya kukabiliana na matatizo yanayosababishwa na wanyama waharibifu.

**MHE. RAMADHAN A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kwamba katika Hifadhi ya Saadani kuna mabwawa 4 ambayo hukauka wakati wa kiangazi, na upo ushahidi wa kipindi hiko cha kiangazi wanyama hutoka ndani ya hifadhi na kuelekea mto Wami na kusababisha uharibifu mkubwa na madhara makubwa kwa wananchi na uharibifu mkubwa wa mashamba ya wananchi.

Je, serikali ina mpango gani sasa, inafikiria nini juu ya kuwafidia wananchi waliopatwa na madhara ya wanyama waliokuwa wanapita kwenye maeneo yao hususan kwenye mashamba?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maneno kama ifuatavyo :-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2007/2008 Serikali imeangalia upya wananchi ambao mazao yao huharibiwa na wanyamapori. Hivyo basi Serikali imeagiza kuwa wananchi ambao mazao yao yataharibiwa na wanyamapori, ambao wana

mashamba zaidi ya hekta moja watalipwa kiwango cha shilingi laki moja. Lakini wananchi hao ambao mazao yao yameharibiwa na wanyama pori, wanatakiwa kutoa taarifa kwa uongozi wa vijiji, ili afisa maliasili wa Wilaya apate taarifa hiyo na tathmini ifanyike kuhakikisha kwamba shamba lile kweli limeharibiwa na wanyamapori na lina ukubwa wa zaidi ya hekta moja. Ndipo watakapolipwa fidia ya laki moja.

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Je, Mheshiwa Naibu Waziri anasemaje kwa orodha ambayo imeshapelekwa Wizarani kwake toka mwaka 2004 kwa wananchi walioharibiwa minazi yao katika Wilaya ya Pangani ambayo inapakana na Hifadhi ya Saadani ?

Je, Wizara iko tayari kuharakisha maombi hayo ya kulipa kifuta machozi yaruhusiwe ili wananchi wapate haki yao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohmed Rished Abdallah, kama ifuatavyo :-

Nilipokuwa Wilayani Pangani, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah aliongelea kuhusu suala hili. Na kwamba nilimwambia, tungeomba tupate hiyo orodha kwa sababu orodha ilikuwa bado haijafika Wizarani na bado sijaipata, tutakapoipata hiyo orodha tutaifanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 97

**Ushuru wa Vitalu vya Uwindaji**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeongeza Ushuru wa Vitalu pamoja na malipo ya wanyamapori wanaowindwa na wageni kwenye msimu wa uwindaji.

Je, Serikali itaongeza fedha kiasi gani kwenye fedha wanazotoa kwa Wilaya zinazozunguka maeneo hayo hasa ikizingatiwa kuwa wanapata hasara kubwa kutokana na uharibifu unaofanywa na wanyama hao kwenye maeneo husika ?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali imeongeza ada za vitalu na ada za wanyamapori wanaowindwa ili mapato yake yalingane na thamani ya rasilimali hiyo na mazingira yake na kwamba mapato hayo yawezeshe Serikali kukabiliana na ongezeko la gharama za usimamizi na uendeshaji katika uhifadhi wa wanyamapori nchini.

Mheshimiwa Spika, mgawo wa asilimia 25 ya fedha kwa Halmashauri za Wilaya hutokana na mgao wa fedha zinazopelekwa Hazina kutokana na ada za wanyamapori waliowindwa katika vitalu vilivyotengwa kwa shughuli za uwindaji wa kitalii. Sambamba na hilo, Wizara yangu, imetoa mwongozo wa matumizi ya fedha hizo ambapo asilimia 60 ya fedha hizo zinatakiwa kusaidia miradi ya Maendeleo ya wananchi kwenye vijiji uwindaji unapofanyika na asilimia 40 kuendeleza uhifadhi wa wanyamapori katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuongeza kiwango cha sasa cha asilimia 25 ya mgawo wa mapato kutokana na uwindaji wa kitalii kwa Halmashauri za Wilaya, kwa kuwa mapato ya Wilaya yataongezeka pia, kwa uwiano sawia, kulingana na ada mpya, aina na idadi ya wanyamapori watakaowindwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa pamoja na asilimia 25 ya mgawo wa kwa Halmashauri unaotokana na uwindaji wa Kitalii, makampuni ya uwindaji wa kitalii huchangia katika miradi ya Maendeleo ya vijiji vinavyozunguka maeneo hayo. Kwa mfano mwaka 2005:

Kampuni ya Uwindaji ya *Old Nyika Hunting Safaris Ltd.* Imechangia jumla ya shilingi milioni 3,492,840.00 katika miradi ya Maendeleo katika vijiji vya Ngereiyani na Tingatinga.

Kampuni ya Uwindaji ya *Nothern Hunting Enterprises Ltd.* Imechangia jumla ya shilingi milioni 7,579,000.00 katika miradi ya Maendeleo ya vijiji vya Sinya, Vilima Vitatu na Mwada.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Ningependa kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyotoa na kuipongeza Serikali kwa makusanyo mazuri ya mapato wanyamapori waliokusanywa.

Ningependa kuuliza kwa kuwa, mwaka jana 2006/2007 hatukupata asilimia 25, Halmashauri hazikupata asilimia 25, Je, Serikali inasemaje kwa sasa kwa ajili ya hizo fedha ili wananchi waweze wakatumia katika miradi yao? Pili, kwa kuwa, kuna Halmashauri zilizogawanywa na tulikuwa tunapata fedha kwa pamoja. Je, Serikali iko tayari sasa kugawa zile fedha katika Halmashauri hizo ili isiende upande mmoja?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Laizer kama ifuatavyo:-

Kabla ya kujibu maswali yake ya nyongeza Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Laizer kwa jinsi ambavyo anafuatilia kwa makini kabisa masuala yanayohusu wananchi wa jimbo lake la Longido.

Mheshimiwa Spika, mgawo wa asilimia 25 kwa Halmashauri za Wilaya ambapo uwindaji wa kitalii huwa unafanyika huwa unatolewa. Na kwa kuwa, Wilaya ya Longido ni Wilaya mpya, awali ilikuwa katika Wilaya ya Monduli.

Hivyo basi, mgawo wa asilimia 25 kwa ajili ya Halmashauri ya Mongduli ilikuwa inatolewa. Ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, hapa ninazo takwimu kwamba mwaka 2006/2007 ilitolewa kiasi cha shilingi milioni ishirini na nne mia nane themanini elfu, mia tatu na ishirini na tano (Shilingi 24,880,325/=) kwa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli.

Lakini kama alivyouliza mwenyewe katika swali lake la nyongeza la pili, kwamba kwa kuwa, mwaka huu wa fedha Halmashauri ya Wilaya ya Longido imeanza kupata Bajeti yake hivyo basi tumeagiza pia kwamba mgawo wa asilimia 25 unaotokana na mapato ya uwindaji wa kitalii katika vitalu ambavyo viko katika Wilaya ya Longido vitapelekwa katika Wilaya ya Longido.

Na. 98

**Ujenzi wa Barabara za Mikoa**

**MHE. MWADINI ABAS JECHA (K.n.y. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA)** aliuliza:-

Kwa kuwa ni nia ya Serikali kuunganisha nchi yetu kwa barabara; na kwamba kwa kuanzia Serikali ingejenga angalau barabara za Mikoa:-

Je, ni mikoa mingapi katika nchi yetu tayari imeunganishwa kwa barabara za uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDO MBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Spika niruhusu niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi na Wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa kunimwagia kura ambazo ni sawasawa na mvua za El Ninyo na kuniwezesha kupona katika lile kundi la vifo, nawashukuru sana Mungu awababriki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundo Mbinu, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya nchi yetu inaunganishwa na barabara ambazo zipo katika mfumo wa kanda kuu tisa ambazo ni kama ifuatavyo:-

1.Kanda ya *TANZAM* ambayo inaanzia Dar es Salaam hadi Tunduma yenye urefu wa kilometa 1,324. Barabara za kanda hii zinaunganisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa na Mbeya kwa barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami.

2.Kanda ya Kaskazini Mashariki ambayo inaanzia Chalinze kupitia Tanga,/Moshi hadi Arusha na Himo-Marangu hadi Tarakea.Taveta yenye urefu wa kilometa 950. Barabara za kanda hii zinaunganisha mikoa ya Pwani, Tanga, Kilimanjaro na Arusha kwa barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami.

3.Kanda ya Kati ambayo inaanzia Morogoro hadi Mwanza kupitia Dodoma, Singida na Shinyanga yenye urefu wa kilometa 1,584. Barabara za kanda hii zinaunganisha mikoa ya Morogoro, Dodoma, Singida, Shinyanga/Tabora na Mwanza. Sehemu kubwa ya barabara za ukanda huu takribani kilometa 1,344 zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Sehemu iliyobakia kiasi cha kilometa 240 kati ya Dodoma na Shelui zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami.

4.Kanda ya Ziwa inayoanzia Sirari hadi Mutukula kupitia Mwanza yenye urefu wa kilometa 1,019. Barabara za Kanda hii zinaunganisha mikoa ya Mara, Mwanza na Kagera. Kiasi cha kilometa 712 za ukanda huu zimejengwa kwa kiawango cha lami na takribani kilometa 220 zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha maandalizi ya ujenzi wa kilometa 92 kati ya Usagara na Geita kwa kiwango cha lami yanaendelea.

5. Kanda ya Kaskazini inayoanzia Iringa hadi Namanga kupitia Dodoma na Arusha yenye urefu wa kilometa 1,067. Barabara za kanda hii zinaunganisha mikoa ya Iringa, Dodoma, Manyara na Arusha. Sehemu kubwa ya barabara za ukanda huu zimejengwa kwa kiwango cha changarawe hasa kuanzia Iringa kupitia Dodoma hadi Manyara (Minjingu). *(Makofi)*

Sehemu ndogo ya iliyoanzia Minjingu hadi Arusha ndiyo imejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha maandalizi ya ukarabati wa kilometa 105 za barabara kati ya Arusha na Namanga kwa kiwango cha lami yapo katika hatua za mwisho.

6. Kanda ya Pwani Kusini Mashariki inayoanzia Dar-es-Salaam hadi Mingoyo kupitia Kibiti na Lindi yenye urefu wa kilometa 508. Barabara za kanda hii zinaunganisha mikoa ya Dar-es-Salaam, Pwani, Lindi na mji wa Mingoyo. Kiasi cha

kilometa 351.5 za ukanda huu zimejengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 96.5 zinaendelea kujengwa. Aidha maandalizi ya ujenzi wa kilometa 60 za barabara kati ya Ndundu na Somanga yanaendelea.

7. Kanda ya Kusini inayoanzia Mtwara hadi *Mbamba Bay* kupitia Mingoyo, Masasi na Tunduru yenye urefu wa kilometa 1,024. Barabara za kanda hii zinaunganisha mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma. Sehemu kubwa ya barabara za ukanda huu zimejengwa kwa kiwango cha lami yanaendelea na yapo kwenye hatua mbalimbali

8.Kanda ya Kati Magharibi inayoanzia Mbeya hadi Nzega kupitia Chunya, Makongolosi, Rungwa, Ipole, Tabora hadi Nzega yenye urefu wa kilometa 1,201. Barabara za kanda hii zinaunganisha mikoa ya Mbeya na Tabora. Barabara za ukanda huu zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na udongo. Maandalizi ya kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami yameanza na yapo hatua mbalimbali.

9. Kanda ya Magharibi inayoanzia Tunduma hadi Nyakanazi kupitia Sumbawanga, Mpanda, Kigoma na Kasulu yenye urefu wa kilometa 1,286. Barabara za kanda hii zinaunganisha mikoa ya Mbeya, Rukwa na Kigoma. Barabara za ukanda huu zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na udongo. Maandalizi ya kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami yameanza na yapo kwenye hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na upembuzi yakinifu, usanifu wa awali na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuzifanyia ukarabati na matengenezo barabara zote za mikoa zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya ili ziweze kupitika mwaka mzima. Barabara za mikoa zina urefu wa kilometa 24,700 na asilimia 98.8 zimejengwa kwa kiwango cha changarawe na udongo na asilimia 1.2 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Barabara za mikoa zitaendelea kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe na baadhi kupandishwa hadi kufikia barabara za lami kulingana na uwezo Serikali kupitia Mpango wa *Transport Sector Investiment (TSIP).*

**MHE. HAZARA P. CHANA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na jitihada kubwa ambazo zinafanyika upande wa Miundo Mbin. Ningependa kujua hatma ya barabara inyounganisha Mkoa wa Iringa na Dodoma?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDO MBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundo Mbinu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge wa Viti Maalum na Mjumbe wa Kamati Kuu na nina mpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu *(Makofi).*

Kama nilivyoeleza kuhusu barabara za kanda ya Kati ambayo kanda inayotoka Iringa, Dodoma kwenda mpaka Babati – Minjingu, kwamba maandalizi yanaendelea. Tunategemea kwamba Barabara kati ya Iringa na Dododma yale maandalizi tayari tutakamilisha ili sasa tuwe tuna kazi ya kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kama ilivyoahidiwa.

Kwa hiyo, ninataka niwahakikishie Waheshimiwa kwamba barabara hiyo iko katika *priority list* ya barabara ambazo zitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami mara tu baada ya kukamilisha kazi za awali ambazo zinakamilika mwaka huu wa fedha. Vilevile upatikanaji wa fedha ambazo zinaendelea kutafutwa.

Na. 99

**Ubovu wa Barabara ya Hungumalwa, Shilima, Kikubiji - Itongoitale**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Sera ya barabara ni kufungua njia za Wilaya kwa Wilaya; na kwa kuwa, barabara ya Hungumalwa, Shilima, Kikubiji hadi Itongoitale ni mbovu sana:-

Je, Serikali itatengeneza lini barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDO MBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundo Mbinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Hungumalwa (N'gwamhaya) – Shilima – Kikubiji – Itongoitale yenye urefu wa kilometa 51 ni Barabara ya mkoa. Barabara hii inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Mwanza.

Barabara hii imekuwa ikipata matengenezo mbalimbali kulingana na upatikanaji wa fedha. Sehemu kubwa ya barabara hii (85%) ipo kwenye hali nzuri baada ya kupata matengenezo ya sehemu korofi *(Spot improvement)* mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2007/2008, barabara hii imetengewa jumla ya shilingi 70.536 milioni kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ambayo ni kuchonga barabara pamoja na kuweka tabaka la changarawe na kuzibua mifereji.

Aidha, jumla ya shilingi 80 milioni zimetengwa kwa ajili ya matengenezo makubwa. Matengenezo yanatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Novemba 2007 na yanatarajiwa kukamilika katikati ya mwezi Januari 2008. Baada ya matengenezo hayo kukamilika barabara hii itaweza kupitika kwa urahisi kwa kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* itaendelea kuifanyia matengenezo barabara hii, ikiwa ni pamoja na kuweka tabaka jipya la changarawe kulingana na fedha zitakavyopatikana mwaka hadi mwaka.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize swali kama lifuatavyo:-

Kwa kuwa, barabara ya Magu inapita Ngudu mpaka inaelekea Hungumalwa ambayo ndio inayoonesha maeneo kwa vijiji ambavyo nimevitaja, iliwekwa katika mpango huu wa *PPR*. Hadi leo ninavyozungumza hapa kazi hiyo haijaanza, sasa Mheshimiwa Spika, naomba Waziri leo anieleze kazi hiyo itaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDO MBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundo Mbinu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mwanza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara aliyoitaja iko katika mpango wa *PMMR* na tayari mchakato unaoendelea ni kukubaliana kati ya wafadhili na sisi kuhusu mkandarasi ambaye kimsingi ameshajulikana kuwa atakuwa nani.

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea sasa katika barabara hii, ni taratibu za kawaida za Mfadhili wa barabara hii kumwidhinisha ili sasa tuweze kuanza hiyo kazi ya ujenzi. Tuandikiane mkataba kwa hiyo nina hakika kwamba baada ya kipindi si kirefu kazi hizo zitaanza chini ya *PMMR*.. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kama uliota, kwamba nilikuwa napenda kufahamu kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa amefanya mizunguko ya kuangalia barabara mbovu za nchi hii na mambo mengine. Je, amewahi kupita barabara ya Nzega kwenda Tabora na Arusha kwenda Manyarara na Sumbawanga kwenda Mpanda akajionea zilivyo mbovu kiasi kwamba ni barabara zinazohitajika sana kwa wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ndiyo ni kweli kwamba nimeshapita barabara zote hizo na kwa kweli hakuna barabara yoyote ya mkoa au barabara kuu nchi hii ambayo sijapita. Kwa hiyo, naelewa hali ya barabara anazozitaja na Serikali imekuwa ikieleza hapa mipango yake ya kukarabati au kutengeneza barabara hizo. Kama nilivyoeleza kwenye jibu langu lililopita kila ukanda tuna mkakati wa kujenga barabara na ndiyo maana nasema kwamba sisi tumejipanga kama ambavyo hata Mheshimiwa Rais amesema kutekeleza ilani ya uchaguzi kuhusu barabara. Kwa hiyo, kazi inaendelea na mwaka hadi mwaka tutakuwa tunaleta programu ya kuonyesha tutatengeneza barabara gani au tutakarabati barabara gani.

Na. 100

**Mapato ya Safari za Anga**

**MHE. IBRAHIM M. S ANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haina sheria yake yenyewe kuhusu udhibiti wa usalama na usafiri wa Anga, hivyo kutumia Sheria ya Tanzania *Civil Aviation Act*, 1977, na Tanzania *Civil Aviation Authority*, 2003 ambazo ni za Muungano na kwa kuwa, ndege zote zinazo *overfly* hutoa malipo ambapo mwaka 2005/2006 Serikali ilikusanya shilingi bilioni 5 *(sbn):-*

(a) Je, kiasi gani kilikusanywa katika mwaka 2006/2007?

(b) Je, Tanzania Zanzibar kama mdau halali wa *TCAA* ilipata mgao kiasi gani kutokana na fedha zilizokusanywa mwaka 2005/2006?

(c) Je, ni Wazanzibar wangapi na kwa majina wanawakilisha katika bodi ya *TCAA*?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali hili naomba nichukue nafasi hii niwashukuru wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kunipa kura za kutosha kuwa Mjumbe wa *NEC* na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi na Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa kwa kunipitisha kwa kishindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, mapato yaliyokusanywa kutokana na huduma zilizotolewa kwa Ndege zilizoruka kwenye anga za juu la nchi yetu (*Over Flying Aircraft)* ni shilingi bilioni 5.9.

(b) Mheshimiwa Spika, mapato yatokanayo na ada ya *Over Flying* ni moja ya mapato ya mamlaka ya usafiri wa anga na hutumika katika shughuli za uendeshaji na pia shughuli za Maendeleo za mamlaka. Kwa sasa, mamlaka haipati ruzuku kutoka Serikalini wala Serikali haipati sehemu yeyote ya mapato ya mamlaka ya usalama wa usafiri wa anga hayagawanywi kwa misingi ya Tanzania Bara au Tanzania Zanzibar, bali hutumika katika shughuli za uendeshaji wa shughuli za Maendeleo za mamlaka. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, kiasi cha shilingi milioni 379 zilitumika katika uwekezaji na uendeshaji kwenye viwanja vya ndege vya Zanzibar na Pemba.

(c) Katika Bodi ya Mamlaka ya usafiri wa Anga ina wajumbe sita akiwemo Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka. Kati ya wajumbe hawa Wazanzibar ni wawili nao ni Bwana Mbwana Juma Mbwana, ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi na Mheshimiwa Subaiba Edington Kissassi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa Maswali umepita na maswali yamepita. Matangazo kwanza nasikitika kutoa tangazo la tanzia wenzetu Waheshimiwa Yahaya Kassim Issa na Issa Kassim Issa, wamefiwa na baba yao mzazi leo asubuhi na wameondoka kwenda kushughuli shughuli hiyo. Ofisi iko nao na wanashirikiana ili kuweza kuchangia katika kila hatua kadri ambavyo kanuni zetu zinavyoruhusu. Tunaomba Mwenyezi Mungu amuweke mzee wetu huyu mahala pema peponi Amina.

Kuhusu wageni, kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Esther Nyawaza, ni bi Amina Kimariyo karibu sana. Pia Waheshimiwa Wabunge tunao maafisa mipango 52 wa Wilaya, miji, Manispaa na Majiji ambao wanahudhuria mafunzo ya utayarishaji wa Bajeti wapo hapo Dodoma na leo wamechukua fursa kuja Bungeni. Ningeomba ndugu zangu maafisa mipango msimame pale mlipo ili Waheshimiwa Wabunge wawatambue. Karibuni sana tunawatakia mafanikio katika kazi zenu sisi Waheshimiwa Wabunge wote. Aidha tunawatakia semina njema itakayoleta tija mtakaporejea katika sehemu zenu za kazi, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ponsiano Nyami anaye mgeni wake Mheshimiwa Analory Choya ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa CCM wa wilaya ya Biharamulo na alikuwa Mbunge wa Biharamulo katika Bunge la kipindi kilichopita, naomba asimame. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ameir Ali Ameir Mbunge wa Fuoni ameniomba nimtambulishe mgeni wake ambaye ni Ndugu Shehe Hamad ni Mwenyekiti wa Wazazi wilaya ya Micheweni, yule pale anapunga mkono karibu sana. Waheshimiwa Wabunge leo saa saba mchana kutakuwa na ufunguzi wa Maonyesho kuhusu asali katika uwanja wa tafrija za Wabunge. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe anawaalika Waheshimiwa Wabunge wote kushiriki katika ufunguzi huo. Hakunidokeza hapa kama kutakuwa na zawadi ya asali au vipi lakini ni vizuri mfike mjionee wenyewe.

Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* Mheshimiwa John Momose Cheyo, anaomba Wajumbe wote wa Kamati ya *PAC*, Kamati ya Hesabu za Serikali mkutane leo tarehe 7 Novemba, 2007 saa saba kamili ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa Omar Kwaangw' Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii anaomba wajumbe wote wa Kamati yake ya Huduma za Jamii, mkutane kuanzia saa nne na nusu asubuhi katika ukumbi wa Pius Msekwa. Nadhani mnakutana na wadau wa masuala mbalimbali ya huduma za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mgana Msindai, Mwenyekiti wa Hesabu za Serikali za Mitaa anaomba leo tarehe 7 Novemba, 2007 saa tano asubuhi wajumbe wote wa Kamati *LAAC* mkutane ukumbi Na. 219.

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira ameniomba niwatangazie wajumbe wote wa Kamati ya Maliasili na Mazingira kwamba kutakuwa na kikao leo saa tano asubuhi katika ukumbi Na. 227 jengo la utawala gorofa

ya pili. Kwa hiyo, wajumbe wote wa Kamati ya Maliasili na Mazingira mkutano ni saa tano asubuhi ukumbi 227.

Waheshimiwa Wabunge mnaombwa nyote bila kukosa kuchukua fomu za tamko la viongozi wa umma kuhusu mali na madeni hili ni suala la Kikatiba na mwisho wa kurejesha fomu hizo zikiwa zimejazwa kikamilifu ni tarehe 31 Desemba, 2007 kwa hiyo hii ni nafasi nzuri ya kupata hiyo fomu kuijaza na kuirejesha katika ofisi ya Spika kabla ya tarehe 31 Desemba, 2007.

Mwaka jana mnamkumbuka baadhi yetu mlipuuzia hili suala na mkapitiliza kidogo, sasa Spika alikuwa rahimu sana mwaka jana. Mwaka huu sina huruma hata kidogo, asiyewasilisha fomu za mali na madeni kufikia tarehe 31 Desemba, 2007 basi hatua za kawaida ambazo zinaathari kubwa sana kwa Mbunge itabidi zifuate. *(Makofi)*

Mwisho Waheshimiwa Wabunge wote, nitakuwa kama mtovu wa fadhila kama sitawashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wote wakiwa ni wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, kwa kumwezesha Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, kupata kura ambazo zinalingana na kiwango cha mke wa Spika wa Bunge hili Tukufu. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kura zenu nyingi na mmeniunga mkono na hii imenipa nguvu na imani kubwa kwenu kwamba mnaniunga mkono. Sasa nitajizatiti upya kuyakabili majukumu yangu kutokana na nguvu mliyonipa. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na *Order Paper*. Katibu Shughuli inayofuata.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kwa Mwaka 2006

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika**,** kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu naomba kuwasilisha taarifa na Maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kwa Kipindi cha Mwaka 2006. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kuendelea vyema na vikao vyetu vya Bunge vya kujadili masuala mbalimbali ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naomba niitumie nafasi hii kwa niaba ya Kamati yangu kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wetumpya wa CCM Taifa; Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa

Zanzibar kuchaguliwa kuwa makamu Mwenyekiti wa CCM taifa upande wa Tanzania Visiwani; Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa upande wa Bara na Mheshimiwa Yusuph Ally Makamba, kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa CCM Taifa. Pongezi pia kwa Waheshimiwa Naibu Katibu Wakuu wote wawili wa CCM wa Bara na yule wa Visiwani, pamoja na wakuu wote, Makatibu wote wa idara bila ya kuwasahau Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kuingia kwenye na wale waliochaguliwa kuingia kwenye Kamati Kuu nawapongeza sana kwa ushindi wa mkubwa walioupata katika uchaguzi mkuu wa CCM wa kutafuta viongozi wa nafasi mbalimbali katika Chama.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba niwapongeze Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu waliochaguliwa nao katika kinyang'anyilo hicho ambao ni Mhe. Andrew John Chenge, Waziri wa Miundombinu; Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari na Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Naibu Mawaziri wa Wizara ya Miundombinu na vilevile Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Anne Kilango Malecela pamoja na Mheshimiwa Richard Nyaulawa, hao wote ni wajumbe Kamati ya Miundombinu, ambao wamechaguliwa kuingia kwenye *NEC* kwa ushindi wao wa kishindo kwa kuchaguliwa kwao kuwa Wajumbe wa *NEC*.

Mheshimiwa Spika, lakini uniruhusu vilevile kwa nafasi yangu kama Mwenyekiti wa Wabunge wa mkoa wa Singida naomba sana niwapongeze Wabunge wa Singida Mheshimiwa Kapt. Mstaafu John Chilligati kwa kuchaguliwa kuingia kwenye *NEC* na kwenye Kamati Kuu na kuwa mkuu wa Idara, dada yetu Mheshimiwa Diana Chilolo kuwa Mjumbe wa *NEC* bila kumsahau Amos Makala ambaye ameingia kwenye *NEC* na sasa amepewa dhamana nyingine kwenye Kamati Kuu. Wote hawa na wengine wote naomba niwapongeze sana wengine ambao nimewasahau au sikuwataja basi naomba pia niwapongeze:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 88(11) Toleo la Mwaka 2004 ya Kanuni za Bunge, naomba kutoa taarifa ya shughuli za Kamati ya Miundombinu kwa kipindi cha mwaka 2006. Kamati hii ni mojawapo ya Kamati 13 za Kudumu za Bunge na imeundwa rasmi mwaka 2003. Kamati hii ni ya kipotfolio na inashughulikia wizara ya Miundombinu. Awali Kamati hii ilikuwa inashughulika na Wizara mbili zilizokuwa za Ujenzi na Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati hii yameainishwa kwenye Kanuni ya 103B (2) ya mwaka 2004 kama ifuatavyo:-

Kushughulikia Bajeti za Wizara hizo.

Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, ambayo chanzo chake ni Wizara hiyo.

Kushughulikia taarifa za kila mwaka za Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hiyo.

Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hiyo kwa Mujibu wa Ibara ya 63(3) (b) ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati, ningependa kwanza kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati hii ya Miundombinu kama ifuatavyo:-

Wajumbe hao ni Mheshimiwa Mohammed H. Missanga - Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Joyce M. Masunga, Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Khadija S. Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Pascal C. Degera, Mheshimiwa Bakari S. Faki, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, na Mheshimiwa Ephraim N. Madeje.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Balozi Getrude I. Mongella, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Sigfrid S. Ng'itu,

Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa Mwaka A. Ramadhan, Mheshimiwa Prof. Philemon M. Sarungi, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Hafidh A. Tahir, na Mheshimiwa Godfrey W. Zambi.

Mheshimiwa Spika, Kazi zilizotekelezwa kwa Mwaka 2006, Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004 Kanuni ya 90 (1) na 103B (2) (iv), Kamati ya Bunge ya Miundombinu ilijipangia ratiba ya kazi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha mwaka 2006. Hata hivyo baadhi ya kazi tulizojipangia hazikutekelezeka kwa sababu ya ufinyu wa bajeti. Majukumu hayo ni pamoja na:-

Kujadili Bajeti, na kwamba tarehe 1 - 2 Juni, 2006 Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Miundombinu kwa Mwaka 2005/2006 na kujadili Makadirio na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2006/2007.

Kutembelea miradi iliyo chini ya *Potifolio* ya Kamati ya Miundombinu. Tarehe 13 Machi, 2006 Kamati ilitembelea na kupata Taarifa ya Utendaji kutoka kwa *Air Tanzania Holdings Corporation (ATHCO)* na Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL).*

Tarehe 14 Machi, 2006 Kamati ilitembelea na kupata Taarifa ya Utendaji kutoka kwa Wakala wa Ujenzi Tanzania *(TBA),* Baraza la Taifa la Ujenzi *(NCC)* na Wakala wa Barabara *(TANROADS).*

Tarehe 15 Machi, 2006 Kamati ilitembelea na kupata Taarifa ya Utendaji kutoka kwa Bodi ya Mfuko wa Barabara *(RFB),* Bodi ya Usajili wa Wahandisi *(ERB)* na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi *(CRB).*

Tarehe 16 Machi, 2006 Kamati ilitembelea na kupata Taarifa ya Utendaji kutoka kwa Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa *(NBMM)*, Bodi ya Usajili wa Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi *(AQSRB)* na Wakala wa Ufundi na Umeme*(TEMESA).*

Tarehe 20 Machi, 2006 Kamati ilitembelea na kupata Taarifa ya Utendaji kutoka kwa Shirika la Simu Tanzania *(TTCL).*

Tarehe 23 Mei, 2006 Kamati ilitembelea na kupata Taarifa ya Utendaji kutoka kwa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam *(DMI).*

Tarehe 24 Mei, 2006 Kamati ilitembelea na kupata Taarifa ya Utendaji kutoka kwa Shirika la Reli la Tanzania na Zambia *(TAZARA)* na Shirika la Usafiri Dar es Salaam *(UDA).*

Tarehe 25 Mei, Kamati ilitembelea na kupata taarifa ya Utendaji ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT).*

Kuanzia tarehe 5 -7 Oktoba, 2006 Kamati ilitembelea shughuli za *Swissport Tanzania* katika viwanja vya ndege vya *JNIA, Dar es Salaam* na *KIA, Kilimanjaro.*

Kamati ilitembelea miradi ya viwanja vya ndege vya Arusha na Moshi tarehe 8 Oktoba, 2006 na tarehe 15 Oktoba, 2006 Kamati ilitembelea mradi wa uwanja wa ndege wa Mwanza.

Kuanzia tarehe 10 – 14 Oktoba, 2006 Kamati ilitembelea miradi ya barabara za Dar - Morogoro – Dodoma, Manyoni – Singida, Singida – Shelui – Nzega – Shinyanga, Shinyanga – Mwanza – Usagara – Geita, Buzirayombo – Kyamiorwa na Bukoba.

Tarehe 15 Oktoba, 2006 Kamati ilitembelea miradi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)*, Mwanza.

Tarehe 25 Oktoba, 2006 Kamati ilitembelea eneo la Ujenzi wa Daraja la Kigamboni.
Kupokea na kujadili Miswada ya Sheria. Tarehe 18 - 19 Oktoba, 2006 Kamati ilipokea na kujadili Muswada wa Sheria wa *The Universal Communication Access Service Act, 2006.*

Mheshimiwa Spika, Kuridhia Maazimio, kwa kipindi cha mwaka 2006 Kamati imeweza kujadili na kuridhia Maazimio 4 ya Mikataba ya Kimataifa ambayo ni:-

*International Convention on facilitation of International Traffic, 1995:*
*International Air Service Transit Agreement (IASTA) of 1944:*

*Ratification of the Convention on Prevention of Maritime Pollution by Dumping of Wastes and Other Matters, 1972:* na

*International Convention for the Prevention of Pollution from Ships (Marpol 1973/78).*

Kujadili Taarifa na Hesabu za Taasisi za Serikali zilizokaguliwa:

Tarehe 29 Mei, 2006 Kamati ilipitia na kujadili Taarifa ya Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Kampuni iliyomilikishwa mali zilizokuwa za *ATC (ATHCO)* na *SIMU 2000 LTD.*

Tarehe 30 Mei, 2006 Kamati ilipitia na kujadili Taarifa ya Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Usajili wa Wasanifu na Wakadiriaji Majengo*(AQRSB)* na Bodi ya Usajili Wakandarasi *(CRB).*

Tarehe 31 Mei, 2006 Kamati ilipitia na kujadili Taarifa ya Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Usalama wa Anga Tanzania *(TCAA).*

Tarehe 5 Juni, 2006 Kamati ilipitia na kujadili Taarifa ya Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Majini, Anga na nchi Kavu *(SUMATRA).*

Tarehe 17 Oktoba, 2006 Kamati ilipitia na kujadili Taarifa ya Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam *(DMI)* na Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa *(NBMM).*

Tarehe 20 Oktoba, 2006 Kamati ilipitia na kujadili Taarifa ya Utendaji na Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania *(TCRA).* Kamati Kukutana na Wadau mbalimbali.

Tarehe 7 Julai, 2006 Kamati ilikutana na Wadau mbalimbali wa Makampuni ya Simu za Mikononi Tanzania, ambao ni *VODACOM, CELTEL, TIGO* na *ZANTEL* ili kuweza kupata maoni yao juu ya Muswada wa Sheria wa *The Universal Communication Access Service Act,2006.*

Tarehe 27 Oktoba, 2006 Kamati iliweza kukutana na watendaji wa *ATCL* na kupokea taarifa ya utendaji na utekelezaji wa zoezi la ubinafsishaji. Semina za kujielimisha kuhusu masuala yahusuyo Potifolio ya Miundombinu.

Tarehe 17 Machi, 2006 Kamati ilipata Semina kuhusu Wakandarasi na Miundombinu iliyotolewa na Chama cha Wakandarasi Wahandisi *Tanzania Civil Engineering Contractors Association (TACECA).*

Kamati ya Miundombinu iliratibu semina kwa ajili ya Wabunge wote kuhusu wajibu na majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* iliyofanyika tarehe 1 Aprili, 2006, Dodoma.

Kamati ilipata Semina kuhusu Muundo na Majukumu ya Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA)* tarehe 15 Mei, 2006.

Tarehe 22 Mei, 2006 Kamati ilipata Semina iliyoendeshwa na *Simbanet* kuhusu umuhimu wa *ICT*.

Tarehe 20 Oktoba, 2006 Kamati ilipata Semina ya Uboreshaji mtandao wa Mawasiliano Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Ukosefu wa fedha za kutosha kuendeshea shughuli za Kamati husababisha baadhi ya ratiba za kazi za Kamati kutotekelezeka. Kamati hushindwa kuwafikia walengwa au kujionea hali halisi ya miradi iliyo chini ya Mashirika au Asasi inazozisimamia na hivyo kutegemea ufadhili wa Wizara husika, jambo ambalo linasababisha Kamati kushindwa kuthibitisha thamani ya miradi hiyo *(Value for Money).*

Ili kuondoa mkanganyiko wa Kamati mbili za Bunge kusimamia Wakala moja inashauriwa kuwa Kamati yenye *Portifolio* ya Wizara ambayo inasimamia Wakala/Taasisi ndiyo ishughulikie Taarifa za Utendaji za Mashirika/Taasisi/Wakala husika ili kuleta ufanisi zaidi wa kazi za Kamati. Hii itaondoa usumbufu kwa Mashirika/Taasisi/Wakala hizo kujadiliwa na Kamati mbili zilizo na portifolio tofauti.

Kamati inashauri uteuzi wa Wenyeviti wa Wakala *(Agencies)* wa Bodi mbalimbali uzingatie wingi wa kazi walizonazo Makatibu Wakuu ili kuepukana na tatizo la vikao vya Bodi kutofanyika kwa wakati unaotakiwa.

Kamati inaishauri Serikali ifanye jitihada kuendeleza Miundombinu iliyopo katika Mikoa ya pembezoni kwa mfano; Mikoa ya Kusini na kuwezesha matumizi ya rasilimali zilizoko huko kama vile Makaa ya Mawe ya Mchuchuma, Gesi ya Songosongo na *Mnazi-Bay* ili kuinua uchumi wa nchi.

Huduma za Mawasiliano, Kamati inashauri kuwa Kampuni za Simu za Mikononi yaani *Celtel, Mobitel*, *Vodacom* na *Zantel* zipunguze gharama ili kuwawezesha Wananchi wengi kumudu huduma hiyo, kwani imebainika gharama wanazobebeshwa Wateja bado ni kubwa ikilinganishwa na baadhi ya nchi jirani.

Kamati inashauri Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (*TCRA)* iweke mkazo kwa Makampuni ya Simu za Mikononi ili yawe na utaratibu wa ushirikiano katika kuchangia gharama za uendeshaji *(cost sharing*) hasa kwenye minara kwa ajili ya kupunguza gharama za uendeshaji na kuhifadhi mazingira.

Shirika la Posta Tanzania linaelekea kuelemewa na ushindani wa soko huria kutokana na kudhoofika kifedha baada ya kurithi madeni makubwa ya lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania; Benki ya Posta; na nakisi ya Mfuko wa Pensheni ya wafanyakazi wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika ya Mashariki *(EAP&T).*

Ama madai ya kodi, riba na tozo ya adhabu ya *TRA* yasiyozingatia hali halisi ya mapato ya Shirika yamezidi kulizamisha kimapato. Kamati inashauri Serikali ichukue hatua za haraka za kulinusuru Shirika hili kwani huduma zake bado ni muhimu kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninashangaa tunapenda kuwakaribisha watu kuwekeza katika *mobile phones* wakati ni kuongeza umaskini katika nchi yetu. Ninatofautiana na wenzangu waliosema ni chanzo cha maendeleo, si kweli na wakati mwingine ni hasara na ni hatari. Kuwawezesha majambazi kufanya ujambazi katika nchi yetu ni kupitia *mobile phones!* Wizi wa kuiba fedha nyingi katika nchi hii unatokana na *mobile phones*. Makampuni haya yanapata fedha nyingi sana. Nchi za wenzetu hata kule walipoendelea unapewa wengine mpaka *one thousand units* bure halafu baada ya hapo ndio upige simu ulipie au mchana ndiyo unapiga simu unalipa, usiku kucha haulipi lakini hapa kwetu kuanzia asubuhi mpaka asubuhi kesho yake hakuna nafuu yoyote, wizi mtupu. Tena gharama za wenzetu kule walikoendelea ni moja ya mia ya bei tunazolipa hapa kwetu. Kwa nini wenzetu wanatufanyia hivyo?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli haya nimeyasema kwa uchungu kwa sababu si wote tunaonunua *mobile phones* ambazo tunazozitumia hapa Tanzania zina faida. Mtu analala na njaa kwa ajili ya kuweka fedha kwenye *mobile phones*, ni hatari! Ni kweli mtu anashindwa kununua chakula cha watoto wake nyumbani ili aweke hela kwenye *mobile phone* ili awasiliane na *girl friend* au apange mpango wa wizi lakini siyo kwa mpango ambao ni wa kuleta maendeleo katika nchi hii na fedha ambazo tunatoa nje ni *five million a day*, *US$ a day* je, tunapata faida? Tujiulize swali hilo halafu ndiyo tuweze kujibu maswali mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ninaomba kuishia hapo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, naomba niungane na walionitangulia kuchangia, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya marehemu Salome Joseph Mbatia, Mbunge mwenzetu aliyekuwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Naomba familia ya marehemu wavute subira na Mungu Mwenyezi ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, aidha, ninawaombea faraja kupitia salamu zangu za rambirambi Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamefiwa na wapendwa wao. Nawaombea na wenyewe Mwenyezi Mungu awape subira katika machungu hayo ya misiba iliyowafika. Aidha, natoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao walipata ajali na kuumia na wanaendelea na maumivu makali kama Mheshimiwa

Mudhihir Mudhihir, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya na Mheshimiwa Zaynab Vulu. Namwomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuungana na wenzangu kumpongeza Mwenyekiti wetu mpya wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa tena kuongoza Chama chetu. Ni ushindi kwa Chama chetu kukamilisha uchaguzi kuanzia ngazi ya Shina hadi Taifa.

Vilevile niwapongeze sana sana wenzetu ambao wamepewa dhamana katika uchaguzi uliofanyika hivi majuzi tu kuingia kwenye Halmashauri Kuu ya Taifa na Kamati Kuu ya CCM. Nawahakikishia ushirikiano wangu akiwemo Waziri wa Miundombinu tunayoijadili sasa hivi, Mheshimiwa Andrew Chenge ambaye ameshinda kuingia NEC na *Central Committee*, kila la kheri Mheshimiwa Andrew Chenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naingia kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, kwa mujibu wa taarifa hii, kazi walioifanya kwa kweli ni kubwa. Wametembelea maeneo mengi ya nchi yetu wakikagua miradi katika zoezi zima la kusimamia Serikali na vyombo vyake vyote kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ambalo nimeliona kwenye mapendekezo ya Kamati na maoni yake na limenigusa sana ni lile eneo ambalo tumeelezwa katika Ibara ya 5.1, Kamati ikieleza kushindwa kutekeleza wajibu wake kutokana na ufinyu wa bajeti na kulazimika kupata ufadhili kutoka kwenye Wizara, ndiyo lugha ambayo wametumia kwenye taarifa. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana. Natambua kwamba taarifa ni ya mwezi Agosti, 2007, ni muda mrefu umepita inawezekana mambo yamebadilika. Kwa hiyo, natarajia Mwenyekiti wa Kamati ya Mindombinu akisimama kujibu hoja, atatupa *update* kwenye eneo hili. Fedha kutotolewa za kutosha kuiwezesha Kamati muhimu kama ya Miundombinu kutimiza wajibu wake ili kufika katika maeneo ambapo inaweza ikafika ili kuweza kuisimamia Serikali, ni jambo la kusikitisha.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa msisitizo kwa sababu tulipopitisha bajeti katika Mkutano wa Bajeti, Wizara ya Miundombinu tuliipatia fedha nyingi sana na ninatambua miradi mingi inayoendelea kujengwa katika nchi yetu na umuhimu wa kukagua na kusimamia ili kuhakikisha kwamba fedha tulizoziidhinisha kutumiwa na Wizara ya Miundombinu zinafanya kazi iliyokusudiwa bila utata. Hata Kamati yenyewe imebainisha kwamba kuhakiki thamani halisi ya fedha zilizotumika kwenye miradi ni jambo muhimu. Sasa Kamati ambayo inafanya kazi kwa niaba yetu, imefika mbele ya Bunge, imetueleza kwamba imeshindwa kufanya hivyo. Hili si jambo ndogo na wala si jambo la subira. Nimesikitika zaidi kwamba ratiba ya kuanza kujadili Taarifa ya Kamati bila kukusudia imegongana na mikutano mingi ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, labda nianze kwa kushauri kwamba siku nyingine tukianza kujadili Taarifa za Kamati, usiruhusu wajumbe wa Kamati kutoka nje kwenda kujadili

mambo mengine kwani Wajumbe wa Kamati waliotoka ni wengi sana tuliopo humu ndani ni wachache na jambo hili ningefurahi sana kama tungelipatia Azimio. Fedha nyingi zilizotengwa kwa ajili ya miundombinu sasa hivi tunakaribia kuingia katikati ya utekelezaji wa bajeti, kama Kamati yetu haitaweza kwenda kusimamia miradi hiyo ili kusudi Waziri wa Miundombinu anapoleta taarifa ya utekelezaji wa bajeti na kuomba fedha nyingine kwa mwaka wa fedha ujao, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu atueleze jinsi alivyohakiki kwa kutumia Kamati yake utekelezaji wa miradi kwa fedha ambazo tuliidhinisha katika bajeti ya 2007/2008, itashindwa na hilo ndilo jambo ambalo litatusaidia. Kwa kweli nisingependa tunapokuja kwenye Mkutano wa Bajeti unaokuja, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu atueleze kwamba ameshindwa kwenda kufuatilia miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ametufahamisha na amelifahamisha Taifa kwamba *TRA* wanafanya kazi nzuri sana na mimi ninakubaliana na Mheshimiwa Rais kwa sababu sote tunafuatilia kazi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania. Kwa sasa hivi wanakusanya shilingi bilioni 300 kwa mwezi, hayo ni mapato ya Serikali na fedha nyingi tulizoziingiza kwenye miundombinu ni nyingi mno. Kwa hiyo, si jambo jema kwa chombo kama Bunge kupata taarifa kwamba kinakosa fedha za kwenda kusimamia miradi kwa niaba ya Bunge. Wanakosa fedha za kufika kwenye miradi hiyo halafu wanaomba ufadhili wa Wizara. Kamati haina fedha, Wizara ina fedha za kufadhili. Kwanza, neno ufadhili nadhani wamelitumia bila kukusudia, inawezekana matatizo ya Mheshimiwa Mwenyekiti ya Kiswahili ni kama yangu. Kwa hiyo, siyo ufadhili ila wanawajibika kutoa fedha kama mnaenda kukagua miradi.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu atujulishe sasa hizo fedha wanazo na kama hawana hizo fedha wa-*draft* Azimio tulipitishe Bungeni hapa fedha zitoke haraka sana kuanzia mwezi Januari, 2008 ili waweze kufuatilia hiyo miradi ambayo wamesema hamjaenda tupate taarifa sahihi kwa maslahi ya wananchi. Kwa sababu hatuwezi kwenda kusema Kamati ya Miundombinu haikupewa fedha na Serikali wakati tunapopitisha fedha ni sisi Bunge. Serikali haitoi fedha ni sisi tunatoa fedha, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu usafiri wa majini. Ninaishukuru Kamati imeliona hilo. Ziwa Victoria tuna matatizo makubwa. *MV Victoria* imesimama, *MV Umoja* ambayo inabeba mabehewa kuyapeleka mpaka Uganda na hivyo kuweka dhana ya meli kupitia Ziwa Victoria, imechoka. Wawekezaji wameshindwa kuingia Ziwa Victoria. Mheshimiwa Andrew Chenge, rafiki yangu anajua hilo, kwa sababu ni gharama kubwa kuingia katika miradi hii, inakuwa kama ni huduma na faida mchanganyiko. Ninaomba kwa kweli eneo hili walitazame, sasa hivi katika Mkoa wa Kagera watu wanahangaika sana.

Mheshimiwa Spika, ndege ya *Precision Air* imeanza kupata tabu sana, kwa kipindi kirefu tulikuwa tunaenda Kagera kwa ndege binafsi ya kukodi badala ya ndege ya *Precision Air*. Hili ni jambo ambalo limetuweka kwenye hali ngumu sana. Ninaiomba kabisa Serikali itoe kipaumbele kuhusu usafiri wa majini katika Ziwa Victoria. Watu wanakufa sana na mimi katika Jimbo la Muleba Kusini nina Kata moja ina Visiwa 11

inaitwa Kata ya Mazinga ndani ya Ziwa Victoria. Kwa hiyo, ninajua hali halisi na kibaya zaidi kwenye Jimbo langu sina gati hata moja. Kupanda mtumbwi mpaka ukanyage majini, mimi sijui kuogelea, kwa hiyo, unakwenda na mtu amekufuatia kwa karibu ndiyo upande mtumbwi unaoweza kukufikisha kwenye Kisiwa. Sasa kwa wakati kama huu ni jambo la kutisha.

Mheshimiwa Spika, la kutisha zaidi nimeona kwenye Televisheni kuna mtu ametuletea mamba katika Ziwa Victoria eti ni utalii, hili halihusiki hapa kwa sababu sio la Wizara ya Miundombinu, lakini Mheshimiwa Andrew Chenge na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari naomba radhi sikumpongeza naye ameingia kwenye NEC na Kamati Kuu na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, mjukuu wangu naye ameingia NEC, wanastahili pongezi kwa sababu tunajadili mambo yao, tuondoleeni mamba. Badala ya kutuletea mitumbwi na boti wanatuletea mamba wameanza kula watu. Ninahitaji gati Katunguru pale na Kasenyi na katika maeneo mengine. Niliona niligusie hili kwa sababu Kamati imelisema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa reli, naona wameanza sijui wamefanya namna gani? Nilikuwa *Railway Station* nikaona treni inapita imejaa abiria toka Dar es Salaam, mabehewa yale yale na *engine* ile ile! Sasa sijui wamefanyaje? Lakini hongera, mimi sitaki kufuatilia, mradi mmeanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TAZARA,* nimevutiwa na Kamati kusema kwamba China wapewe kipaumbele katika uwekezaji kwenye *TAZARA*, mimi ninaungana na Kamati. Hivi kweli tunaweza tukaweka kwenye *tender* China inataka kuingia kwenye ubia na *TAZARA*? Hata marehemu Baba wa Taifa alipolala mbinguni anaweza akatucheka sana. Marehemu Mwalimu Julius Nyerere alikwenda China kuomba tukapewa reli bure sasa tumeshindwa kuiendesha tuanze kuijadili China iingie au Marekani waingie, China kwanza. Hata Kiwanda cha Urafiki ni aibu tu kimechakaa wakati tulipewa bure, Wachina waliopewa sijui sio wenyewe hao hata kupakaa rangi wanashindwa!

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa anga, Kamati wamefika Mkoa wa Kagera lakini katika paragraph 5.2, Kiwanja cha Ndege cha Bukoba wameshindwa kuandika katika taarifa. Nadhani ni kosa la uchapishaji. Kwa kweli kinahitaji lami ya haraka haraka na kinahitaji kuboreshwa sawasawa kwa sababu ni hatari kwa maisha ya wananchi na viongozi wanaotua pale. Wakati ndege inatua mnaenda mmekata pumzi!

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa shukrani. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu afikishe shukrani za wananchi wa Muleba Kusini, barabara ya Kagoma – Kyamiorwa - Lusahunga, Lusahunga - Buzirayombo, Wakandarasi wapo wanafanya kazi na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu amekuwa akifuatilia kwa karibu na ananiuliza wanaendelea namna gani na mimi ninasema waache wafanye kazi kwa sababu na sisi hatujui zinatengenezwaje hizo lami ili mradi wapo. Lakini nimevutiwa na Kamati imesema itashirikiana na wao kusimamia ili kazi ifanyike kulingana na thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kwamba Kamati lazima ipewe fedha. Naomba Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati atakaposimama, kwa niaba ya Mheshimiwa Spika, atwambie kama wamepewa na kama hakuna tupitishe Azimio ili wapewe pesa. Sisi Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama tunaweza tukasubiri kidogo lakini Kamati ya Miundombinu wapewe kwanza ili waweze kusimamia fedha za umma kwa sababu ni nyingi sana katika Wizara ya Miundombinu ili tusije tukadanganywa na Makandarasi ambao siyo waadilifu na waaminifu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Wilson Masilingi na mimi pia ninakushukuru kwa yote yale uliyoyasema. Msemaji wetu wa mwisho kwa mchana huu ni Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu, iliyoletwa na Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nitumie fursa hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi, kwa kukamilisha mchakato mrefu sana wa kupata uongozi mzima wa Chama kutoka ngazi ya chini hadi juu kwa ufanisi mkubwa na vilevile kwa kuzingatia misingi yote ya demokrasia.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne kwa kazi nzuri na kubwa inayofanywa ya kuboresha miundombinu nchini, kazi ambayo hata sehemu zilizopo pembezoni kabisa mwa nchi kama vile Makongorosi - Chunya, Matema - Kyela, zimeshuhudia.

Mheshimiwa Spika, sina wasiwasi kabisa kwa kasi tunayoenda nayo sasa kwamba kufika mwaka 2010 tutakuwa tumekamilisha au tumeanza utekelezaji wa miradi yote ya miundombinu tuliyowaahidi wananchi mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, nimeguswa kipekee, ndiyo maana pengine nimeona nichangie safari hii na utendaji kazi mzuri wa Wizara ya Miundombinu. Miezi mitatu tu baada ya Mheshimiwa Rais wakati huo akiwa mgombea Urais, kuwaahidi wananchi wa Kyela kwamba atajenga barabara yetu kwa kiwango cha lami, barabara ya kutoka Kikusya - Ipinda – Matema. Naibu Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, akaja na wataalam wa barabara Kyela na miezi minne baadaye tukaanza kuona mchakato wa kitaalam umeanza wa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha uliopita, tulitenga fedha na kuendeleza kazi za awali za kitaalum. Kwa kweli kasi ya aina hii haijapata kutokea. Mwaka huu vilevile Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, amekuja Kyela na timu nzima ya *TANROADS* kuja kukagua maendeleo na kama nilivyosema, kwa kweli kasi ya kazi ya aina hiyo inastahili kupongezwa sana.

Mheshimiwa Spika, mwezi uliopita tulipata bahati Mkoa wa Mbeya kutembelewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika ziara yake ya Mkoa akiwa ameongozana na Mawaziri mbalimbali. Lakini muhimu ninayemtaja hapa ni Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Andrew Chenge. Pamoja na mambo mengine aliikagua barabara yote hiyo ya Kyela kutoka Kikusya - Ipinda – Matema. Waziri Mkuu akawa kiongozi pengine wa kwanza wa Kitaifa katika miaka 30 kuikagua barabara yote mpaka huko na barabara yenyewe ni ya vumbi, yenye mawe na mashimo mengi tu.

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo wakati wa mvua inageuka kuwa mto. Tunatumia mitumbwi tu pale. Kweli ziara hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Andrew Chenge, ilichochea sana ari ya wana-Kyela ya kuongeza juhudi ya kilimo, maana wana uhakika kwamba mazao yao sasa yatapita kwenye barabara ya uhakika ambayo itatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kyela, kwa kweli ninawapongeza sana viongozi wetu hao. Nampongeza Waziri Mkuu kwa ziara yake iliyokuwa na mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kuguswa na tatizo kubwa ambalo linanikabili mimi Kyela hasa katika Kata ya Lusungo. Pengine nikukumbushe tu. Niliongelea hapa kuhusu tabu ninayopata kufika kwa wananchi wangu wa Kata ya Lusungo upande wa pili, kuvuka mto huku nikiwa nimeshika suruali mkononi.

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe uliona ile picha na ukahakikisha picha hiyo anaiona Mheshimiwa Waziri Mkuu, anaiona Waziri Andrew Chenge, anaiona Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mizengo Pinda.

Mheshimiwa Spika, ninataka kukuambia leo hii kwamba picha hiyo imezaa matunda. Wizara ipo kwenye mchakato wa kutujengea daraja la kudumu kwenye Mto Lufilyo na hilo alitutangazia Mheshimiwa Waziri Andrew Chenge alipokuja kwenye ziara na wananchi wa Lusungo sasa hivi wanasheherekea. Kwanza hawaamini, wanadhani pengine ni tarehe 1 Aprili, kwa watu waliozoea hiyo tarehe lakini kwa kweli ni ndoto ambayo ni nzuri sana kwa sasa hivi. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Andrew Chenge kwa hatua hiyo. Lakini kwangu huu ni ushahidi tosha kwamba Serikali ya Awamu ya Nne ni *people centred*, ni Serikali ambayo inajali sana matatizo ya wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, nigusie ukurasa wa tisa wa Taarifa ya Kamati. Ukurasa huo umeeleza kuhusu matatizo yanayolikabili Shirika letu la Posta. Nakiri kuwa huduma za Shirika la Posta ni muhimu sana kwa Taifa na naungana na Kamati kabisa kuiomba Serikali kuchukua hatua za haraka na za makusudi za kulisaidia Shirika hili hasa kwa maana ya kuliongezea mtaji ili kuweza kuhimili ushindani mkubwa ambao umejitokeza

sasa hivi katika mfumo wa soko huria. Lakini pamoja na hilo, nadhani kuna umuhimu kwa Shirika lenyewe liwe na ubunifu zaidi kwa kutafuta njia mbalimbali za kujiongezea kipato. Nitatoa mifano michache hasa katika kutafuta *new products*.

Mheshimiwa Spika, miezi michache iliyopita nilikuwa nchini Zambia ambako nililiangalia pia Shirika la Posta la Zambia. Sisi huku Tanzania Shirika letu linasafirisha vifurushi vya posta, linasafirisha barua na hata magazeti kwa kutumia *Landcruiser hardtops*. Lakini wenzetu wa Zambia wamekwepa hilo kwa sababu kwa kweli kutumia magari madogo kama hayo ni gharama kubwa, hailipi, wao wanatumia *luxury buses.* Wameanzisha mabasi ya kifahari ambayo yanatoka kona moja ya nchi kwenda nyingine yakibeba vifurushi hivyo vya posta, yakibeba barua, yakibeba magazeti, lakini wakati huo huo mabasi hayo yanafanya biashara ya uhakika kweli kweli. Mabasi hayo yanatembea katika muda ambao mabasi mengine hayaendi na ni rahisi sana kwa Shirika letu la Posta kutokana na maslahi ambayo Serikali inayo ndani kuweza kupata kibali cha kwenda muda ambapo mabasi mengine hayaendi na tukayapa ulinzi mzuri tu kuweza kufikisha abiria sehemu wanayokwenda. Kwa hiyo, nilichokuwa nasisitiza hapa ni kwamba Shirika letu pia la Posta lijaribu kutafuta mbinu mbalimbali ya kuanzisha *products* mbalimbali mpya kuweza kujipatia kipato.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 13, lipo suala la ujenzi wa uwanja wa ndege wa Songwe. Nimefarijika sana kwa taarifa za hivi karibuni za Serikali kwamba imepata fedha za kumalizia uwanja huo. Kwa kweli taarifa hizo ni changamoto kubwa sio kwa Mkoa wa Mbeya tu lakini kwa Mikoa yote jirani kuhakikisha kwamba kweli uwanja huo wa ndege utakapoanza usiwe tu kwa ajili ya abiria kushuka na kupanda, hapana. Uwanja huo wa ndege wa Kimataifa uweze kuchochea biashara hasa kwa watu wetu kuongeza kilimo cha mazao ya biashara yakiwemo hata maua, ikiwemo *cocoa* ambayo inalimwa sana Kyela. Watu wetu wawekeze kwenye huduma mbalimbali kama za hoteli, wawekeze kwenye usafiri na vilevile tuna changamoto sasa hivi kwa Kanda nzima ile kuweza kuboresha miundombinu inayoelekea kwenye vivutio vyetu mbalimbali. Tuna *Kitulo National Park*, *Ruaha National Park*, *Crater Lake* iitwayo Ngozi, tuna fukwe za ajabu duniani za Matema huko Kyela. Kwa hiyo, changamoto tuliyonayo ni kuboresha hiyo miundombinu ili uwanja huo wa ndege uwe na maana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa ombi maalum kwa Wizara. Wakati umefika naamini wa kuhakikisha kwamba barabara zetu kwa kweli zinakuwa na vyoo. Hili nimeshaliongelea hapa. Nadhani pengine viongozi mbalimbali hawajaelewa hili tatizo ni kubwa kiasi gani na limebakia Tanzania tu.

Mheshimiwa Spika, nimeshapata bahati ya kusafiri kutoka Zambia, Ndola kwa basi nikaja Mbeya, Arusha mpaka Kampala. Ni Tanzania tu unakuta tabia za ajabu ajabu ambazo kwa kweli zinatudhalilisha sana watu wazima. Basi linasimama, kuna watoto wadogo kuanzia miaka mitatu mpaka wazee wenye zaidi ya miaka 80, wote mnatoka kushambulia vichaka. Halafu watoto wadogo wanaangalia, watoto wengine wanashindwa kabisa kwenda haja ndogo, wanabakia wakiangalia wazee wanafanya mambo gani pale! Sasa hii ni aibu kubwa mno. Hivi kweli tunashindwa kuhakikisha kila baada ya kilomita fulani kunakuwa na choo?

Mheshimiwa Spika, nina mgeni wangu sasa hivi anafundisha *University of Dar es Salaam*, ni Mjerumani. Anasema ahaa, unajua nyie Watanzania, Waafrika ni watu wa ajabu sana, mnatusema sana Wazungu kwamba sisi tunatembea nusu uchi, tunapenda kuvaa vichupi na sisi tulifikiri nyie mna aibu sana lakini ukipita katika hizi barabara zenu mnavyojipanga kunyunyizia hayo majani na mimea, yaani inashangaza!

Mheshimiwa Spika, tufike mahali tulionee aibu suala hili. Huwezi kuona nchi kama Zambia ambapo unatoka Ndola unafika Kapirimposhi, kuna *petrol station* pale, kuna choo cha kulipia pale, watu wanashuka pale. Sisi ukipita tu barabarani ukiona majani yamebadilika rangi kuwa ya kijani, unajua hapo ndipo kuna choo cha Kitanzania. Hayo ni mazingira gani? Namwomba Mheshimiwa Andrew Chenge, yeye ni mchapa kazi mzuri sana, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, wameishika hii Wizara, wanaiendesha vizuri sana, wanafanya mambo makubwa mno, lakini kitu kidogo kinawatia dosari maarufu kama "kuchimba dawa". Hebu futeni kabisa uchimbaji dawa katika kipindi chenu cha uongozi! Sio lazima Serikali ijenge, wekeni mazingira ili *private entrepreneurs* wajenge hizo *facilities* na kuhakikisha watu wa mabasi wanasimama sehemu hizo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vigumu sana pengine kwa viongozi kuelewa adha hiyo na aibu hiyo kwa sababu pengine wao wanatumia magari yao *private* lakini Wabunge tunayatumia sana mabasi, kwa hiyo tunaelewa.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe nakushukuru sana. Niseme tu kwamba hii hadithi ya "kuchimba dawa" ilisaidia sana uwekezaji pale Segera. Aliyewekeza pale alipatwa na shida hiyo hiyo na kwa kuwa alitoka katika utamaduni ambao hauruhusu kuchimba dawa ovyo ovyo, akaamua kununua ardhi na ndiyo maana unaona kuna hoteli pale kwenye kona ya Segera. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hakuna muda tena wa kutosha kuendeleza mjadala huu mzuri sana. Jioni saa 11.00 tutaanza na Mheshimiwa Ruth Msafiri, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Peter Serukamba na hatimaye Mohamed Rished Abdallah. Kwa hiyo, kwa sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu, majadiliano yanayoendelea yanahusiana na Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kama ilivyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Mohamed Missanga. Wasemaji wetu watatu wa mwanzo ni Mheshimiwa Ruth Msafiri ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga ajiandae.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na hasa kunipa nafasi ya kuchangia nikiwa ni mchangiaji wa kwanza kwa jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nikipongeze Chama cha Mapinduzi na nimpongeze sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa jinsi ambavyo amesimamia vizuri Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi na hata yeye mwenyewe kuibuka kuendelea kuwa Mwenyekiti wa Chama chetu kwa kura nyingi sana. Nampongeza kwa upangaji mzuri wa safu yake aliyoipanga tangu Sekretariet mpaka Kamati Kuu. Ninaamini kabisa amepata watenda kazi wazuri na naamini Chama chetu kitazidi kuwa mfano wa uongozi bora wa nchi na Mataifa mengine na vyama vingine vitakuja kujifunza Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Kamati ya Miundombinu kwa uwasilishaji mzuri wa hoja. Wamewasilisha vizuri hoja yao na nawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru sana walionipatia mimi kura. Nimepata kura nyingi sana katika uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi uliomalizika juzi sikuweza kufaulu kufika katika idadi iliyotakiwa, lakini nilipata kura za heshima, nashukuru sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii nitoe salamu zangu za shukrani kwanza kwa wanachama wa Chama cha Mapinduzi kwa wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini, kwa viongozi wote wa Chama na Serikali wa Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Muleba kwa jinsi walivyonifariji katika kifo cha mpendwa mume wangu. Pia naendelea kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wanaoendelea kunifariji, ahsanteni sana. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa nimetoa salamu zangu za mwanzo, leo nitawasilisha hoja zangu kwa mtindo wa *zigzag.* Nitaanzia mapendekezo na hoja zingine nitazimalizia kama muda utaniruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la kwanza, ninaendelea kupongeza utaratibu wa Bunge kupokea hoja za Kamati. Ni jambo zuri na jambo hili liendelee. Lakini ninachopenda kuomba si pekee kwamba ni Kamati ambayo inafanya kazi juu ya taratibu zetu za kila siku za Bunge, tunazo safari mbalimbali za Wabunge wanaokwenda nje ningeshauri kwamba zile taarifa nazo zikawa zinawasilishwa Bungeni. Tuna Wabunge mmoja mmoja au vikundi tumevichagua vinaliwakilisha Bunge letu katika

sehemu mbalimbali navyo vingepewa nafasi vikawa vinaweza kuwasilisha ripoti yao ili kusudi iweze kueleweka ni kitu gani kinafanyika kwa sababu wakati mwingine inakuwa hakieleweki kinachofanyika na hata wakati mwingine safari inakuwa haina maana sana kwa mwendaji, labda wengine wanaangalia ni posho tu, kama safari haina posho anakataa kwenda kwa sababu haoni faida na atakapokuja hana mahali pa kuja kueleza alikwenda kufanya nini na hasa Bunge linafaidika nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge letu sasa limekwishapata fungu lake na litakuwa linatoa fedha kugharamia safari za Wabunge, ni lazima pia lipate taarifa walikwenda kufanya nini na wameleta taarifa gani? Hilo lilikuwa pendekezo langu la kwanza likiendana na kuwaomba Wabunge wa *East Africa* tupate ripoti yao. Tumewachagua Wabunge wa Bunge la Afrika, naomba tupate ripoti yao. Tumewachagua Wabunge wa EU, naomba nao tupate ripoti zao? Tuzipate hizo ripoti ili kusudi tuweze kuona tunafaidika nini na hivi vikundi ambavyo tunavichagua pia na za wale wanaokwenda nje kwa niaba yetu kuliwakilisha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo leo hii nimependa kulizungumzia ni kuhusu mawasiliano ya simu za mkononi. Simu za mkononi ukweli ni kwamba Tanzania sisi tunatozwa kiwango cha juu sana pamoja na utetezi wa viwango hivi kwamba vinafanana na vya Afrika Mashariki. Kama viwango vya Tanzania vinafanana na vya Afrika Mashariki basi Afrika Mashariki nzima inatoza viwango vya juu sana kwenye simu za mkononi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu vidogo vidogo wanavyoviweka kwenye simu nikiviangalia nasikia kama sijui niviite namna gani. Kuna vihuduma vinaitwa huduma ya bure, tafadhali nipigie, huduma ya bure niongezee salio lakini hii inageuzwa kwa yule anayekuletea wewe ndio sasa ubebe gharama ya yule anayetaka huduma kwako. Hii inatakiwa kuwa ni huduma ya Kampuni sio huduma yangu mimi ambaye fulani anataka tuongee. Lakini kwa nini wananchi wanashindwa kumudu hizi huduma na badala yake zinageuzwa kuwa ni za bure, *indirect?* Mimi ninayetakiwa kupiga ama kupigiwa natozwa mzigo ule ni kwa sababu gharama ni za juu sana! Ni kweli Watanzania wanahitaji huduma ya simu za mkononi kwa sababu huduma za *TTCL* za simu zetu za Kitaifa za Shirika hazijaweza kufika maeneo mengi lakini wenzetu wa simu za *cellular* hizi za mkononi kupitia katika milingoti mbalimbali wanayoweka inasaidia kuweza kupata mawasiliano maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Watanzania wanahitaji simu hizo na sisi wote tunaunga mkono suala hilo lakini gharama hizi wazipunguze. Wanafikia mahali upige simu kuanzia saa fulani, sijui saa 6.00 za usiku yaani mimi niwe macho mpaka saa 6.00 kutafuta huo unafuu wa gharama? Ebu nyie Kampuni punguzeni hizo gharama mumwezeshe kila mmoja apige simu na habari ya huduma ya bure hiyo mnamdanganya nani? Yaani mtu apige toka kule mimi niwalipie nyinyi gharama, mimi nakuwa sihitaji kujua yule anachotaka kwangu, sikijui, kwa sababu anaposema tafadhali nipigie, mimi sijui ana shida gani. Kwa nini shida yake nimgharamikie mimi ambaye anataka kuongea na mimi? Inatakiwa ninyi wenye Kampuni muhakikishe kwamba mnagharamikia gharama zao kwa kupunguza viwango vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi si mtaalam wa mahesabu ya biashara lakini ninavyofahamu ni kwamba ukipata wateja wengi hata kiwango kikiwa kidogo utapata faida. Miaka waliokwisha *operate* hapa nchini, haya makampuni ya simu wamekwishapata fedha za kutosha kwa sasa hivi wapunguze viwango wasitudanganye, mara *message* za bure, mara nakupa sijui meseji tano za bure, havina maana yoyote. Tunachohitaji gharama zao ziwe ni *manageable* kila mmoja anunue simu, kila mmoja atumie simu na kwa jinsi ambavyo anavyotaka, awe na uhuru. Kama akipiga simu saa mbili asubuhi sawa, saa mbili usiku sawa, saa nane usiku uamue mwenyewe sio mpaka ulazimike uwe macho kesho yake ushindwe kufanya kazi zingine kwa sababu tu eti unataka kuongea na simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine dogo ambalo nimelipanga leo nilizungumze katika mpangilio wangu huu wa leo ambao umekaa kwa namna ambavyo nimeuweka, nilitaka nizungumzie nguvu ya Kamati. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC).* Miaka mitano iliyopita nilikuwa mjumbe wa Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala. Lakini mara chache huwa napenda kuhudhuria *LAAC* nikipata nafasi, lakini naangalia jinsi ambavyo wale watendaji wakuu wanavyokuja wakati mwingine huwa wanababaika katika kutoa taarifa za matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipopokea taarifa ya *LAAC* kipindi kilichopita hapa Bungeni walituelezea jinsi ambavyo walifikia mahali pa kudanganywa kwamba kuna mradi fulani lakini walipokwenda kuutembelea walikuta huo mradi ulikuwa haupo ama umefanyika katika hali ambayo haikuwa imeridhisha. Sasa nikajiuliza hivi Kamati imepewa mamlaka gani na uwezo gani wa kuishauri Serikali juu ya ule utendaji wa mtendaji wake, je, unakidhi? Kwa sababu kama huyu mtendaji anaweza akaidanganya Kamati kwa kuiandikia taarifa isiyokuwa sawa sawa, wajumbe wakakagua mradi wakakuta mradi hauko sawa sawa na taarifa, je, wana nafasi ya kuishauri Serikali juu ya huyu mtu ama ni basi wakishapokea ikaja Bungeni ikapokelewa, tukajadili yale mapungufu ndiyo imekwisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri kwamba Kamati ipewe uwezo wa kuishauri Serikali juu ya uwezo wa watenda kazi wake. Wao wanafahamu kwamba Kamati inapofika pale haitaki mzaha, inataka kufuatilia fedha za Serikali, zinazotolewa hapa ni fedha za kila za Mtanzania aliyetakiwa kuzisimamia si zake! Kwa hiyo, hatakiwi kutoa taarifa ya uongo kuidanganya Kamati kwa sababu kuidanganya Kamati ya Bunge ni kudanganya wawakilishi wa nchi! Hapa sisi ndio sauti za wananchi wa Tanzania, zimekaa hapa, ndio tunaokaa kusema fedha za Watanzania zitumike wapi. Tunapokuwa tunakwenda kuangalia fedha zimetumika vipi kama mwenye kuzisimamia hawezi kuwa si mwadilifu na Kamati isiseme, naomba Kamati ipewe nguvu ili iweze kuwa na nafasi ya kushauri kusudi matumizi mazuri ya fedha za Serikali yaweze kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema matumizi mazuri ni pamoja na kujali wakati. Imekwishafika mwezi wa nne, bajeti zimeanza tena kupangwa ndiyo kwanza fedha kule hazijafika na zinapofika wanaamua kufanya sherehe na mambo mengine ili

fedha zile zimalizike. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali lakini Kamati haina mahali pa kusemea kwamba huyu mtendaji hafai. Kwa hiyo, napenda kushauri kwamba suala hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda nilizungumzie ni kuhusu usafiri katika Ziwa Victoria. Ziwa Victoria ni kweli maji yanapungua na nilipokuwa nasoma kwenye Taarifa ya Kamati, *paragraph* 5.14, wanazungumzia habari ya kupungua kwa kina cha maji na habari ya kuweka usafiri vizuri. Mimi nilikuwa nafikiria kwamba imefika wakati pengine kuona kwamba usafiri katika Ziwa Victoria upewe kipaumbele cha hali ya juu sana. Meli iliyokuwa inategemewa ya *MV Victoria* baada ya kuwa mbovu kwa kweli usafiri umekuwa ni mgumu kwa sababu ile meli ilitegemewa kusafirisha abiria na ilitegemewa vile vile kusafirisha mizigo yao tena kwa wingi na ilikuwa inaridhisha japokuwa ilikuwa ni meli moja lakini ilikuwa inaweza kufanya kazi kwa namna ambavyo ilikuwa inaridhisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa, nimeona ame-*cross floor,* umejiunga na CCM?

**MHE RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika yangu moja utanifidia, kwa kuwa umekalia Kiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua mpango wa Serikali, je, Serikali ina utaratibu gani kuhusu kuboresha usafiri katika Ziwa Victoria? Hivi Serikali ina taarifa kwamba katika Ziwa Victoria kuna makazi ya watu wengi mle ndani ukiachilia mbali Visiwa vya Ukerewe, kuna visiwa ambavyo amevitaja vya Mheshimiwa Masilingi viko mle, mimi vile vile nina visiwa 21 vinakaliwa na watu na ni visiwa maarufu sana ambavyo vinachangia uchumi wa Wilaya ya Muleba, kisiwa cha Kerebe, Bumbile na kisiwa cha Gozba, lakini havina usafiri hivi. Kuna utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba katika Ziwa Victoria tunakuwa na usafiri wa haraka kati ya Mwanza na Bukoba na katika bandari zake mbalimbali. Napenda kujua jambo hili na naiomba sana Serikali iliangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, uchumi wetu mwingi sana umekaa katika bandari zetu za Maziwa Makuu na bandari zetu za bahari yetu. Kuna mkakati gani wa kuboresha hizi bandari ili kusudi kuhakikisha kwamba tunafaidika na bandari hizi na kufanya wale wenzetu wanaotuzunguka waache kuwa wanapeleka mizigo yao kule katika bandari ambazo ziko nje ya nchi yetu? Napenda kujua ni nini mkakati wa Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuishauri Serikali iangalie uwezekano wa kubadilisha mgawanyo wa zile fedha zinazojulikana kama *fuel tolls* au maarufu kwa *road toll*. Naomba zibadilishwe kwa sababu sehemu kubwa ilikuwa inaachwa kwenye Serikali Kuu na sehemu ndogo inaenda kwenye Serikali za Mitaa. Lakini sasa hivi baada ya barabara nyingi kuu kuwa za lami na mwelekeo mkubwa ni wa kuziimarisha barabara za Serikali za Mitaa ambazo ni mbovu zaidi na ambavyo maendeleo yanatakiwa yarudi kwenye Serikali za Mitaa, ninaomba, hapa ninazo barabara nyingi tu ambazo pengine kulingana na muda siwezi kuzitaja zote lakini nizitaje hata

chache tu kwa mfano barabara ya Izigo - Kyamkwikwi tumetumia fedha nyingi za Serikali, tuna Katoke - Nyawaibaga imetumia fedha nyingi za Serikali, Katoke - Byazi na kadhalika, barabara hizi zimetengenezwa na Halmashauri yaani Serikali za Mitaa lakini haziwezi kupata fedha za kuzikarabati kila wakati kwa sababu pato lile ni dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tayari Serikali ina namna nyingine ya kupata fedha kutoka katika haya Mabenki mbalimbali na hizi zilikuwa zinatokana na fedha za mafuta naomba mgawanyo ule ubadilike walau hizi fedha nyingi ziende kwenye Serikali za Mitaa ili barabara zetu ndogo hizi ambazo ni za vumbi ziwe ni imara wakati wote, madaraja yatengenezwe, mahali kunapoharibika mara baada ya mvua kutengenezwe, maeneo yote ambayo yanaonekana kwa kweli ni makorofi yatengenezwe, ndipo hata manufaa ya barabara kuu yataweza kuwepo kwa sababu kutakuwa na usafiri ulio na uhakika kutoka katika barabara ndogo kwenda katika barabara kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, napenda kusema kwamba nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kama ushauri naomba wakati wa ku-*wind up* Wizara inayohusika itupatie majibu pamoja na kwamba najua Mwenyekiti atajibu lakini Wizara inayohusika ijitahidi kututafutia majibu yaliyo sahihi hata kama si kwa leo katika muda mwingine ambao utakuwa ni muafaka ili waweze kutupatia majibu kwa hoja hizi ambazo nimezitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB J. MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo na mimi nitoe mchango wangu kuhusu taarifa hii ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla ya kujikita na hiyo taarifa, ningependa nichukue nafasi hii kutoa pole kwa ndugu wa marehemu Mheshimiwa Salome Mbatia, aliyefariki kwa ajali ya gari pamoja na wenzetu wengine wote waliofiwa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira, watasahau baada ya muda, lakini awape uvumilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa wale wenzetu waliopata ajali mbalimbali, Mwenyezi Mungu awajalie wapate nafuu, awape moyo wa uvumilivu na awaondoshee maumivu haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia nimpe pole Mheshimiwa Kiongozi wetu wa Upinzani,Mheshimiwa Hamad Rashid na Mwenyezi Mungu amjalie apate *recovery* ya haraka baada ya kufanyiwa operesheni huko India na taarifa tulizonazo mpaka hivi leo ni kwamba leo ameanza mazoezi na tunamwomba Mwenyezi Mungu amsaidie apate salama haraka haraka ili arejee kuungana nasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya taarifa hizo za pole kwa waliopata matatizo na waliofiwa, nigeukie kwa watani wetu. Hivi juzi ndio walikuwa na uchaguzi, ni vyema tuude utamaduni wa kupongezana. Nachukua nafasi hii kuwapongeza wale wote

walioshinda katika uchaguzi huo. Nichukue nafasi hii, kutoa pongezi mahsusi kwa ndugu yangu, kijana wetu Profesa Makame Mnyaa pamoja na kaka yetu Wangwe, tunawakaribisha katika ulingo wa siasa na nawapongeza kwa ushindi wao. Kwa wale walioshindwa, wawe wapole kidogo, wavumilie kwa sababu ndiyo hivyo, wenyewe mnasema ina wenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, sasa naomba niingie katika Taarifa ya Kamati ya Miundombinu. Sehemu ya 5 na 6, Kamati imezungumzia masuala ya hizi simu za mkononi na akataja simu kama *CELTEL, TIGO, VODACOM* na *ZANTEL* na naiongezea Kamati na *TTCL* kwamba wapunguze hizi gharama. Ni kweli na hata mchangiaji aliyepita Mheshimiwa Ruth Msafiri amezungumzia hizi gharama. Sina haja ya kuendelea kusisitiza zaidi wachangiaji waliopita wameshazungumzia lakini mimi niibebeshe mzigo *TICRA* kwa sababu hiki ndicho chombo kinachoangalia haya Makampuni yote na chombo hiki ni lazima kiwe imara na kifanye kazi yake vilivyo na wao ndio wanaweza ku-*regulate* hizo bei na kujua duniani viwango vikoje na sisi Tanzania tunatozwa namna gani na wao ndio wa kuishauri Serikali. Kwa hiyo, *TICRA* ina dhamana ya kuangalia yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, haya Makampuni yana ujanja wa *promotion* ambayo mwenyewe niliwahi kuzungumzia, unaweza ukaambiwa ukiingiza dola 5 unapata dola 6 au kitu kama hivyo au kama alivyozungumza mwenzangu aliyepita lakini nani ana *regulate* ile simu pamoja na kwamba hizi simu zetu unaweza ukaangalia matumizi yako lakini ukweli wa mambo tunaibiwa sana. *TICRA* wanapaswa waangalie sana haya matumizi na kusimamia haya Makampuni yasituibie sana. Inaonekana kuna ujanja ujanja si wananchi wengi wanajua kwamba mimi nikiweka dola 10 nimetumia dakika ngapi kwa vile bei zipo na sasa hivi nimetumia kiasi gani, mtu hana muda huo wa kuangalia. Kwa hiyo, ni dhamana yao wao kuangalia haya Makampuni yanafuata kweli hizi taratibu au *promotion* zao hizi ni za kuhadaa, ni za kibiashara tu? Kwa hiyo, hata kama uko uwezekano wa kufunga mita katika hiyo mitambo yao ya kujua simu zilizopigwa na fedha zilitozwa na watu namna gani walivyogharamia ingekuwa vizuri lakini *TICRA* wana wajibu wa kusimamia hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, kuna Waheshimiwa Wabunge waliyapongeza haya Makampuni ya Simu na mimi nawapongeza kwa juhudi zao, wametusaidia sana katika maendeleo lakini kuna sehemu hizi simu hazijafika yaani mawasiliano hayapatikani. Nitakuwa tofauti na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotaka kuongezwa minara hizo sehemu ambazo mawasiliano hayapatikani. Mimi nashauri vinginevyo. Minara hii ikiwa mingi kila pahali kwa upande mwingine inachafua mazingira. Haiwezekani Makampuni matano sita ya simu eneo fulani kwa mfano Bariadi tena eneo zima liwe na minara yote hii haiwezikani, wanatuchafulia, mazingara yanachafuka! Taratibu zipo za kuwezesha mawasiliano kupatikana kwa minara michache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri umeonyeshwa na *ZANTEL* na *VODACOM* wanatumia minara hiyo hiyo. *ZANTEL* inafanya kazi hapa Dodoma lakini hawana mnara hapa Dodoma ni *VODACOM* wanayo minara hapa. Kwa hiyo, sisi

tunapata mawasiliano kwa kupitia simu za *ZANTEL* kwa kutumia minara ya *VODACOM* na Makampuni mengine yaige mfano huo yafanye hivyo hivyo. *TTCL* wana mtandao mkubwa nchini kwa hiyo ni wajibu wa *TTCL* wa kuyaruhusu makampuni mengine kuweza kutumia minara yao ili hayo mawasiliano yapatikane na hizo sehemu nyingine ambapo hayapatikani badala ya kujenga minara kila mahali, inachafua mandhari ya miji, inachafua mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande huo huo pamoja na kwamba kwenye taarifa ya Kamati halijazungumziwa, lakini hata haya ma-*satelite dish* na *butterfly antenna* zinachafua miji kwa kiasi fulani. Lakini *TICRA* ipo wangeieleza Kamati hii ya Miundombinu huu mpango mzima wa *cable network* ya mawasiliano ya simu na kadhalika umefika wapi na namna gani hatujaona katika taarifa yao wakati walipaswa watueleze? Au *cable television* ambayo inapunguza haya mambo ya *satellite dish* na *butterfly antenna* ambayo kabisa zinaharibu mandhari ya miji, hawajasema chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Kamati, kifungu cha 5.11, Kamati imezungumzia masuala ya bandari na zikatajwa bandari za Mtwara, Tanga, Dar es Salaam, Kamati imeshauri kwamba hizi bandari zifanyiwe matengenezo na ziimarishwe kivifaa kabla ya kubinafsishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bandari ningetaka Mwenyekiti wa Kamati hii ya Miundombinu, tukiangalia katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukurasa 128, suala la bandari, *item* ya 11 limetajwa kwamba ni suala la Muungano. Lakini ki-*practise* sijasikia hata bandari moja ya Zanzibar, Pemba kushughulikiwa na Jamhuri ya Muungano zinashughulikiwa na Serikali ya Zanzibar lakini hapa linatajwa kwamba ni suala la Muungano. Ninashauri Kamati ingepata ufafanuzi kama hili suala kama halitekelezeki kwa nini lisifutwe katika Katiba? Kamati ishughulikie suala hilo na kama halitekelezeki na limo ndani ya Katiba watuambie. Katika ripoti ya Kamati hakuna popote walipotaja bandari yoyote ya Unguja au Pemba kwa ajili ya matengenezo au kitu kingine chochote wakati limetajwa kwenye Katiba kwamba ni suala la Muungano. Kamati ingeishauri Serikali kwa sababu ndio wajibu wao kama suala hili halitekelezeki lifutwe katika Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine katika suala hili la bandari, Kamati imeshauri kuimarishwa hizi bandari kivifaa. Mimi ushauri wangu katika hapa hizi bandari zetu hivi sasa kuna matatizo yanayotokea na tuliwahi kuzungumzia hapa Bungeni kwamba na kwenye maziwa au baharini ajali nyingi zinatokea, vifo vingi vinatokea, vyombo vinakumbwa na madharuba au wavuvi na wasafiri wengine wanazama lakini vyombo vya uokovi *(rescue equipments)* hakuna. Nashauri baharini au nchi kavu kiundwe chombo kama *coast guard* maalum na hata kuwe na *radder* ambayo inaweza kutazama mwenendo wa wavuvi na wasafiri baharini panapotokea ajali bandari ziwe na chombo maalum cha ku-*act* haraka kufanya uokozi au kuwe na helkopta moja ni kitu muhimu sana. Ni lini tutakuwa na vitu kama hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naishauri Kamati masuala kama hayo pia iweze kuishauri Serikali kwa sababu kuna matatizo mengi sana katika Ziwa Victoria na

Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia na katika mwambao wa bahari yetu kutoka Mtwara mpaka Tanga huko na visiwa vya Unguja, Pemba na Mafia vifo vinatokea lakini hatuna cha kufanya. Kwa hiyo, nashauri bandari zetu pia ziimarishwe katika masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika liko katika *section* ya 5.22 mpaka 5.28 ambapo Kamati imezungumzia huduma za usafiri wa anga pamoja na viwanja vya ndege. Msemaji mmoja aliyepita alizungumzia namna ya ndege hizi zinazo-*operate* lakini hazina viwango, zinaharibika. Katika hili, nataka nizungumzie Makao Makuu Dodoma. Tunacho Kiwanja cha Ndege lakini mpaka leo hakuna *scheduled flights* zinazokuja Dodoma pamoja na kwamba uwanja upo na unatosha pamoja na kwamba uwanja mwingine unatengenezwa lakini ipo haja ya Kamati kuishauri Serikali kuwepo na usafiri wa kawaida wa ndege za abiria hapa mjini Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kidogo kwamba Makao Makuu ya nchi hakuna *scheduled flight* katika uwanja wa ndege wetu hapa Dodoma, ni kitu ambacho hakiingii akilini. *ATC* tayari tumejikomboa kwa nini isianzishe safari za kuja Dodoma? Kwa nini *ATC* isikodi ndege ndogo ndogo zikawa zinakuja hapa? Kuna safari nyingi za Dodoma lakini hata ikitokea dharura, Mbunge amepata dharura katika Jimbo lake inamchukua siku tatu au nne kufika Jimboni lakini ingekuwa kiwanja cha ndege cha Dodoma pana ndege za abiria ingewezekana mtu akipata dharura akaweza kwenda Jimboni na siku ya pili yake au ya tatu akawahi Bunge hapa lakini hivi sasa ni vigumu. Ninaishauri Kamati iishauri Serikali au ndiyo tunaishauri Serikali kwamba suala hili linatusumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nafikiri inatosha, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU JUMA KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia hoja hii muhimu ya Kamati ya Miundombinu.

Mheshmiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuungana na wenzangu wale waliotoa salamu za rambirambi. Kwa mara nyingine nami nitoe rambirambi kwa wafiwa. Pili, natoa pongezi nyingi na za dhati kwa Chama cha Mapinduzi kwa kumaliza uchaguzi wake salama na hususan napenda nitumie fursa hii kumpongeza Waziri mwenye dhamana ya miundombinu pamoja na wasaidizi wake wote wawili kwa kuweza kufanikiwa kuingia kwenye *NEC* na hatimaye kwenye Kamati Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo kwa kuwa muda ni mfupi sasa nitumie fursa hii kuzungumzia baadhi ya maeneo ambayo yameguswa na ripoti hii ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kile ambacho ripoti imekiita ziara kwenye eneo la ujenzi wa daraja la Kigamboni kule Dar es Salaam. Imesema tu walipitia kwenye

eneo ambalo daraja litajengwa lakini hawajatupa maelezo kuhusu nini kinachoendelea. Labda nitumie fursa hii kuiomba tena Serikali kwa maana ya kuikumbusha kwamba tayari Shirika la Hifadhi ya Jamii la *NSSF* ambalo lilipewa jukumu la kusimamia na kuandaa ujenzi wa daraja hili kwa ubia. Imekwishafanya tathimini kwa maana ya kiuchumi na tathimini ya mazingira na zote hizi zimeonyesha kwamba daraja hili linaweza kujengwa kwa faida ikiwa.

Naweka neno ikiwa hasa tukizingatia kwamba gharama zilizotokana na utafiti wa *economic feasibility* zilionyesha kwamba daraja hili litagharimu takribani *Euro* 45.0 milioni. Katika hizi *Euro* 45.0 milioni ili mradi huu uweze kuwa mradi ambao ungewekeza kwa njia ya hisa basi ilibidi kufanyike mambo fulani fulani ambayo yangeweza kufanya mradi ule uwe na sura ya mvutio kwa wale ambao wangewekeza kihisa na *NSSF* ikiwa ni mojawapo. Kilichofanyika ni nini?

Serikali ya Uholanzi chini ya Shirika lake linalojulikana kwa jina la *ORIET*, ilikuwa tayari kutoa msaada kwa Serikali ya Tanzania wa asilimia 50 wa gharama hiyo ya *Euro* 45.0 milioni. Halafu Serikali hiyo hiyo ya Uholanzi chini ya Shirika hilo la *ORIET* iko tayari kutoa mkopo nafuu kwa kiwango cha asilimia 33 zile za gharama inayobakia. Kwa maana hiyo gharama ambayo itawekezwa kwenye mradi huu kwa njia ya hisa *equity* ni 17 *percent* ya *Euro* 45 milioni. Hizi ni pesa ambazo *NSSF* pamoja na wabia wengine ambao wanaweza kuwa tayari kuingia katika mradi huu wako tayari kuzitoa na wana uwezo wa kuzitoa. *ORIET* kwa taratibu zake ikikubaliwa ku-*fund* mradi huu itatangaza tenda za kimataifa. Kwa hiyo, suala la *transparency* na nani atajenga litapatikana kutokana na tenda za ushindani. Kwa maana hiyo ninapenda kuikumbusha Serikali kwamba ni vizuri wakakaribiana na hii Serikali ya Uholanzi na kuona chini ya programu ya *ORIET* kitu gani kilichababakia kufanywa ili daraja hili muhimu sana kwa maendeleo ya sehemu ya upande wa Kigamboni Dar es Salaam liweze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, napenda sasa nije kwenye eneo ambalo repoti yenyewe imesema kwamba inawezekana hawakujadili haya mambo kwa kina lakini ndiyo mambo ambayo yamekwishatokea kwa hiyo, hatuwezi kuyafumbia macho. Mambo yenyewe ni ubinafsishaji wa Shirika letu la Reli pamoja na kulifanyia marekebisho kwenye wabia wa Shirika letu la Ndege la *Air Tanzania*. Pamoja na kwamba mambo haya yametokea ndani ya mwaka huu wa 2007 na ripoti imekiri kwamba wao wamejikita kwenye yale yaliyotokea mwaka 2006, ni vizuri kwa sababu ya umuhimu wa mashirika haya mawili wale ambao kwa namna moja au nyingine tuna bahati ya kufahamu nini kinachoendelea tutumie fursa hii kueleza nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Reli tayari Serikali imekwisha tiliana saini na Kampuni ya India inayojulikana kwa jina la *RITES* kwa njia inayoitwa *concession* kwa maana ya kwamba hii kampuni ya India imepewa idhini ya kuendesha shughuli kwenye reli ya Tanzania ambayo inaendelea kuwa mali ya Serikili kufanya shughuli za kibiashara kwa maana ya kuendesha *locomotive engine* pamoja na mabehewa ya abiria pamoja na mizigo kutoka Dar es Salaam kuelekea magharibi kwa maana ya Kigoma mpaka Mwanza.

Lakini ninalotaka kusisitiza hapa ni kwamba kama alivyoelezea Mwenyekiti wa Kamati hii ya Miundombonu kwamba Serikali ilichukua muda mrefu na mara nyingi inachukua muda mrefu kuyabinafsisha mashirika kiasi kwamba hata uwekezaji kwenye mashirika hayo unakuwa haufanyiki. *By the time* ubinafsishaji unafanyika hali ya yale mashirika inakuwa mbaya kweli kweli. Nataka nisisitize hili hasa kwenye eneo la Shirika la Reli. Hivi karibuni katika vyombo vya habari kumekuwa kunaonekana hali ya kwamba picha zinaonyesha kwamba sasa treni zinaanzia Dar es Salaam zinakwenda moja kwa moja mpaka Kigoma bila kuanzia Dodoma. Lakini wanasema hali ni mbaya, mabehewa ni mabaya injini ni mbovu, ni zilezile, kila kitu ni kibovu. Sasa ni kana kwamba walifikiri au hao wanaoeleza habari hizo ni kwamba walifikiri baada tu ya *RITES* kuchukua jana basi leo mabehewa yangekuwa mapya, injini zingekuwa mpya, kila kitu kingekuwa kizuri, haiendi hivyo. Shirika hili tumekaa nalo kwa muda wa miaka minane bila kuwekeza chochote. Kwa hiyo, ni dhahiri pamoja na kwamba *RITES* wamechukua uendeshaji katika reli hii.

Lakini itachukua takriban si chini ya miaka miwili ili kuliweka Shirika hili na mabehewa hayo na injini hizo katika sura ya kuridhisha. Kwa sababu ni lazima mabehewa yagizwe, *spa*res ziagizwe, ni lazima mambo mengi yaliyosahaulika kufanyika yaanze sasa kufanyika. Upatikanaji wa *spares* ni shida, upatikanaji wa injini na mabehewa ni shida, hakuna mabehewa ya aina ya *gage* ambayo sisi Tanzania tunatumia unaweza kwenda kuyachukua *off the shelf. You have to place an order, spare parts* lazima u-*place orders*. Kuna *lead time,* kuna masuala ya *tendering* na kadhalika. Nilidhani nilizungumze hili ili wote tuelewe kwamba ni kweli *RITES* imechukua kuendesha Shirika la Reli lakini haitokuwa miujiza kwamba baada ya kuchukua jana leo basi huduma zitakuwa nzuri kana kwamba kumetokea mambo, mabehewa hayo yamekuja na *spares* zimekuja kwa haraka kama ambavyo wengine tungetarajia iwe. It *will take time,* kwa hiyo, ni lazima tuvumilie tuipe *time* kampuni hii ijipange ili iweze kurekebisha mipango yake ya *business plan* kama vile ambavyo imepatana na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, Shirika la *Air Tanzania* hali kadhalika. Ripori imekiri kwamba hii ni ya mwaka 2006. Lakini kati ya wakati huo mpaka leo tunafahamu kwamba Serikali imekwishaachana na Shirika la *South Africa.* Tulinunua hisa za *South Africa* kwa dola moja, sasa tunajipanga upya tunalijenga upya Shirika letu na matarajio yetu litakuwa zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitize sasa kuhusu Bandari. Tanzania ina bahati ya kuweza kuwa katika nafasi nzuri sana ya kijiografia. Lakini kwa bahati mbaya hatujaweza kuitumia nafasi yetu nzuri ya kijiografia kwa maana ya kuendesha uchumi wetu vizuri zaidi. Nafasi hii tukiitumia vizuri na hasa kwa kuwekeza katika Bandari zetu pamoja na reli na barabara zinazotoka mashariki kwenda magharibi uchumi wetu utapaa zaidi ya vile ambavyo tunasema unapaa. Kwa hiyo, hapa ipo haja ya kuwekeza zaidi ya vile ambavyo tunasema unapaa; ipo haja kuwekeza zaidi katika sekta ya usafiri na usafirishaji husasan katika eneo la bandari. Bandari yetu sasa katika eneo la *container* limelemewa, kuna haja ya kuongeza *container* nyingine pembeni na ile ambayo iliyopo sasa hivi kwenye *general cargo let us convert that into another container terminal* kwa sababu ndiyo ulimwengu wa usafirishaji wa baharini sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kitu ambacho hatuelewi ni kwamba kwenye ile *container service terminal* iliyopo sasa hivi nayo imelemewa. *Efficiency* si nzuri, kuna haja ya kuhakikisha kwamba *efficiency* katika upakuaji na uondoaji wa mizigo kwenye eneo la *container* la sasa hivi unakwenda vizuri ili kuhakikisha kwamba mizigo inayokuja na kupitia Bandari ya Dar es Salaam inapita kwa haraka na kwa maana hiyo kuliongezea pato la taifa la nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuzungumzia barabara ya Itigi, Tabora mpaka Kigoma na Nzega mpaka Tabora. Barabara hizi zimetajwa tu kwa kupitia katika ripoti lakini haikuelezwa *progress report* hali ikoje? Barabara nyingine tunaambiwa zinajengwa, zingine hela zinatafutwa na kadhalika. Lakini hii ya Itigi, Tabora, Kigoma na Nzega Tabora hali ikoje? Tuliambiwa zinatafutwa pesa Dubai sijui Benki ya Abu Dhabi je, hizo fedha zimepatikana, kama hazijapatikana utafutaji wake umefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maeneo muhimu katika kuuweka uchumi kijiografia ambao nchi yetu imejaliwa kuwa katika nafasi nzuri sana, kama yatakuwa sawa uchumi wetu utapaa zaidi ya vile ambavyo tunasema unapaa. Nimalizie tu kwa kuelezea eneo la *concrete*, mataluma ya *concrete* kama ambavyo ripoti imesema. Hoja ni nzuri lakini haikuwa *quantified*. Kwa maeneo mengine haikuonyeshwa kiuchumi; je, tukitumia mataluma ya *concrete efficiency* kwa maana ya *engineering*, ni sawa na *in terms of cost* ni *cheaper* kuliko mataluma mengine. Haya ndiyo mambo ambayo ripoti ingejikita vilevile ili kuwafanya wale wanotoa maamuzi waweze kutoa maamuzi ya kisayansi zaidi kuliko ya mvuto tu wa kusema tuache hiki tutumie hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu kwa uchumi wetu wa Tanzania, ahsante sana.(*Makofi*)

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia machache kuhusu taarifa ya Kamati ya Miundombinu. Lakini kabla sijafanya hivyo naomba na mimi niungane na Wabunge wenzangu kwa kutoa pongezi. Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi kwa kura nyingi sana.

Aidha, niwapongeze na Makamu wawili, Ndugu Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kuchaguliwa tena kuwa Makamu Visiwani. Aidha, nimpongeze Ndugu yetu Pius Msekwa naye kwa kuteuliwa na kuchaguliwa kuwa Makamu Bara.

Pia niwapongeze Wabunge wenzetu waliopata nafasi katika Halmashauri ya Taifa, wote waliochaguliwa nawapongeza sana lakini nimpongeze zaidi Mheshimiwa Yusuf Makamba, kwa kuteuliwa tena kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Niwapongeze pia Mheshimiwa John Chiligati, Mheshimiwa Kidawa Salehe na

Mheshimiwa George Mkuchika, kwa kuchaguliwa kuongoza Idara, Makao Makuu ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba na mimi nichangie maeneo machache ya taarifa ya Kamati. Labda nitangulize kwa kusema kwamba mimi ni mwanakamati wa Kamati ya Miundombinu kwa hiyo yale ambayo yamependekezwa nayaunga mkono na ni taarifa nzuri. Kwa kweli inabaini mambo mengi yanayohusiana na miundombinu. Lakini naomba nichangie maeneo machache tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze na Mfuko wa Barabara. Niipongeze Serikali kwa kuongeza ushuru wa mafuta katika bajeti iliyopita kwa lengo la kuongeza fedha za Mfuko wa Barabara. Hivi sasa fedha ambazo zinatokana na ushuru wa mafuta zimeongezeka na matokeo yake ni kwamba Wilaya zetu zote zimeongezewa pesa takriban mara mbili ya kiwango ambacho tulikuwa tunapokea kabla ya kuongeza ushuru wa mafuta. Maana yake ni kwamba sasa uwezo wa Halmashauri zetu ni mkubwa kuweza kuhudumia barabara zetu.

Lakini upungufu ambao nimeaona ni kwamba mpaka sasa pamoja na kwamba fedha zimeongezwa lakini hizi za Halmashauri bado hazijapokea pesa hiyo. Kwa mfano, Wilaya ya Kondoa kabla ya kuongezwa ushuru wa mafuta ilikuwa inadaiwa takriban shilingi milioni 300 kila mwaka. Hivi sasa Wilaya imegawiwa zaidi ya shilingi milioni 730 hivi. Lakini hivi ninavyozungumza ni kwamba hiyo pesa haijafika Halmashauri kwa lengo la kuboresha barabara zetu, naamini kwamba hii si kwa Wilaya ya Kondoa tu inawezekana Wilaya zote ama nyingi bado hazijapokea fedha za barabara. Ushauri wangu ni kwamba Serikali ijitahidi kuwahisha pesa hii ili iweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichangie eneo linalohusu kupandisha daraja barabara zetu. Kama unakumbuka wakati tulipokuwa tunajadili Muswada wa Barabara *(Highway Ordnance)*, kipindi kifupi kilichopita Waziri aliahidi kwamba baada ya Muswada huo kupitishwa na kuwa Sheria angeweza kuzingatia maombi ya Halmashauri ya kupandisha baadhi ya barabara ambazo zimependekezwa.

Lakini nashangaa kuona kwamba mpaka sasa zoezi hili bado halijafanyika. Wilaya ya Kondoa tulipendekeza barabara mbili zipandishwe ziwe chini ya *TANROADS*, nazo ni barabara ya kutoka Kondoa, Kwamtoro mpaka Mpendo na barabara ya kutoka Mnenya, Kisese hadi Kikore, lakini mpaka sasa barabara hizi hazijapandishwa daraja. Naomba basi zoezi hili lifanyike mapema ili *TANROADS* waweze kupewa pesa za kuweza kuhudumia barabara hizi na barabara nyingine ambazo zilizipendekezwa kutoka katika Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda nilichangie ni kuhusu barabara ya kutoka Babati Dodoma hadi Iringa. Taarifa imetaja kwamba barabara hii pamoja na nyingine ama Kamati imesisitiza kwamba ipatiwe fedha ili kazi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami uweze kuanza.

Hivi sasa hatua ambayo imefikiwa na Serikali katika maandalizi ya ujenzi wa barabara hii iko katika hatua ya Usanifu wa kina. Ombi, naomba sana mwaka kesho mwaka 2008 basi barabara hii itengewe fedha ili kazi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami uweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa nilichangie ambalo limetajwa pia kwenye taarifa hii, linahusu barabara ambazo zinasuasua ama miradi ya barabara ambayo inasuasua. Katika ukurasa wa kumi na nne kuna baadhi ya barabara ambazo zimetajwa katika taarifa hii na imesema hivi, "barabara hizi zimekwama kwa sababu mbalimbali". Moja ya sababu nafikiri ni ubovu wa mikataba ambayo imesainiwa kati ya Serikali na Wakandarasi, na mfano ni barabara ya kutoka Dodoma kwenda Manyoni na ile ya kutoka Singida kuja Manyoni. Makandarasi walikuwepo kwenye *site* lakini mpaka sasa hawafanyi kazi kwa sababu kuna tatizo kwenye mikataba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Waziri amelishughulikia tatizo hili lakini ninashauri kwamba tuwe makini wakati tunaposaini hii mikataba tuhakikishe kwamba vipengele vyote vya mikataba vimewekwa vizuri. Hapa ninachofahamu ni kwamba katika zile bei, *variation* ya bei ilikuwa haikuzingatiwa, kwa hiyo, baada ya vifaa kupanda bei watu wameweka dhana kuwa hawaendelei.

Kwa hiyo, naomba basi mikataba hiyo izingatie mabadiliko ya bei wakati itakaposainiwa ili tusiweze kukwama kama ilivyo sasa kwa baadhi ya barabara. Barabara ile inayotoka Geita kwenda Bukoba ama kwenda Chato na kwingineko mkataba wake ni mzuri sana, kazi inaendelea vizuri lakini mkataba kati ya Dodoma, Manyoni na ile ya Singida Manyoni kwa kweli umekwama kwa sababu ya vipengele hivyo ambavyo nimevitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ambalo napenda kuchangia ni hili deni la makandarasi waliotengeneza barabara, ni kweli Serikali iliwaagiza mameneja wa *TANROADS* wa Mikoa kuweka mikataba na makandarasi mbalimbali ili waweze kurekebisha barabara zenye kuharibika sana kipindi cha mvua . Na tuwashukuru sana hawa makandarasi walijitolea na walitumia fedha zao kufanya kazi hiyo lakini mpaka hivi sasa hawa Makandarasi hawajalipwa fedha.

Serikali iliahidi kwamba ingetoa shilingi bilioni 10.0 ili iweze kulipa hawa makandarasi. Sasa yapata miezi sita hakuna kilichotolewa. Kwa hiyo, baadhi ya makandarasi waliotumia mtaji wao ni kama vile wamefilisika. Ninaomba Wizara ya Fedha ichukue hatua ya haraka iweze kutoa fedha ili hawa makandarasi waweze kulipwa na waweze kuendelea na shughuli za kuhudumia barabara zetu. Baada ya kuchangia hayo machache, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba niunge mkono taarifa ya Kamati ya Miundombinu na mimi nikiwa mjumbe mmojawapo ahsante sana.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi kuweza kuchangia japo kidogo lakini katika taarifa ya Kamati hii. Nadhani Bunge hili Tukufu litakumbuka kuwa sisi Wabunge tumekuwa tukiomba sana taarifa hizi ziweze kujadiliwa humu ndani ya Bunge ili kuweza kupata

mawazo mbalimbali na pengine kuweza kutoa mwelekeo wa Bajeti ya kwenye mazungumzo yetu kuonyesha wapi kuna vipaumbele. Kwa kweli nashukuru sana kwa taarifa hii kuletwa mbele yetu.

Kabla ya kuanza, kwa niaba ya wananchi wa Kilindi na mimi naomba nitoe pole kwa msiba wa mpendwa wetu, Salome Mbatia lakini vilevile kwa Wabunge wengine ambao wamefiwa na jamaa zao na wapendwa wao. Lakini pia naomba nitoe pole kwa wote wale ambao wameumia kwa ajili au kwa matatizo mengine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kukipongeza chama tawala, Chama cha Mapinduzi, kwa kuendesha Mkutano wake Mkuu kwa ufanisi mkubwa wa kufikia malengo yake yote na hali kadhalika kufanya uchaguzi ambao umeenda kwa utulivu ambao ni mfano ukilinganisha sio tu hapa Afrika lakini hata na nchi nyingine. CCM imeonyesha Demokrasia ya kweli ambayo inafaa kuigwa. (*Makofi*)

Naomba nichukue fursa hii pia kuipongeza sana Kamati hii ya Miundombinu kwa kazi nzuri waliyoifanya na taarifa ambayo wametuletea pamoja na kuipongeza Wizara ya Miundombinu. Vilevile nimepata ugumu kidogo hasa ukizingatia baadhi ya maeneo ambayo wameyazungumzia kwenye taarifa hii tayari yana mabadiliko makubwa ambayo tumeyaona ambayo tungependa kuyajadili.

Lakini kwa sababu hayajaonekana kwenye taarifa hii na tunajadili taarifa hii inakuwa ni vigumu kidogo. Labda pengine katika siku za usoni tuangalie tutafanyaje ili kuweza kujadili mambo hata ambayo ni ya karibuni yanayohitaji kufanyiwa kazi. Kwa sababu mengine ukiyajadili utakuwa ukwenda nje ya taarifa ili hali halisi ni kwamba yamebadilika.

Mhesimiwa Mwenyekiti, Barabara. Kwanza nipongeze Kamati hii kazi nzuri walioifanya kwa kutembelea baadhi ya maeneo japo yanaonekana si mengi sana lakini kwa kweli ni mengi, nawapongeza kwa kazi nzuri. Lakini nichukue fursa hii basi niwakaribishwe Kilindi. Kilindi kuna miradi pia ambayo inaendelea na nadhani miradi hiyo itawapeni changamoto kubwa sana ndani ya Kamati yenu na kuwapeni mwelekeo mpya wa kuelekea na kutambua kwamba yale ambayo yanakusudiwa kama kweli yanakwenda kama yalivyoainishwa hayaendi jinsi yalivyo.

Mtakumbuka niliipongeza sana *TANROADS* wakati wa mchango wa Bajeti, kwa kweli walifanya kazi nzuri lakini baada ya kuwasifu, naona kidogo tena wamepunguza kasi, hata hivyo, nashukuru kwa kazi nzuri wanayoifanya. Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi inajitahidi sana, tunapopata fedha na vilevile kwa kushirikiana na kwa kufuatilia Wizarani kuweza kupata fedha mbalimbali kwa ajili ya kazi zinazofanyika.

Kwa upande wa barabara hapa naomba tu nieleze, maana yake sijui kwamba tunachangia labda kunakuwa na ufafanuzi au tunachangia ili kueleza hali ilivyo baadaye Kamati itafanyia kazi. Lakini vyovyote ilivyo naomba niseme, wakati mwingine napata ugumu hasa sisi ambao si watalaamu wa fani hii. Unakuta barabara yote ni mbovu haipitiki, kila ukienda hatua mbili tatu ni shimo, huku ni bonde na kadhalika lakini

unashangaa fedha inatolewa kidogo unaambiwa ni *spot improvement*, sasa hii *spot improvement* unashindwa kujua kwamba mna *improvement* wapi, mnaacha wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina pendekezo. Labda tunapopata fedha tufanye kiwango kidogo cha barabara ambayo inatosha ile fedha lakini kwa kiwango cha juu ambacho hamtarudia kwa muda wa karibuni badala ya kugusa hapa mnaruka mnagusa hapa. Kwa kweli mimi naona mwishoni mwa siku kazi yote inaanza upya.

Kwa hiyo, napendekeza kama haina tatizo kwenye utengenezaji wa barabara na taratibu zake, vilevile niombe barabara ambapo zinapandishwa kiwango sasa kufikia kuwa chini ya *TANROADS* ya Mkoa, naomba tuwe tuna taarifa. Kwa mfano, barabara ya kutoka Handeni kwenda Songe, hii imekuwa *up-graded* kuwa barabara ya kiwango cha Mkoa.

Hata Halmashauri haina taarifa. Nilivyoenda kwenye Kamati pale nikiwa najaribu kuwaeleza, tukawa tunatofautiana kidogo wanasema hatujapata maelekezo. Basi ni vizuri hata wakawa wanaandikiwa barua hizi Halmashauri wapate kujua hali ilivyo. Lakini hata hivyo nashukuru kwa kupandishwa kiwango barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile pale ambapo tunapitisha bajeti hapa na kuamua kwamba barabara sehemu fulani inafanyika basi kama haifanyiki ni vizuri pia barua ikaandikwa ikaenda kwenye Halmashauri ikieleza kwa nini kazi ile haijafanyika au haitafanyika. Inakuwa ni rahisi hasa sisi Wabunge tunapofika pale tunaambiwa tumesikia mmepitisha bajeti hii lakini kazi haijafanyika. Nikitolea mfano wa barabara hiyo ya Handeni Songe, zilitolewa fedha tukiamini kwamba barabara itatengenezwa kwa kufikia Songe lakini likapita greda, kweli baada ya kupita kukawa ni tope kote baada ya mvua kunyesha.

Baada ya kuwaambia jamani mbona hamuweki vifusi wakasema hatuna hela na tulipewa hela ya kupitisha greda tu. Sasa mimi naona mvua ikinyesha kazi inaanza upya, kwa hiyo, kwa kweli tunakuwa hatufanyi kitu chenye tija.

Ushauri wangu tu ni kwamba labda kama nilivyosema mwanzo tuchague yale maeneo ambayo tunaona kwamba hela hii tuliyonayo kwa safari hii inakidhi kutengeneza kiwango fulani cha barabara. Maana yake vinginevyo kwa upande wangu kule mvua zikinyesha barabara zote zinaanza moja, kwa hiyo, tutakuwa tunarudia jambo lilelile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisemee kidogo usafiri wa anga. Niliwahi kuchangia hapa kuhusu Uwanja wa Ndege wa Julias Nyerere. Mimi nafikiria tuangalie mbali kidogo miaka 50 ijayo, tuangalie pia tunavyokwenda, sasa hivi tunaanza kuwa kijiji. Dunia nzima matukio yanakuwa ni mengi. Sasa mimi nafikira kwanini tusianze kufikiria sasa hivi kuhamisha ule uwanja tukaenda tukatafuta eneo kubwa kabisa. Maeneo yapo wazi, lakini siku zinavyozidi kwenda tutazidi kubanana na mwishoni tutakosa.

Napendekeza hata kule maeneo ya Kibaha twende nje, mbona nchi nyingine zipo mbali sana na mijini tujaribu kwenda mbali, badala ya kuendelea kulipa fidia watu

tunabanana pale pale na ilhali tunajua kwamba tunazidi kupanuka. Miaka 50 mbele itakuaje. Sasa mimi nasema niache hiyo changamoto kwamba tufikirie kupanua zaidi huo Uwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwanja wa Ndege wa Tanga, kweli uwanja upo, nimeona kwenye taarifa ukarabati unaendelea. Kwa kweli naomba niseme hata kama ukarabati unaendelea basi ukazaniwe, kwa sababu naamini njia mojawapo kuna watu wengine wanapenda kwenda kuwekeza Tanga, anakuja kwa muda mfupi mwekezaji mkubwa lakini unakuta hana ule muda. Akifikiria saa ya kutoka na gari Dar es Salaam mpaka Tanga atakuwa anashindwa. Kwa hiyo, nayo pia itatusaidia kwenye wawekezaji lakini pia itatusaidia kwenye mambo mengine mengi hasa kwenye matumizi ya bandari yetu, wengi watazidi kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa usafiri wa anga, nilikuwa naomba basi, kwa sababu Kilindi kwa kweli tuna matatizo mengi sana ya barabara, hilo silo jambo la kufanyika siku moja. Serikali imetusaidia kwa kiwango kikubwa, tunakiri na tunashukuru. Lakini kutokana na hali yenyewe ilivyo, kwa kweli inakuwa ngumu. Kwa hiyo, nafikiri *Air Strip* ingeweza kutusaidia pale ili angalau pengine wawekezaji waweze kufika maeneo yale na hata viongozi ambao wanashindwa kufika kwa sababu ya barabara mbovu wakaweza kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Bandari ya Tanga, nataka niulize kitu kimoja tu; hivi kitendawili gani kipo kwenye matumizi ya ile Bandari? Tatizo ni nini? Kwa sababu wenzetu wa Kamati mlifika, labda tunaweza tukajua, tatizo ni nini? Kwa sababu nikiwa katika Bunge la Afrika Mashariki, tulikwenda pale.

Kulikuwa na malalamiko mengi sana kuhusu upotevu wa mizigo kwenye Bandari ya Mombasa, wingi wa mizigo kwa wakati mmoja kwenye Bandari ya Mombasa. Sasa, tukasema ile ya Tanga, tatizo ni nini? Labda tupate ufafanuzi kwenu, kwa sababu mimi nadhani kama wengine walivyosema ile Bandari itasaidia kwa kiasi kikubwa. Ninaomba tu tujue tatizo ni nini ili hata ikibidi basi tujue tunafanya nini na sisi Wabunge wa Tanga tujue tunachangia vipi ili kuweza kuhamasisha kazi hiyo iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mawasiliano, kwa kweli napenda niishukuru sana *Celtel*, *Vodacom* na *Tigo* kwa kufunga minara. Lakini bado eneo kubwa sana la Jimbo, nusu ya Jimbo la Kilindi hakuna huduma hizo. Kwa mfano katika Kata za Lwande, Kikunde, Pagwi, Kilindi, Masagalu na Msanja, nimekwishapeleka maombi na Halmashauri imepeleka maombi, basi tunaomba wanaohusika watusaidie kuweka msisitizo ili hawa watu nao wajisikie wako karne ya 21.

Vilevile kuna tatizo sugu la malipo katika ile mikataba na Vijiji. Sasa hivi 2005, 2006 na hata 2007, malipo hayajafanyika. Tunajaribu kufuatilia, basi wahusika kama wapo, tunaomba watusaidie kuweka nguvu ili angalau huduma hiyo na makubaliano hayo yafanyike. Pamoja na Waziri kuahidi kwamba *TTCL* wangefunga mitambo Kilindi, mpaka leo naona ile kazi nadhani bado iko kwenye utaratibu. Lakini ni muda kidogo,

miaka karibu miwili sasa. Ninaomba basi msisitizo angalau na *TTCL* na sisi tuweze kutumia *Fax* na mambo mengine kupitia *TTCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naamini wale wanaohusika kutengeneza bajeti wamesikia. Hii sekta ni muhimu sana ambayo kwa kweli wanavyosema wajumbe wa Kamati ni kwamba bajeti ndiyo tatizo. Kwa hiyo, kwa sababu saa hizi wanaanza kuandaa bajeti, mipango inaanza na *ceiling* zinaanza kufikiriwa, basi naomba na mimi niongeze sauti yangu. Hapo kwa kweli wafikirie bajeti itakayokuja iwe na sura tofauti ili waweze kufika na hata maeneo ya pembezoni kama Kilindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na asante kwa kunisikiliza! *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, nami niungane na wachangiaji waliopita ili niweze kutoa rambi rambi kwa msiba uliotufika sisi Wabunge pamoja na familia nzima ya Marehemu Salome Mbatia aliyekuwa Mbunge mwenzetu. Pia niwape pole wale wote walifikwa na maswahibu kama hayo, waliofiwa ambao ni Wabunge wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia niupongeze Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi uliomalizika hivi juzi kwa kazi nzuri iliyofanywa kwa kumchagua Mwenyekiti wetu, mpendwa wetu, Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliyejizolea kura nyingi, na kuwachagua Makamu wake wawili, Bara na Visiwani na pia kumchagua Katibu Mkuu, Mzee wetu Rajab Yusufu Makamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue nafasi hii nitoe pongezi za kipekee kwa Mheshimiwa John Chiligati. Mheshimiwa John Chiligati ni Mbunge mwenzangu tunayetoka Mkoa mmoja. Na kwa sisi watu wa Singida, tulikuwa tukimtabiria mema toka alipochukua *form* na kwa kweli tunamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa nafasi aliyoipata, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia nipomngeze Mwenyekiti wa Kamati hii ya Miundombinu, Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga. Huyu Mwenyekiti, ni mahiri sana na ndiyo maana naamini hata sisi wenyewe wa Mkoa wa Singida, Wabunge wa Singida ni Mwenyekiti wetu. Kwa hiyo, nampongeza sana pamoja na Kamati yake yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie katika kujadili juu ya taarifa hii ya Kamati iliyoletwa mbele yetu. Kamati hii ni muhimu sana na ni Kamati nyeti sana na ndiyo ambayo inatuunganisha kimawasiliano kwa nchi nzima. Kama Kamati inaweza ikafanya kazi vizuri ya kuishauri Wizara, basi utekelezaji wa Ilani hata ya Chama utakwenda vizuri sana. Kwa hiyo, ninaweza nikasema kwamba Kamati hii ni nyeti sana na ina majukumu makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipitia taarifa na katika kusoma taarifa ya Kamati, kwa sababu Kamati zote za Bunge zimeundwa kwa mujibu wa Kanuni ya Bunge ya 98,

pamoja na mambo yote katika kutekeleza majukumu yake, sijaona mahali ambapo pengine Kamati ingetoa ushauri au maoni, inaonaje katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka uliopita? Ilikwama sehemu gani na inahitaji iboreshwe kwa kiasi gani ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi kwa mwaka unaokuja. Hili sijaliona na ninaomba basi katika Kamati zingine wakati mwingine tunapokwenda tuhakikishe tunazingatia hili kwa sababu sisi tunaleta maoni ili tushauriane na tuweze kuweka uboreshaji kwa utekelezaji mzuri kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii inajadili na inapitia bajeti ya Wizara nzima kabla ya kuletwa kwetu sisi au kuletwa katika Bunge hili na inatoa ushauri na ushauri ule unafanyiwa kazi na baada ya kufanyiwa kazi, baadaye unaletwa hapa kwa makubaliano na Kamati na Wizara husika. Sasa nasema kazi ya Kamati ni nzito sana na ninaomba nishauri mambo yafuatayo ambayo naona kwamba Kamati inapaswa iyaboreshe ili tuweze kuondokana na matatizo ambayo mara kwa mara tumekuwa tukiyalalamikia.

Nikianzia na suala la barabara, naishukuru Serikali ya Awamu ya Nne katika utekelezaji wake wa ahadi kama ilivyoahidi na kwa kweli nashukuru sana na hasa ninavyoweza nikazungumza nikiwa nimesimama hapa leo, hii barabara kubwa ambayo inaunganisha Jimbo langu, yaani barabara ya Kati, eneo ambalo barabara ya lami iliishia, iliishia eneo la Malendi, Shelui ambapo unaingia Mkoa wa Tabora katika Wilaya ya Igunda. Sasa barabara ile ipo tayari kutoka pale Malendi hadi Singida na imebakia asilimia tano tu ambapo ni kwenye yale madaraja ya mlima Sekenke ambapo haijawekwa lami. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa kazi nzuri na naamini Kamati ndiyo iliyoshauri na ndiyo iliyoweza kutoa kipaumbele kuisukuma Wizara na ikafanya kazi hiyo vizuri zaidi. Kwa hiyo, hili nashukuru sana na naishukuru Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuzingatia na kuweza kuangalia na kusikiliza kilio cha wananchi na hasa kilio cha wananchi wa Jimbo langu na Mkoa mzima wa Singida. Nataka niishauri Kamati, wakati inapokutana na Wizara, kwa nini isiwe na mpango wa kuishauri Wizara, tuwe na barabara hizi tunazotengeneza kwa kiwango cha changarawe? Barabara hizi tunazitengeneza mwaka hadi mwaka, hatujapata dawa ya kuhakikisha kuliko kupoteza pesa nyingi kwa mwaka mmoja na ili sasa tupate dawa itakayoondoa kwamba tutaondokana na hili tatitizo, tukitengeneza barabara tuwe tumetengeneza barabara kwa muda wote na pasiwepo matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimshauri Mwenyekiti wa Kamati watakapokutana mara nyingine na Wizara washauriane, tuone umuhimu kwa nini sasa tusianze na barabara japo kwa ile pesa tuliyonayo, ambayo ni kidogo iliyopitishwa na Bunge, pesa hiyo ianze kwa kutengeneza barabara ya lami, hata kwa kiwango kidogo. Na ili mwaka unaofuata tutakapokuja katika Bunge hili tukapitisha pesa, pale tulipoishia tunaendelea kutoka pale na tunaendelea hata kama tutatengeneza kilomita tano tano kwa kila mwaka kwa kila Mkoa, itatusaidia sana kuliko kupoteza mamilioni ya pesa kila mwaka na kila mwaka tunaidhinisha pesa, tunapoteza pesa.Kwa hiyo, napenda nishauri tu kwamba Kamati hii ione, iweze kushauriana na Wizara ili tusipoteze pesa nyingi, kwamba tuweke vipaumbele kwa kuhakikisha kwamba tunaanza kutengeneza barabara ambazo ni za lami. Na kama tutashindwa zaidi, tuanze basi hizo barabara hata za lami nyepesi ile *otta seal*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizo, nasema zinasaidia sana. Mimi nina kumbukumbu, Mlima Sekenke, waliweka lami nyepesi, iliweza ikakaa pale karibu kwa muda wa miaka 10 na ilikuwa inafanyika kazi ndogo tu ya ukarabati, na ukarabati ule ilikuwa mahali panapobomoka, inarudishiwa. Sasa kama tutahakikisha na tukafanya kazi hiyo nzuri, naamini tutaondokana na matatizo na tutaondokana na tatizo la kupoteza fedha nyingi kila mwaka kwa barabara ambazo tunatengeneza kwa changarawe na zinakuja kuzolewa nyakati za mvua. Lingine ninalotaka kuulizia, labda ningeomba Kamati ilitilie mkazo, ni juu ya suala *contractors* wanaopewa kazi za kujenga barabara na kujenga majengo mbali mbali ya Serikali. Kwa nini *contractors* hawa wanapokuwa wanatengeneza hizi barabara, wanatengeneza kwa kiwango hafifu? Mbali ya uhafifu na viwango vyenyewe haviridhishi! Tatizo hili linatoka wapi? Kwa hiyo, ninaomba Kamati itakaporejea tena ihakikishe inaziba mianya ya namna hiyo ambayo naamini kwamba hili suala linaweza kujitokeza ambalo linatukosesha imani na watu na inaonekana tumepeleka kiini macho kwa wananchi, likaondoka kwa sababu viwango vinavyotengenezwa vinasikitisha sana. Viwango vya madaraja vinasikitisha, mfano ni kwamba ile barabara ya Sekenke ambayo ndiyo hii mpya, yale madaraja 6 ni *Contractor* aliwahi kutengeneza na alilipwa mabilioni ya pesa, lakini yalikuja kuzolewa na mvua ilipofika. Kwa hiyo, lazima tuangalie, tuzibe mianya ya kupoteza fedha nyingi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru sana Kamati kwa ushauri wake mzuri hasa kwa kushauri Shirika letu la Ndege *(ATCL)* kurejeshwa mikononi mwetu. Lakini naomba wakati tunalirejesha hili Shirika, Kamati ishauri na Wizara ihakikishe kwamba hili Shirika linakuwa ni Shirika la kisasa, lisiwe Shirika ambalo tumelizoea sisi. Shirika linaloendana na wakati, Shirika litakaloingia katika ushindani wa kibiashara. Tusiwe na Shirika ambalo litakuwa maadamu tumerejesha tu, lakini tukiliweka katika soko, likawa haliwezi kwenda mbele. Watanzania tunaelewa sana masuala ya utandawazi na kwamba sasa hivi tunaona mazingira ya ndege mbalimbali na ushindani wa biashara. Ndege zetu kama tutakuwa nazo zilezile ambazo tulikuwa nazo wakati ule na huduma zitaendelea zilezile, nakuhakikishia kwamba bado hili Shirika la Ndege hatutalipeleka mbele na Shirika la Ndege litarudi tena, litaanza kuchechemea na baadaye tutafika tutalibinafsisha na tutakosa kabisa kuweza kuliendesha. Kwa hiyo, ili tuweze kufanya vizuri, ni lazima Kamati ihakikishe kuwa inalishauri hili Shirika lifanye mageuzi ya kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niongezee hapo hapo kwamba Kamati ishauri Wizara kwamba upo umuhimu basi hapa Dodoma tunaomba japo tupate usafiri wa Ndege, kwamba Ndege ije hapa. Kuna mashirika ya Ndege tuyashawishi ili yaweze yakafika hapa yafanye safari za kuja ili tupunguziwe adha kwa sababu watu wanaweza wakafanya uchaguzi wa safari, wapo wanaotaka Ndege, wapo watakaosafiri na usafiri wa barabara, wapo wanaotaka kusafiri na Treni. Hapo ndipo tunaposema tuna maendeleo na ndipo tunaposema tupo katika ushindani wa suala la Dunia ya Utandawazi. Nizungumzie Shirika la Reli. Singida tuna treni ya abiria, na treni ya abiria, Singida….!

*(Hapa Kengele ililia)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naomba niiunge mkono hii taarifa nzuri iliyowasilishwa. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi mchana huu ili nami pia niweze kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu. Kwanza na mimi nianze kutoa rambi rambi kwa watu wote waliopatwa na matatizo. Lakini pia nichukue nafasi hii kukipongeza Chama chetu, Chama cha Mapinduzi kwa kufanya uchaguzi uliofanyika kwa heri na umekwisha kwa salama. Lakini kubwa zaidi, kwa jinsi ambavyo demokrasia imeshamiri kwenye chama chetu, nimalize kwa kusema nawapongeza viongozi wote waliochaguliwa na walioteuliwa na niwaombe waendelee kukiongoza chama chetu ili tuweze kuendelea kuongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwanza, nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati kwa Ripoti yake nzuri kabisa. Lakini mimi kwenye ripoti hii nina mambo machache sana ambayo ningependa nichangie ili tuweze kwenda vizuri. La kwanza ni la upande wa barabara. Wakati anachangia Mzee wangu, Mheshimiwa Degera, amelisema kidogo, lakini na mimi naomba hili nianze nalo. Mwaka jana tulipata tatizo la mvua, barabara nyingi sana zikaharibika. Tulikuwa na *emergency*, tukaamua kuwaomba Mameneja wetu wa *TANROADS* watafute makandarasi wafanye hizo kazi. makandarasi hao waliofanya hizi kazi ni Watanzania wenzetu tena ni wale ambao ni wadogo, ambao kila siku tunaongea namna ya kuwafanya wakue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ambacho kinanipa tabu kidogo, ilikuwa ni *emergency*, mpaka leo tunavyoongea wengi wao hawajalipwa. Sasa matokeo yake ni nini wasipolipwa? Sasa hivi kwenye bajeti ya mwaka huu tuna pesa nyingi sana za kufanya *maintenance* ya barabara. Hawa makandarasi ambao wanadai hawatakuwa na uwezo wa kufanya hizo kazi kwa sababu wengi unakuta wanadaiwa mafuta, wanadaiwa sijui walikuwa wanachukua vitu gani, kwa hiyo, wale waliokuwa wanawakopesha na wao hawawezi kwenda leo tena akasema amepata kazi, "nikopesheni!" Serikali yetu hatuwezi kuwakopa hawa watu, matokeo yake hawatafanya kazi, matokeo yake pesa hizi tulizopata nyingi, tutafika mwaka kesho bado hizo pesa zipo, watu hawajafanya kazi, tutaanza kumlalamikia Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali, hawa ni Watanzania wenzetu, ni watu waliotusaidia wakati tuna shida, siyo jambo jema kabisa kuendelea kuwakopa. Siyo jambo jema kabisa! Na mimi naamini uwezo tunao! Uwezo tunao, kwa sababu hili lilikujwa ni suala la *emergency* na tukasema tutatenga *ten billion* kwa ajili ya *emergency*. Haiwezekani tunasema leteni *certificate*! *Certificate* zimeletwa, zimekaa Wizara ya Fedha, wanaangalia! Wanaoangalia *certificate* siyo waliosimamia hiyo kazi! Hapa mimi napata matatizo kidogo! Mimi nilidhani, kuna *Agency*. Wakala wetu ni *TANROADS*, ndiye aliyesimamia zile kazi, ndiye anaweza kuonyesha kwamba hii *certificate* ni ya haki au siyo ya haki. Lakini unasema lete *certificate* hii, *certificate* tuletee Wizara ya Fedha ndiyo tuwalipe. *Number one*, Wizara ya Fedha hawakuona wakiwa wanafanya hizo kazi.

Wizara ya Fedha wana mambo mengi, matokeo yake zimekaa pale, watu wetu hawalipwi, kazi haziendi na tunategemea hawa hawa makandarasi watufanyie kazi kesho. Mimi naamini tutakuja mwaka kesho, tutasema barabara hazikutengenezwa, ndiyo itakuja ile lugha kwamba, tumetuliongeza fedha nyingi wakati uwezo haupo. Mimi naamini uwezo upo, lakini tujitahidi tuwalipe watu hawa ili waweze kuendelea na kazi. Ninaomba sana hili tulifanye, *it is a priority. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kusema kuhusu barabara, maendeleo yoyote ya nchi, miundombinu ni *focal point* ya maendeleo. Hatuwezi tukaenda mbali, hatuwezi tukakuza uchumi wetu bila miundombinu, kwa lazima tufanye maamuzi magumu. Lakini hata miundombinu, hii kwa sababu tuna pesa kidogo, lazima tujue tunazipeleka wapi, wapi tuki-*invest* tutapata pesa yetu. Ndiyo hapa tunapokuja, uchumi wa jiographia na bahati nzuri nchi yetu imezungukwa na *landlocked countries*. Tukiweza kutumia vizuri reli yetu, tukatumia vizuri bandari yetu, tukatumia vizuri barabara zetu na anga, katika nchi hii, *contribution* ya hii *sector* kwenye *economy* itakuwa kubwa mno! Tunasema, tunategemea *agriculture* ndiyo *backbone* ya *economy* yetu, mimi nakubali kabisa. Lakini hiki kilimo hakiwezi kufanikiwa kama hakuna *infrastructure*. Hayuko *serious investor* atakuja, umpeleke Kigoma akalime wakati namna ya kutoa mazao Kigoma haipo. Mimi naamini mipango iko vizuri sana, Ilani yetu inasema vizuri sana. Sasa lazima twende kwenye kuyatekeleza hayo. Nimesoma kwenye hii ripoti, ukiangalia barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora – Kigoma, imetajwa *by the way*, najua yako yanayoendelea, nayajua lakini naomba tuyafanyie mkakati twende haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo la msingi kwenye barabara ni kwamba ukiangalia sasa kuna barabara ambazo tuna *tender* leo, ukiangalia ile *tendering process*, ni miezi sita mpaka mwaka mmoja. Inafika mwaka mmoja watendaji wetu wanatwambia hapa hakuna aliyepatikana anayeweza kujenga hii barabara, tuna-*re-tender*. Hapa tunaongea *another year!* Wananchi wetu hawatakuwa wanatuelewa. Hatuwezi tukawa tunasema kila siku, “tuko kwenye mipango”, “tuko kwenye mipango!”

Barabara mmehangaika nayo, *tendering process* inafika, mnasema hakuna aliye-*tender!* Na mki-*re-tender* maana yake ni nini, gharama imeongezeka. Kwa hiyo, bajeti ile mliyopanga haitaweza kufanya hiyo kazi. Mfano kama kazi ungeifanya kwa bilioni 10, baada ya miezi 6 au mwaka mmoja, ukasema na-*re-tender* kwa sababu hamna anayeweza kuifanya hii kazi, unapoi-*re-tender* maana yake ni bilioni 20. Kwa hiyo, nasema haya yote lazima tuyaangalie kwa ukubwa wake ili tuweze kuyapeleka mbali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *ICT Backbone* (Mkonga wa Taifa). Ili tuweze kuendelea, hizi gharama za simu tunazosema zipungue, lazima *ICT Backbone* iwe *in place*. Niiombe Serikali hili tulipe kipaumbele. Lakini lingine ni suala la *Postal Code*, hii ni *Project* ya maana sana. Leo tunaongelea vitambulisho vya uraia, hivi vitambulisho vya uraia, kama hatuna *Postal Code*, hatuwezi kufanikiwa. Kwa hiyo, lazima *Project* hii nayo tuipe pesa za kutosha ili tuweze kuitekeleza. Ni suala muhimu na wanasema kupanga ni kuchagua, mimi nawaombeni tuchague haya , mambo mengine yatawezekana tukishafanya haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ninataka tu nichukue nafasi hii kwa sababu uliniambia muda ni kidogo na nimeupata, kwa kipekee kabisa, nimpongeze Waziri wa Miundombinu kwa kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa *NEC* na hatimaye kuwa Mjumbe wa *CC*, ninaamini atatusaidia sana. Lakini pia, nimpongeze Mheshimiwa Maua Daftari, naye kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa *NEC* na kuwa Mjumbe wa *CC* na nimpongeze Mheshimiwa Milton Makongoro Mahanga, kuchaguliwa kwenda kwenye *NEC*. Ni matumaini yetu watakisaidia Chama chetu. Baada ya kusema hayo, naomba na mimi niunge mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Nitajitahidi kwa kifupi. Kwanza, niipongeze Kamati kwa kutoa taarifa hii ya utekelezaji wa shughuli za Kamati ya mwaka 2006. Kuniona mimi nimesimama hapa pamoja na Mheshimiwa Waziri, wanajua nataka kuzungumza nini. Hoja yangu ni Kivuko cha Pangani, *priority* namba moja. Kama kweli Waziri anatupenda watu wa Pangani, kwa kweli suala la Kivuko linatutesa. Hali ni mbaya, mbaya sana! Sasa tusifike pahala tukaanza tena tukaulizana, “lakini si niliwaambia!” Haitusaidii! Serikali yetu hii ni moja, ni Serikali yangu, naamini inajitahidi. Lakini nina maswali machache ya kuiuliza tu Serikali. Tunafahamu bajeti ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne katika Kivuko cha Pangani, waliahidi na tenda ikatangazwa, Mzabuni akapatikana, akabadilisha, akataka kuongeza masharti mengine ambayo sheria hairuhusu, mkafuta tenda ile. Sawa, akaenda Mahakamani, kukawa na tatizo la barua kutoka *World Bank* ambayo inajulikana kama *Letter of no Objection*.

Hatimaye baada ya kama mwaka mmoja Benki ya Dunia ikatoa barua ambayo inajulikana kama *Letter of no Objection*. Sasa tulitegemea baada ya muda mfupi tu Serikali ingetangaza tenda nyingine kwa sababu hata katika bajeti iliyopita Serikali imetenga fedha kwa ajili ya Kivuko cha Pangani. Kwa hiyo, sasa hivi tuna fedha za Serikali, tuna fedha za *World Bank*, lakini kwa masikitiko nasema mpaka leo hii, sijui labda gazeti la leo, hakuna chochote katika magazeti kusema kwamba kuna taarifa ya watu wanatakiwa wazabuni kwa ajili ya Kivuko cha Pangani. Hii inatuumiza. Kivuko cha Pangani kinafanya kazi kwa injini moja. Kwanza, injini zote mbili, *propeller shaft* zote mbili tunakarabati. Lakini Serikali ilijitahidi ikatuletea *propeller* moja kutoka sijui maeneo gani, wakaja wakaifunga, ndiyo maana Kivuko kile kinatembea kwa ijini moja na *propeller* moja. Upande wa injini ya pili, hamna chochote. Lakini nafahamu kwamba ijini ya pili inakarabatiwa pale Tanga. Basi tuleteeni hiyo *propeller* nyingine ifungwe pale angalau kile Kivuko kifanye kazi kwa ijini mbili. Mwenyekiti ulifika Pangani na kasi ya maji ya Mto Pangani unaifahamu. Tutakuja kuwaumiza wananchi wetu na sisi ndiyo tutakaobeba mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Kamati yako, tusaidiane kuihimiza Wizara watangaze hiyo tenda. Toka wakitangaza mpaka Kivuko kije, itachukua mwaka mzima mwingine. Hivi tutakaa vipi mwaka huu mzima bila ya Kivuko ambacho kitakuwa ni salama? Basi tengeni fedha za kutosha angalau kile Kivuko kikarabatiwe kwa kiwango kikubwa sana. Lakini ukarabati mdogo mdogo ambao Kamati imehimiza humu, kwa hali ya Kivuko cha Pangani unahitaji *Major Repair* kwa sababu ni *obsolete* sasa hivi.

Hilo la kwanza. Mimi sina zaidi ya kuongezea katika Kivuko cha Pangani. Lakini Mheshimiwa Waziri Chenge mara kwa mara baada ya salamu mimi na yeye, tunakumbushana Kivuko cha Pangani. Sasa na Mwenyekiti wa Kamati tafadhali sana na Kamati yako, Kivuko cha Pangani ni tatizo, tunapata tabu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nataka kujua suala la Bandari ya Tanga ambayo kunatakiwa kujengwe Bandari mpya katika eneo la Mwambani, lakini, katika taarifa yako haikusema lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka Rais Yoweri K. Museveni alipokuja Tanga kutembelea Bandari ile ili tujenge reli kutoka Tanga kwenda Musoma iweze kuisaidia Uganda, katika kufanyia *feasibility study* ya Bandari ile pamoja na reli, wakati ule gharama ilikuwa ni dola milioni 4.

Tulikubaliana na Serikali ya Tanzania na Uganda kwamba tuchangie gharama hizo, kwamba milioni 2 iwe ni Tanzania na milioni 2 iwe ni Uganda, lakini hakuna kilichofanyika. Gharama za leo za kufanya fea*sibility studies* inaweza ikawa ni maradufu , kwa hiy,o kama hatukuweza kwa milioni 2, sijui sasa kama ni milioni 4 ama 6 itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijui tatizo liko wapi lakini nataka kusema tu kwamba miradi kama hii ya baadaye ikitaka Serikali ndiyo ijenge haitaweza, ni bora kutafuta wawekezaji wajenge bandari na hatimaye Serikali ijikusanye kwanza. Lile eneo lipo katika *EPZ* sasa sijui tatizo liko wapi? Nafahamu kuna wawekezaji walikuja wameonesha *interest* lakini taarifa yako Mwenyekiti haikueleza juu ya suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi yangu mawili ni hayo, kivuko cha Pangani kama kutakuwa na maelezo mazuri basi, lakini angalau wananchi wawe na matumaini na Serikali yao ama sivyo tunakwenda kubaya. Nakushukuru na naunga mkono hoja hii ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, ahsante sana.

**MHE. JOB I. NDUGAI – MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mohamed Richard Abdallah, kwa mchango wako. Sasa kuna karatasi moja ilijichanganya kidogo nimeipata sasa hivi ya Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia lakini itabidi atanguliwe na Prof. Raphael Benedict Mwalyosi na kwa sababu wote wawili ni maprofesa, naomba kila mmoja wenu atumie dakika zisizozidi kumi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa nami nichangie kwenye ajenda iliyopo mbele yetu.

Kwanza, na mimi kwa sababu sijazungumzia masuala ya huzuni, naomba nitoe rambirambi zangu kwa niaba ya wananchi wa Ludewa, kwa familia ya Mheshimiwa Salome J. Mbatia ambaye ametutoka, tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema, *Amen!*

Pili, naomba niwapongeze wote kwa pamoja waliopata nafasi mbalimbali kwenye *NEC* pamoja na Kamati Kuu, nawapongeza sana pamoja na ndugu zetu Mawaziri wa Wizara hii tunayoizungumzia.

Nilitaka kuchangia tu kwenye maeneo matatu hapa, kwanza, kwenye suala la mawasiliano nataka kuyashukuru mashirika ya *Vodacom, Celtel* na *Tigo* kwa kusambaza mtandao katika Wilaya yetu ya Ludewa tukilalamika wakati mwingine tutakuwa tunakufuru. Kiasi cha kusambazwa kwa mawasiliano katika Wilaya ya Ludewa kinaridhisha na tunashukuru kwa hicho kilichofanyika na tunaomba waweze kuendelea kukamilisha maeneo yaliyobaki, nilitaka nishukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama walivyochangia wenzangu, maswala ya makampuni haya kutokushirikiana kuchangia gharama za kujenga hasa minara ile inakuwa mingi, kwenye *public* mnapopita minara *almost everywhere* sio sura nzuri sana, wanaweza kabisa kuchangia gharama za kujenga minara ili kupunguza athari za mazingira pengine hata na kelele pamoja na mionzi inayotokana na mitambo inayoendesha minara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kunakuwa na *pollution* kwa sababu kuna ku-*service* hiyo minara inayoendesha vituo hivyo na kadhalika. Kwa hiyo, suala limezungumzwa mara nyingi sana, lakini ni mara chache sana tunaona makampuni haya yanakuwa tayari kushirikiana na sijui ni kwa nini kitu ambacho kingeweza kuwa ni kwa faida yao wao wenyewe wakawa kama wana-*share* gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie katika usafiri wa majini. Napenda kukubaliana na wenzetu wa Kamati kwenye Ibara ya 5.1.3 kuhusu matengenezo ya mara kwa mara ya vyombo vya majini na hapa nilitaka nisisitize kwenye maeneo ambayo hawafiki sana hata Kamati.

Katika ziwa Nyasa sijawahi kusikia hata siku moja kwamba Kamati imekwenda kule. Mimi ningewashauri watembelee ziwa Nyasa labda mwingilie Kyela mkatokee Mbambabay halafu mwende wakati wa mwezi wa sita ama wa saba ili mpate athari wanazopata wananchi wa kule. Kwa kufanya hivyo ndipo mtaweza kuisukuma Wizara hii itusaidie kuhakikisha kwamba kunakuwa na matengenezo ya mara kwa mara ya vyombo hivi vinavyofanya kazi katika ziwa lile ambalo wote tunajua *is the roughest lake in the world*, kwa hiyo ku-*travel* katika ziwa lile na vyombo ambavyo sio vizuri ni kuhatarisha maisha ya wananchi kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nakubaliana na hoja iliyopendekezwa na Kamati kwamba tujenge vyoo maeneo ambayo wasafiri wanaweza kukaa wakati wakingojea kusafiri. Wanakaa kwenye mvua, jua na hata mahali pa kujisaidia hamna sijui kwa nini, nadhani hiki kitu hatujakiangalia sana lakini *is very strange*, sasa hivi hata kwenye barabara tunasema kwenye *high ways* kuwe na *pool off the road,* watu wanafanya shughuli zao. Lakini hata kwenye maziwa haya hivi vitu ni vya muhimu kusudi watu waweze kupumzika, kujikinga na mvua lakini pia hata na jua vilevile. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa kuzungumzia kwa upande wa ziwa Nyasa tusaidie meli hizi kwenye ziwa lile. Maeneo mengi karibu yote ukiacha Kyela sina uhakika na Bambabay ambapo meli zikifika *passenger* kuna geti au eneo la kuweza kutoka kwenye meli au kwenye boti na kuingia nchi kavu au *vice-versa*.

Vituo vingi ninavyovijua kandokando ya ziwa nyasa *you have to get out* na utumbukie majini na kama wewe hujui kuogelea ni hatari sana kwa sababu wakati mwingine maji yanakuja mpaka kiunoni utembee uende nchi kavu au uingie kwenye meli. Sasa kwa nini maeneo haya hatuyatengenezei utaratibu wa kuhakikisha kwamba meli ina *anchor,* kunakuwa na utaratibu mzuri wa kushuka kwenye meli na kuweza kuwa na usalama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la barabara. Kwanza sasa hivi linazungumzwa suala la kujenga viwanda vya *sponge* kule Ludewa kwa kutumia chuma kilichopo lakini kwenye vilima vidogovidogo. Kuna vilima vingi sana ambavyo vina chuma cha Liganga lakini kuna vingi sana vilima vina chuma ambapo wanataka sasa wapewe wawekezaji wadogo wadogo hasa wazalendo waweze kuzalisha *sponge iron*.

Lakini maeneo yote hayo *infrastructure* ni *very poor* au hakuna, sasa sijui Wizara hii inalionaje hili, *how do you send people* unapeleka wawekezaji kuanza kuchimba chuma na kujenga kiwanda? Hivi vifaa vya ujenzi na hicho chuma kikiwa tayari watapitishia hewani au watapitishia kwenye barabara za tope, *does it work that way*?

Sasa sijui kama Kamati mngeweza kushauriana na Wizara tuone ni lini wataanza kuyaangalia mambo haya *in totality* wakati wanazungumza kwamba kazi za kujenga hivyo viwanda ni kwa kasi mpya, wanataka ifikapo 2010 kuwe kunaonekana kwamba viwanda hivi vimeanza kujengwa au vipo na pengine vinaanza kuzalisha sasa Barabara au miundombinu iko wapi? Mimi ninawakaribisha wanakamati vilevile mtembelee maeneo haya mkiweza nendeni Liganga na hata Mchuchuma muone miundombinu iliyopo na mwangalie mtaishauri vipi Wizara kuhakikisha kwamba Miundombinu ile inakuwapo kabla pengine hata viwanda hivi havijaanza kujengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilidhani ni suala zuri kuzungumzia Barabara ya kutoka Itoni kwenda Manda. Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika alipita huko juzi juzi lakini Barabara ile na nikimsemea Ndugu yangu , ni aibu sana kwa Wizara hii kumwachia Naibu Spika wetu anakuwa na Barabara mbaya namna ile kwenye jimbo lake lakini wanaoumia ni watu wa Ludewa ambao sisi tupo mwishoni mwa ile Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliona jinsi Barabara ilivyo na mashimo makubwa ambayo magari yanayobeba mahindi yanashindwa kupita na sasa hivi mvua zimeanza kunyesha Ludewa yamekwama barabarani kwa sababu Barabara hazipitiki. Lakini ni eneo nyeti la maendeleo, kuna uwekezaji mkubwa lakini barabara ni duni, wanachofanya kila wakati wanarudishia tope lilelile, mvua ikinyesha inatoa lile tope mashimo yanabaki palepale ambapo ilitakiwa waitindue kabisa ile barabara na kutengeneza tuta upya na kuweka moramu.

Barabara ile kurudishia kila mwaka tope haitusaidii sana. Kuna kilio kikubwa cha wananchi wa Ludewa na upande wa Njombe Kusini kuhusu Barabara ya kutoka Itoni kwenda Manda, tunaomba sana Kamati mkiweza mtembelee maeneo hayo ili muweze na ninyi kutusaidia kuishauri Wizara namna ya kutusaidia barabara zile. Kwa vile nilikuwa na dakika kumi naomba niachie hapo Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na ninakushukuru sana Mheshimiwa Prof. Raphael Benedict Mwalyosi, kwa matumizi mazuri ya muda. Sasa mzungumzaji wetu wa mwisho si mwingine bali ni Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia. Karibu sana!

**MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Hakika nilitaka kuzungumzia pointi mbili yaani mawasiliano ya simu ya mkononi na Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenyewe umeshuhudia ulivyotembelea mbuga za wanyama za Kingupira *Eastern Selous.* Kutoka Utete ambapo kuna mnara wa *Celtel* kwenda Kingupira ni zaidi ya kilomita 80, kule tunatazamia kupokea watalii, kule tunatazamia mambo yaendelee kimaisha na wananchi simu wamenunua lakini hatupati minara kupelekwa kule.

Mimi binafsi nimeandika barua moja kwa moja kwa *Director General* lakini vilevile kwa Naibu Waziri wa Mawasiliano sijapata jawabu zuri. Sasa ukiangalia ile Rufiji na ile Kingupira kilomita 85 kupata mnara Kilimani, Nyaminywili, Mloka na hata Mhaseni huku kote tumeandika barua kuwaambia tunahitaji kwa sababu *area* hii inapitiwa na watalii wanaokwenda Selous kwani kila siku ukienda utakuta gari zimejaa barabarani wanashindwa kuwasiliana.

Suala langu nililosimamia hapa ni kumwuliza Mwenyekiti kama amewahi kutuulizia, tumepitisha Sheria ya *Universal Communication Action Service Act* 2006 maana yake mahali ambapo ni *remote rural* kama Kingupira mwekezaji apewe fedha ili aweze kujenga minara kule kwa kusaidiwa na fedha zilizoahidiwa katika Muswada huu ambao sasa hivi ni Sheria.

Naomba Mheshimiwa Waziri afanye hima Sheria hii itumike ili wawekezaji maarufu kwa mfano kule nyumbani kwetu sisi *Celtel* ndiyo maarufu na *Vodacom* kidogo na pia *Tigo* waweze kwenda katika vijiji waweke minara ili watu wetu wapate kuwasiliana na wenzao waliko lakini *most important* ni kunyanyua biashara ya utalii katika sehemu na vijiji nilivyovitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ilikuwa nizungumzie juu ya Barabara na hapa ina sehemu mbili. Ibara ya 5.32 imetajwa Barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara lakini kwa nini Kamati haikusema Ndundu kwenda Somanga ndiyo pachafu zaidi na mimi naomba Kamati iende kwa gari kutoka Dar es Salaam wapite Ndundu – Somanga waone mashimo yaliyopo pale.

Kwa hiyo, namkumbusha Mheshimiwa Waziri, naona sikumpa hongera lakini hongera nyingi sana kwa kupita *NEC* na kwenda Kamati Kuu. Ndundu – Somanga ni donda ndugu, naomba sana na ninaiomba Kamati vilevile itie mkazo, huwezi kuandika mstari mmoja Barabara ile, mstari mmoja yaani Dar es Salaam–Mtwara, haiwezekani ni lazima useme pana matatizo makubwa Ndundu–Somanga na yachukuliwe kwa uzito wake. (*Makofi*)

Sehemu ya pili ya Barabara ni maombi ambayo tuliomba Wilaya ya Rufiji ina barabara inayotoka Ikwiriri -Mkongo-Ngorongo – Nyaminywili - Mtanza- Mloka kwenda *Selous* kilomita 110. Barabara hii imeachiwa Wilaya lakini Wilaya haina ubavu wa kulipa hela hizo na tukaomba Serikali ikubali kuipa dhamana ya kutengeneza Barabara hii iwe mikononi mwa *TANROADS* Mkoa.

Sheria tuliyopitisha hapa ilikuwa na vigezo, kigezo ambacho Barabara hii imetimiza ni kwamba inaunganisha Wilaya na Makao Makuu ya Mkoa. Barabara inayotika Ikwiriri–Mkongo–Ngorongo– Mtanza – Mloka inaweza ikaenda mpaka Vikumburu – Kisarawe na ikafika Kibaha Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kigezo kilichowekwa kwenye Sheria ile, hii Barabara inakidhi, namwomba Mheshimiwa Waziri afanye hima kuinyanyua ili iwe katika daraja la Barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Mkoa yaani *TANROADS* Mkoa.

Vilevile kati ya ahadi ya Rais kuna Barabara ya Kibiti – Mkongo – Utete.

Hii inasuasua utekelezaji wake mwaka huu wa pili tunaulizwa vipi? Maskini haikuwa inatakiwa itiwe lami ni kutiwa *moram* nzuri ambayo inaweza kustahimili hekaheka za mvua za masika. Ninadhani hapa Mheshimiwa Waziri angesukuma kidogo *TANROADS* Mkoa imalize kazi ile maana hii ni ahadi ya Rais, kumuenzi Rais ni kumtimizia ahadi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nilitaka kuzungumzia Kivuko cha Utete. Bunge limeahidiwa kivuko cha Utete kitakuwa na uzito wa tani 50 lakini mpaka leo hatujaona matangazo ya zabuni au sijui itanunuliwa kama vitumbua maana yake tulikuwa tunatazamia kwamba hizi zabuni zinatangazwa ili watu katika miezi sita kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha ile *panton* iwe imekwishanunuliwa na kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na vilevile namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu na namwomba aangalie sana barabara ya Ndundu – Somanga. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nichangie, lakini katika kuchangia niwe natoa ufafanuzi au majibu kwa baadhi ya maeneo yaliyoguswa katika taarifa hii.

Nianze na moja la kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wameniletea salamu nyingi sana za pongezi kutokana na kubahatika kwangu juzi kuchaguliwa kuwa mjumbe wa *NEC* na baadaye kubahatika mara ya pili kuchaguliwa

kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi. Nawashukuru sana. Imani niliyopewa na CCM nitaitumia kwa kurejesha imani hiyo hiyo kwa Chama changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wabunge kwa kumpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kwa taarifa nzuri aliyowasilisha humu Bungeni. Ni taarifa iliyosheheni taarifa katika maeneo mengi ambayo Kamati inayashughulikia ya Wizara yetu, ina maeneo mengi ya ushauri ambayo tunauchukua, ni ushauri mzuri tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni niliamini hata Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia nilidhani tupo katika Bunge la Bajeti lakini hii ni taarifa ya utekelezaji kwa mwaka 2006. Bajeti ya Wizara yote mnaifahamu, hayo mliyosema baadhi yake yapo ndani ya bajeti ya mwaka huu na hakuna kipya ambacho tunaweza kufanya kama miujiza tutoe fedha sasa hivi kwa maeneo kama ya Mheshimiwa rafiki yangu Prof. Iddris Mtulya kwa barabara aliyoitaja hata kwa Mheshimiwa Prof Mwalyosi kwa barabara ya kutoka eneo la Mheshimiwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema kwa kifupi sana katika maeneo ambayo yamegusiwa, moja ni miradi ya *BoT*. Waheshimiwa Wabunge tunakamilisha sasa *guidelines* hizi za mwongozo ambao utatumika katika miradi ya *BoT* hasa kwa upande wa barabara na madaraja likiwepo daraja la Kigamboni na mengine kama Pangani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mto Pangani tunafikiri kuwa ni mmoja kati ya *candidates* ambazo zinaweza kufikiriwa kwa utaratibu wa *BoT*. Sisi kama Serikali tunajenga mazingira mazuri ya kuwezesha *private sector* kuweza kushirikiana na Serikali kuleta maendeleo ya nchi yetu. Hivyo hivyo kwa maziwa makuu tumeona kabisa usipoweza kutoa vivutio vizuri kwa maziwa haya, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, na Ziwa Victoria. Ni tofauti na Mwekezaji katika *Indian Ocean*, Bahari ya Hindi kama biashara haijachanganya meli inaondoka kwenye Maziwa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza lazima mtu afikirie mara tano mara kumi, kuwekeza huko ni kitu gani kinampeleka huku? Tumesubiri kwa kipindi kirefu hatuoni wawekezaji wapya katika maeneo hayo na Serikali hatuwezi kila siku hapa Bungeni tunasema tunakaribisha wawekezaji, kwanza kabisa ni lazima Serikali iangalie kuweka *intervention* zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Wizara hili tumeliona na tutaishauri Serikali nini kifanyike pale ambapo tumejaribu njia zote za kukaribisha wawekezaji lakini *nothing is happening.* Mheshimiwa Mwandoro nakuhakikishia kabisa kwamba barabara ya kutoka Tanga mpaka Horohoro ni sehemu ya mpango wa *MCC* na katika hili nilisema wakati wa bajeti kwamba bahati nzuri tatizo ambalo lilianza kujitokeza na wenzetu wa Kenya tumeliza maana hii ilikuwa tunai-*promote* kwa pamoja tupate pesa za *ADB* wao waichukue kutoka Lungalunga, Mombasa mpaka Malindi.

Jibu lililopatikana ni tutazipata fedha hizo hizo, sisi tutajenga barabara ya Tanga –Horohoro kutumia pesa ya *MCC* lakini tunatumia fedha za *ADB.* Kutoka Tanga

tunakuja Pangani, Sadani na Bagamoyo tena *a longer network*, Sadani kwa sababu tunajua ni eneo zuri sana kwa utalii kwa hiyo, kazi inakuja hiyo. Bandari ya Lindi jamani chanzo cha tatizo ni kujaa mchanga katika eneo la maegesho ya meli, vilevile kwa Bandari ya Itungi, Bandari ya Kigoma, Mwanza, Mbambabay, yote haya matatizo tunayo. Kwa upande wa ziwa Victoria na ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria nchi tatu ambazo tunamiliki kwa pamoja maji ya ziwa hili, Tanzania, Kenya na Uganda, tumekubaliana tuangalie uwezekano wa kununua *Dragger* yetu sisi kwa pamoja, *dragger* hiyo itakuwa inafanya kazi katika ziwa Victoria pale ambapo mchanga umejaa inapelekwa inafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tumeunganisha na mradi ambao tunashirikiana na Serikali ya Ufaransa kwa suala zima la utafutaji na uokoaji. Pale ambapo tunapata matatizo ya mitumbwi au meli kuzama inaendelea vizuri sana kwa upande wa ziwa Victoria. Kwa upande wa ziwa Tanganyika Serikali ya Ubelgiji tunashirikiana nayo kwa kuchimbua tena mchanga katika bandari zetu na lengo ni hilohilo ukichimbua ndiyo kina cha maji kinakuwa kirefu, kwa hiyo, meli kubwa zinaweza zikafika pale bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa upande wa Shirika la Posta, nakubaliana na ushauri uliotolewa na ndicho tulichokifanya. Mengine hatuyasemi tu lakini ndiyo hiyo nadhani tusipoyasema watu wanadhani kwamba hayafanyiki na ndiyo maana lazima niseme, mzigo wa madeni unaolielemea Shirika la Posta sasa umepatiwa ufumbuzi, Serikali imechukua madeni ya Shirika la Posta ya kiasi cha shilingi bilioni 20.4.

Serikali imechukua deni la Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki ya dola za Kimarekani 670,871/-. Serikali imelifutia Shirika la Posta madeni ya shilingi bilioni 5.2 na pia imelifutia deni la Benki ya Dunia ya dola za Kimarekani 412,085/- na katika mwaka ujao wa fedha Wizara ya Fedha itatenga kwenye bajeti ya Serikali kiasi cha shilingi billion 8.2 kwa ajili ya kulipa pensheni ya wafanyakazi waliotoka katika shirika lililokuwa la Afrika Mashariki la Posta na Simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo tumeyafanya na lengo ni kusafisha mizania ya shirika hili liweze sasa kwenda kukopa kwani Serikali haitaendelea kulipatia fedha shirika hili, wana ubia pamoja na Benki ya Posta wanaendelea vizuri lakini tumewaambia kuna *cost center* ambazo tunajua kabisa wakizishughulikia shirika hili litaanza kutengeneza faida. Na wao katika mkakati wao wanaona kabisa lazima wakumbatie teknolojia ya kisasa na hili wanalo katika mpango wao, lakini mzigo uliokuwa unawasumbua sasa haupo, Mheshimiwa Mwenyekiti watafute mchawi mwingine.

Narudia tena, mkakati wa Serikali yetu katika kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami una malengo makuu mawili. La kwanza, ni kuunganisha nchi yetu na nchi jirani zinazotuzunguka kwa barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami na tunafanya vizuri, kwa upande wa Kenya tumefanya vizuri sana, wote mnajua tunahangaikia sasa hivi barabara ya kutoka Arusha, Namanga na upande wa pili ni Namanga mpaka *Usa River.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelisemea hii ya Tanga - Horohoro, dhana ni hiyohiyo. Taveta kutoka Himo tunapandisha Tarakea, lengo ni hilo hilo. Tumekamilisha

upande wa Tarime-Sirari. Kwa upande wa Uganda tumekamilisha mpaka Mtukula na upande wa Burundi na Rwanda, Nyakasanza, Rusumo na kwenda pia upande wa Burundi Kodoro. Kwa upande wa Kigoma kwenda nchi jirani ya Burundi ndiyo tunasema kutoka Mwandiga –Mwanyovu.

Haya tunayafanya kwa Kusini tuna Tunduma tumeshaifanya wote tunajua, lakini tuna lengo pia la kutoka Mpemba kwenda Isongele katika Wilaya ya Ileje ambayo inaunganisha na nchi ya Malawi.

Tumemsikia Mheshimiwa Dr. Mwakyemba asubuhi, tulipokuwa kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tumepitia barabara hiyo kutoka Kikusya – Ipinda – Matema na yenyewe inakufikisha Matema *Beach.* Mnaendelea maji ya Tanzania kwenye ziwa Nyasa unaelekea upande wa Mbamba Bay. Sasa yote haya tumedharia kabisa kuunganisha nchi yetu. Lakini pia tunaangalia uwezo huo kutoka Sumbawanga – Matai unakwenda Kisesya, Zambia, kutoka Matai unakwenda Katanga yote hii ni connectivity na nchi jirani.

Lengo la pili ndugu zangu Tunduma, Ndundu haiunganishwi na nchi yoyote. Ungeniambia sehemu ya Mtambaswala barabara ya kutoka Mangaka kupitia Nanyumbu unakwenda mpaka Mtambaswala kuunganisha na nchi jirani ya Msumbiji. Kwa hiyo, tunaendelea vizuri kwenye eneo hili.

Lakini la pili ni hili la kuunganisha mikoa yetu, makao makuu ya mikoa yetu barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami. Hili tunalifanya vizuri. Hata hivyo, kuna maeneo ambayo tumeamua ambayo ripoti inasema maeneo ya mikoa ya pembezoni na ndiyo maana unaona tunahangaikia sana Mikoa ya Lindi na Mtwara. Barabara hizo zinajengwa sasa hivi na madaraja yale ambayo umepita juzi ukiondoa sehemu ya mtani wangu anayosemea ya Ndundu – Somanga kilomita 60 hizo na zenyewe zimo katika mpango huo. Sasa barabara za lami jamani hukurupuki tu. Tuvumiliane. Lakini inakwenda vizuri sehemu hiyo.

Eneo lingine ni hili la kutoka Mkoa wa Ruvuma na Mtwara. Kwa hiyo, ndio maana tunahangaika sana na ukanda huo na ndiyo maana tunaishukuru sana Serikali ya Marekani katika maeneo ambayo imekubali kutusaidia. Serikali ya Japan pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika, tunashukuru sana, maana ndiyo uhakika huo. Sasa hivi tutabaki na sehemu ya kutoka Tunduru kwenda mpaka Namtumbo na kutoka Mbinga kwenda Mbambabay maeneo haya tumesema hata kama hatutapata mtu wa kutusaidia tutajipiga mfukoni mwetu tuweze kujenga kwa nguvu yetu. Lakini tunakwenda vizuri. Lakini kwa upande wa Mkoa mwingine ni Mkoa wa Rukwa. Tunaishukuru sana Serikali ya Marekani pia *MCC* kuchukua ile sehemu ya kutoka Tunduma mkutano mpaka Sumbawanga. Lakini lazima tutoke Sumbawanga tuunganishe Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Kigoma. Kazi inayoendelea sasa hivi mnaifahamu nilieleza wakati wa Bajeti ya usanifu wa kina kutoka Sumbawanga – Mpanda tuje mpaka Uvinza, tunakwenda vizuri ndugu zangu.

Mkoa mwingine ni Mkoa wa Kigoma, lazima tujenge barabara hiyo, tuunganishe na Mikoa jirani ya Kagera na Tabora. Yote haya yako katika mpango ambao upo. Ndugu zangu barabara hizi tunazijenga kwa gharama kubwa sana, shilingi milioni 800 kwa kilomita moja. Mimi nashawishika sana kuchukua mawazo yenu kwamba kwa nini tupoteza fedha kila mwaka. Mimi nawashauri nendeni mkajaribu kwenye barabara za Halmashauri muone maana ya kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami. Sisi tunasema kwa sababu hii ambayo tumeijenga kwa gharama kubwa kidogo watu watatushangaa, tuiachie tu iharibike eti kwa sababu hela yote sasa tunahamisha kwenda kujenga barabara za vijijini.

Hii ni ndiyo *life line* ya uchumi wa nchi yetu ambayo tunahangaika kuitengeneza. Tuifungue nchi yetu yote ili tuweze kuhakikisha kwamba angalau kutoka kwenye sehemu moja kufika kwenye *centre* ya barabara kuu bidhaa hizi zitafika kwa haraka kwenda masoko kwa haraka na kwa gharama nafuu. Nadhani nimeyagusa haya ambayo alisema Bandari mpya ya Tanga. Ndugu zangu mawazo yetu ni hayo hayo, sisi tumekuwa tunaisubiri sana Serikali ya Uganda, mawazo ndiyo hayo sisi wakitupatia *commitment* kwamba wataitumia *full time* reli ya kutoka Arusha, Tanga mpaka Arusha, Musoma, tunachukua *wagon fery* mpaka *Port Bell* sawa kabisa.

Lakini kama humpati wa namna hiyo, lazima wewe mwenyewe uihangaikie kama ya kwako na ndiyo maana nasikitishwa na hawa wana mazingira kuhusiana na mradi huu wa *lake Natron*. Watanzania tufike mahali tuonekane kabisa kwamba *we are in-charge* ya uongozi na hatma ya nchi yetu. Njia moja ya kuweza kuijenga reli hii ni kuwa na mradi kama huo ambao unaku-*guarantee* mzigo. Sasa *environment impact assessment* imefanyika. Sasa kama wao wanadhani kwamba yale wanayotaka kuyafanya na kusema wao kwamba Serikali ya Tanzania ndiyo lazima iyakubali, tunasema hapa. Lakini sisi hatuendi kichwa kichwa na ndiyo tulisema fanyeni tathmini ya uhakika kwenye eneo hilo la mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumekusudia kabisa na tumedhamiria kabisa kuimarisha reli ya kutoka Tanga, Arusha, Minjingu, Musoma kwa sababu hiyo hiyo na tulieleza. Kuna swali najua litakuja kuulizia reli hiyo, kama halikujibiwa labda nachanganya lakini najua kama tutavyofanya kwa reli ya kati na reli hiyo tunaimarisha kwa ukarabati kwa maana ya kuongeza uzito wa reli. Kwa hiyo, ndugu zangu tunakuja vizuri na mandhari ya Tanga tatizo lake wote tunalijua, *is not a deep port*, meli kubwa haziwezi kufika pale kuegesha kwenye gati.

Sasa biashara ya leo huwezi ukaenda na namna hiyo, na ndiyo maana eneo jipya la mwambani ambalo limefanyiwa usanifu tunali-*promote* sana sasa hivi kwa wawekezaji wenye uwezo wa ndani na wa nje. Vilevile kwa bandari ya Dar es Salaam kwa sababu eneo la *container* limeshafikia *all most* kama jana, mimi sijui siku hizi nadhani mambo makubwa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa Bandari ya Mtwara tunajua umaana wake. Lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Abdulkarim Shah kuhusiana na sifa alizotumwagia kwa haya tunayofanya kwa Mafia kwa sababu ndiyo *commitment* yetu na

tutaangalia uwezekano kwa upande wa Ukerewe. Sasa ni tatizo kweli kweli katika maeneo kama haya kama huna *equipment* angalau itakuwa pale, mkandarasi atakuja ataikuta pale anaikodisha anafanya kazi. Lakini iwe ni ya *TANROADS* ambayo itasimamia na meneja wa *TANROAD* wa Mkoa husika.

Suala la kupandisha daraja ndugu zangu barabara zilizoombwa zina utaratibu. Ndugu zangu Mheshimiwa Paschal Degera na wengine mliolisemea hili ni juzi tu wiki mbili zilizopita Mheshimiwa Rais ndiyo ameweka *assent* yake idhini ya kukubali sheria hiyo. Sasa tupeni na sisi nafasi tutafakari haya maombi kwa vigezo ambavyo vimo ndani ya sheria kama maombi yenu yanafuzu barabara hizi zitapanda daraja. Lakini kupanda daraja haimaanishi kwamba sasa zitaimarika na kuboreka kwa sababu *kit* ni ile ile.

Tunashukuru mmetuidhinishia fedha tuone utendaji wetu, lakini fedha hizo ni za matengenezo na siyo kwa kujenga barabara mpya. Tulipenda tuziimarishe tuziboreshe. Nijibu hoja ya Mheshimiwa Ndesamburo, Watanzania ni kweli neno la *maintenance* huwa linatupita kidogo lakini angalau kwa upande wa barabara kwa *network* ya barabara kuu na barabara za Mkoa tunahakikisha utumishi uliotukuka. Tunataka tuone tofauti kwamba hizi barabara zitunzwe maana tumezijenga kwa gharama kubwa kweli jamani. Sasa nikizungumzia uwanja wa ndege wa Mwanza, ndugu zangu shabaha ya Serikali ni hiyo hiyo, tumeanza na *phase one* hii lakini lengo ni kukifanya kiwanja hicho kifikie kiwango cha cha Kimataifa. Tumeanza hatua hiyo na tunataka nafasi hii tuitoe sana kwa *private sector* kwa sababu tunajua *private sector* ikishirikiana na Serikali inaweza ikafanya kazi hiyo kwa haraka zaidi kuliko kama sisi tutaifanya kazi hiyo. Tunawashukuru *BADEA* kwa kuonyesha nia ya kushirikiana na sisi na ndio itasaidia hata kuteremsha kiwango cha *tariff* na kuwezesha kiwanja hicho kiweze kujilipa mapema.

Mheshimiwa Madeje, nakuelewa na kiwanja cha Msalato na fidia kwa Dar es Salaam na Msalato tunayokwenda nayo. Barabara ya Arusha, Babati, Dodoma, Iringa haipewi kipaumbele, hapana ndugu zangu, leo asubuhi tumejibu swali, mtuelewe tumedhamiria kweli kweli tukamilishe hatua zile ambazo ni muhimu ambao ni usanifu wa kina ili ujue gharama ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami na baadaye sasa uhangaike kutafuta fedha.

Iringa – Dodoma tuna *commitment* kabisa ya *ADB* hili nasema wazi kabisa kwa sababu nimekutana na uongozi wa juu kwa sababu ilikuwa ni *commitment* yao tangu zamani. Tunayohangaikia ambayo haina *funding* ya uhakika ni kutoka Dodoma – Babati – Minjingu. Lakini barabara ya kutoka Singida – Quatesh – Babati mnajua tuna fedha *ADB* na tunakamilisha *process* ya mwisho ya kumpata mkandarasi.

Reli ya Mpanda – Kaliwa – Singida – Manyoni inaimarishwa kwa uzito wa ratili 80 kwa yadi. Nimeelezea mambo ya barabara za upande wa Kilwa – Rukwa – Kigoma na mengine hayo. Maeneo mengine yaliyoguswa kwenye taarifa hii Linganga na Mchuchuma, hii tunaiona kama ni *integrated project*, lazima uangalie pia miundombinu ya barabara na reli, huo ndiyo mtazamo wa Serikali katika masuala hayo.

Kulikuwa na fedha za dharura, ndugu zangu nakubaliana na ninyi, si nia ya Serikali kuwakata miguu hawa makandarasi wadogo ambao walijitolea kufanya kazi hiyo. Endeleeni kutusaidia, tuna tatizo hilo, mimi sina hela kwenye bajeti yangu ya mwaka huu, wale ambao walisema watalipa, watulipe, tumefanyakazi hiyo. Mimi huwa mnanielewa.

Ndugu zangu nimalizie kwa kuishukuru sana Kamati kwa taarifa yake nzuri. Kuna maeneo mengine ambayo kwa sababu ya muda sikupata nafasi ya kuyasema. Lakini kwa kivuko cha Pangani nataka nimhakikishie tu ndugu yangu Mheshimiwa Rished *process* ya kivuko kipya kuandaa zabuni ndiyo inakamilika sasa, vilevile cha Utete na cha Kinesi. Jamani tunafanya kazi, mkituona wengine vichwa vinaanza kuharibika kwa sababu ya matatizo. Nchi hii lazima tuipeleke mbele jamani. Katika kufanya hivyo lazima tuchachalike. Mkongo wa Kitaifa hili ndiyo eneo muhimu katika kuikwamua nchi yetu na tunasema ni la kufa na kupona.

Tunakwenda vizuri sana na Serikali ya China katika kutupatia mkopo wa masharti nafuu ili tuweze kufanya kazi hii katika Mkongo wa ndani lakini na huu sasa wa baharini mazungumzo kati ya nchi zetu hizi 23 yamekwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Afrika Kusini juzi imesema tukikamilisha yale ambayo ni ya msingi kwa kila nchi, kwetu tutakuja hapa Bungeni kuomba ridhaa ya kuridhia Itafaki ya Kigali sehemu ya fedha ambayo haitapatikana kutokana na makampuni ambayo yatashiriki. Serikali ya Kusini imeahidi kukamilisha kulipa tofauti.

Tunataka Mkongo huo uwe umekamilika *by* 2010 kuwahi mchezo wa dunia wa *World Cup*. Lakini kwetu hilo ndilo tunaunganisha na huu wa ndani ambao lengo letu ni kupeleka mfumo huu kwa kuanzia ngazi za Wilaya zetu zote. Hatutaki sehemu ya Tanzania ijisikie kwamba imesahaulika katika suala zima la teknolojia. Hayo tunayafanya ndugu zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimalizie hapo. Sasa kwa kusema kama kuna mengine ambayo sikuyasema, maeneo ya viwanja tumetafuta maeneo Dar es Salaam, tunajua ni ndogo sana sasa hivi, tutaendelea kuitumia hadi hapo tutakapokamilisha kujenga kiwanja kipya cha Kimataifa. Tumepata eneo moja Bagamoyo, kubwa tu, eneo lingine tumepata Mkuranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kukushukuru tena kwa kunipatia fursa hii kuweza kufafanua. Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Andrew Chenge. Natumaini na suala la Uwanja wa Ndege wa Dodoma litakumbukwa.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati kwa kuwasilisha taarifa nzuri ya Kamati yake kwa mwaka uliopita. Nawapongeza Wajumbe wa Kamati kwa kutembelea miradi mbalimbali hasa mradi wa ujenzi wa kiwanja cha Ndege cha Songwe Mbeya. Wananchi wana shauku kubwa kuona uwanja ule unakamilika haraka.

Moja, kuhusu usafiri wa majini napenda kuishauri Kamati kuwa katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Wajumbe wa Kamati wajitahidi kupanga ziara ya kujionea miradi inayotekelezwa katika Ziwa Nyasa hasa ujenzi wa magati.

Usafiri katika Ziwa Nyasa ni mgumu sana. Meli au boti zinazofanya kazi katika Ziwa lile ni mbovu, ni za siku nyingi, huharibika mara kwa mara. Meli hizo zinapoharibika, utengenezaji wake ni nchini Malawi kwa nini nchini kwetu tusiwe na karakana ya kutengeneza meli zetu? Je, ikitokea uhusiano wetu na nchi hiyo jirani ukawa si mzuri, tutafanya nini?

Pili, kwa kuwa meli zetu si za kuaminika, Kamati iishauri Serikali yetu ya Tanzania kuzungumza na Serikali ya Malawi ili meli zao kubwa ziweze kutumia bandari zetu ili kuwasaidia wasafiri hasa wakati wa dhoruba kali. Wazo hili likikubalika, itabidi Serikali yetu iboreshe mazingira ya Bandari zetu za Itungi, Makonale, Lupingu, Lunalu, Liuli na Mbamba Bay yawe mazuri.

Tatu, ujenzi wa barabara za lami. Naomba Kamati iishauri Serikali kuwa makini wakati wa kuteua Makandarasi wazuri wanaojenga barabara imara. Mfano mzuri wa Mkandarasi mzuri ni yule aliyejenga barabara ya Uyole –Ibanda mpaka kati ya Malawi. Barabara ile imedumu mpaka sasa miaka kumi na tano bila kubomoka tofauti na zile zilizojengwa baadaye kwa mfano, barabara ya Mbeya – Tunduma ambayo ina miaka 6 tu, tayari ina mashimo makubwa. Ni bora kuzingatia ubora wa barabara kuliko kuangalia wingi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ushauri huo mfupi, naunga mkono hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kama ilivyotolewa.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa Mkutano wake Mkuu wa mwaka 2007 uliopata mafanikio makubwa. Napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa ushindi mkubwa sana kuwa Mwenyekiti wa Taifa. Hali kadhalika, ningependa kuwapongeza viongozi waliopata fursa ya kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Wakuu wa Idara za Sekretarieti,Wajumbe wa Kamati Kuu na Wajumbe wote wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM. Ninawatakia kheri na mafanikio mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wake wa Kamati ya Miundombinu kwa kazi nzuri na taarifa yao

nzuri. Naunga mkono taarifa ya Kamati kwa asilimia 100. Hata hivyo, ninapenda kugusia maeneo ambayo hayakutajwa au hayako wazi. La kwanza kabisa, linahusu barabara ya Tanga-Handeni. Barabara ya Tanga-Horohoro ni barabara pekee inayounganisha nchi mbili za Tanzania na Kenya ambayo imekuwa ikitolewa ahadi ya kuwekewa lami kwa miaka mingi sana lakini dalili thabiti bado haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile barabara ya Tanga-Pangani hadi Sadani haijaonyesha dalili ya kuwekewa lami kwa miaka ya hivi karibuni. Katika mpango mzima wa *Northern Development Corridor* pamekuwepo na mapendekezo ya kujenga na kuendeleza bandari ndogo kama vile za Moa, Kwale na Pangani. Upo umuhimu wa kulipa mkazo suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu kwa maana ya majengo na vitendea kazi katika mpaka wa Horohoro inastahili kuboreshwa. Majengo ya Makao Makuu mapya ya Wilaya ya Mkinga, yamekamilika lakini ufunguzi na matumizi yake yatategemea sana kupata umeme, maji na samani mapema iwezekanavyo. Hili ni suala ambalo Kamati ya Miundombinu inaweza kuliwekea msukumo kwa Wizara ya Miundombinu kupitia *Tanzania Bulding Agency.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono taarifa hii ya Kamati kwa asilimia mia moja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pole kwa wote waliofiwa na kwa wagonjwa. Pia napenda kuwapongeza wale wote waliopata mafanikio mbalimbali katika kipindi cha mwezi Agosti mpaka Novemba, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa majini, Mkoa wa Kigoma una Ziwa Tanganyika na katika Ziwa hilo tulikuwa na meli mbili, *M.V.* Mwongozo na *M.V.* Liemba. Meli ya Mwongozo ndio inayojikongoja kufanya kazi lakini Liemba sasa imechoka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, meli ya *Mv. Mwongozo* inaelemewa na kazi nayo haijafanyiwa ukarabati wa kutosha kwani inatembea kwa kusuasua. Ziwa Tanganyika likiimarishiwa vyombo vyake usafiri masuala ya usafiri na uchumi kati ya nchi yetu na nchi jirani za Zambia, *DRC* na Burundi yatakuwa rahisi. Mwisho, nashauri Serikali kukarabati Bandari ya Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa reli. Ni vema sasa Reli ya Kati imerudisha utaratibu wa safari zake kutoka Kigoma, Shinyanga, Mwanza hadi Dar es Salaam. Wasiwasi wangu ni kwenye uimara wa treni yetu iliyochoka na vilevile reli hasa kutoka Dodoma Morogoro eneo la Kilosa reli ni chakavu sana na ajali nyingi zimetokea pale. Serikali iwe makini ajali isitokee tena.

Suala la usafirishaji wa mizigo linakuwa na urasimu sana kwani ni kawaida mzigo kukosha behewa kwa zaidi ya miezi miwili. Hii inasababishwa na *policy* mpya ya kuruhusu wafanyabiashara wenye uwezo wa kubeba mzigo wa mabehewa 20 ndio wanaopata nafasi. Nashauri uwekwe utaratibu angalau mara mbili kwa mwezi yapangwe mabehewa ya wafanyabiashara wadogo wadogo wenye uwezo mdogo wa behewa moja hadi matano wapewe utaratibu wa kuwasafirisha mizigo yao kwa pamoja ili wafikie lengo lao la behewa 20 au zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi waliopunguzwa kazi walilalamika mafao kidogo na wengi waligoma mwezi Septemba. Serikali itueleze ni kwa nini wafanyakazi hao waliopunguzwa walipewa mafao kidogo yasiyolingana na miaka waliyotumikia shirika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Makampuni ya Simu, nashauri Serikali iongee na Makampuni ya Simu ya *Celtel, Vodacom* na *Tigo* ili waweke mitambo yao Kigoma vijijini kwani sasa wananchi hasa waishio mpakani mwa Kigoma, Kagunga, Mwamgongo na vijiji vingine wanatumia mtambo wa simu wa *Onatel* wa Burundi, hivyo, itasaidia katika masuala ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wakandarasi wazalendo, uwepo utaratibu wa kuwawezesha Wakandarasi wadogo wadogo hasa kwa kuwakopesha pembejeo na mitambo ya kazi zao ili wazifanye kwa *standard* inayotakiwa. Wizara iige mfano wa Wizara ya Kilimo inavyojitahidi kukopesha wakulima pembejeo za kilimo. Nilishuhudia Tunduru, Mkandarasi anatumia jembe la mkono na koleo kutengeneza barabara. Hata kama amesoma ni *Engineer* mzuri lakini kwa uduni huo hatafanya kazi ya kuonekana ubora wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mchango wangu uzingatiwe.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kutoa rambirambi kuhusiana na kifo cha marehemu Salome Mbatia, Mbunge mwenzetu na aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Pia nichukue nafasi hii kukipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kufanya Mkutano wake Mkuu na kupata viongozi wapya kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii tena kumshukuru Mheshimiwa Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kwa kazi nzuri ya kuishauri Wizara juu ya masuala mbalimbali yanayohusu miundombinu ya nchi yetu. Naipongeza Kamati kwa kuandaa taarifa nzuri iliyoainisha maeneo yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuboresha taarifa ya Kamati ikiwa ni katika utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha 2007/2008. Nashukuru kwa kazi nzuri ya kurejesha Shirika letu la Ndege *(ATCL)* mikononi mwetu. Pamoja na hayo, Kamati ilishauri Shirika liende na wakati kwa kuwa na ndege za kisasa na huduma zenye viwango ili kuvutia na kuingia katika hali ya ushindani wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilishauri Wizara juu ya mkazo kwa Wakandarasi wale wanaoshindwa kutekeleza muda waliowekewa katika utengenezaji wa barabara na hata majengo. Udhibiti wa viwango vya matengenezo ya barabara, madaraja, majengo na kadhalika utiliwe mkazo ikiwezekana adhabu zichukuliwe kwa wale wanaoshindwa kutekeleza matakwa ya mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ishawishi mashirika mengine ya ndege kama vile *ATCL*, *Precision Air* na kadhalika kuanzisha safari za ndege kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na Mwanza hadi Dodoma – Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati ishauriane na *TRC* juu ya kuimarisha usafiri wa treni wa Singida hadi Dodoma ikiwezekana iongoze mabehewa kutoka mawili ya sasa hadi manne kwa abiria na moja kwa behewa la mizigo.

Aidha, Kamati iyashauri Mashirika ya Simu za Mikononi yaeneze mtandao wa simu sehemu za Vijijini mfano mzuri Vijiji vya Iramba Magharibi vile vya Tulya, Doromoni, Mizilango, Kidaru na Ntwike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Kamati na naunga mkono taarifa hii.

**MHE. MOHAMMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia tatizo la Bandari ya Lindi. Serikali ilitoa ahadi kuwa inafanya uchunguzi ili kubaini chanzo cha tatizo la kujaa mchango katika eneo la maegesho ya meli. Hadi hivi sasa, tatizo la mchanga katika Bandari ya Lindi lipo vilevile. Ninapenda kujua Serikali ina mpango gani wa kufufua bandari ya Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ujenzi wa barabara ya Mbwemkuru-Mingoyo, kampuni ya Kharafi ilijenga majengo ya kudumu kwa ajili ya kambi ya wafanyakzi katika eneo la Mitwero - Lindi Mjini. Aidha, wamejenga nyumba za wafanyakazi wa daraja la juu katika eneo la Rasbura- Lindi Mjini.

Ningependa kupata uhakika, nyumba hizo zitamilikiwa na nani baada ya miradi kukamilika. Napenda kutoa pendekezo kwa Wizara ya Miundombinu kwamba nyumba hizo iikabidhi Halmashauri ya Mji wa Lindi ili ziwe shule ya sekondari. Ombi hili tulilitoa siku ya kusainiwa Mkataba wa ujenzi huo hapa Dodoma.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na wenzangu waliotoa salamu za rambirambi kwa kifo cha Mheshimiwa Mbatia (Mb.) na wale waliopata ajali, Mwenyezi Mungu awape subira na nafuu ya haraka. Napenda kuipongeza Kamati kwa taarifa nzuri waliyowasilisha hivi punde. Kwa masikitiko makubwa, taarifa haikutoa maoni yoyote kuhusu reli ya Mpanda na Singida ili ziweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi kwa kuimarisha reli, mabehewa na injini. Naomba mchakato wa kukodisha huduma za reli katika njia hizi, upewe umuhimu unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika nasikitika sana kazi iliyopo ya kuunganisha Mkoa wa Rukwa na mengine ni ndogo sana. Nimepata kuambiwa kuwa ifikapo 2010 kwa mujibu wa Ilani ya CCM, barabara zote zinazounganisha Mikoa zitajengwa kwa lami, pengine isiwe hivyo hata 2015, basi barabara inayounganisha Mpanda – Rukwa na Tabora ipewe umuhimu unaostahili halikadhalika Rukwa na Kigoma ili ziweze kupitika kwa kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si Rukwa pekee ambayo haina barabara za uhakika Mkoa wa Kigoma kadhalika haufikiki katika kipindi chote cha mwaka. Napenda kuiomba Wizara katika mipango yake mizuri, kuifungua Mikoa ya Rukwa na Kigoma. Nakushukuru sana.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza sana Wizara ya Miundombinu pamoja na Kamati ya Bunge ya sekta hiyo.

Kazi ni nzuri sana na nina imani kuwa kwa kazi hii baada ya miaka mitano au kumi nchi yetu yote na nchi jirani kutakuwa na mtandao mzuri sana wa barabara na miundombinu mingine na hivyo kuchochea maendeleo au kukua kwa uchumi kwa kasi sana.

Aidha, naipongeza sana Wizara hatimaye kwa kutimiza ahadi yake ya kutengeneza kwa kiwango cha lami baraba ya kutoka Mbeya – Chunya – Makongorosi. Awamu ya kwanza ya kilomita 36 imeanza na wananchi wa Chunya wana matumaini makubwa sana.

Pia napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwa mkakati wa kuimalizia barabara hiyo aliyoitangaza mbele ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wananchi wa Chunya hapo tarehe 17 Oktoba, 2007, akiwa kwenye msafara wa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliwaambia wananchi kuwa mwakani Wizara itagawa barabara iliyobaki kwa makandarasi wawili yaani mmoja toka Lwanjilo hadi Chunya mjini na wa pili toka Chunya hadi Makongorosi. Hivyo basi, naomba wakala wa barabara kulichangamkia hili na kutangaza tenda ili kuiwezesha Wizara kuwa na tarakimu za kuingiza kwenye bajeti ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuipongeza Kamati pamoja na Wizara kwa kazi nzuri na naunga mkono hoja.

**MHE. DR. SAMSON MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono kwa asilimia mia moja. Pili, napenda kuchangia hoja ya barabara za mkoa wa Lindi hususan Wilaya ya Kilwa, Jimbo la Kilwa Kaskazini. Barabara ya Tingi – Kipatimu ambayo ipo chini ya *TANROADS*, ina malalamiko kadhaa ambayo nataka yaainishwe.

Kwanza, barabara ilikubaliwa kwamba watu watakaovunjiwa nyumba zao na mali zao zingine wapewe fidia. Nashukuru wachache wamepewa lakini wengi wao hawajapatiwa fidia. Hivyo naomba wapewe japo kifuta jasho kwani mwaka 1974 wakati wa operesheni Vijiji watu walihamishwa kusogea karibu na barabara.

Sasa cha ajabu kwa nini hawalipwi? Pili, barabara hiyo ilikuwa chini ya wamisionari na sasa ipo chini ya mkoa kwa nini wasipewe kifuta jasho? Wakati wa operesheni vijiji barabara ilikuwa na hadhi ya wilaya na sasa ina hadhi ya mkoa.

Hivyo *TANROADS* imewekwa *beackons*, wananchi hao ni sababu ya kutopewa haki zao au taa alama za *beackons* ziondolewe maeneo yao ili wananchi hao waweze kuendeleza maeneo yao ambayo yapo karibu na barabara.

Barabara ya Nangurukuru-Zinga hasa maeneo ya Mbwindi kwa kweli hali sio nzuri hasa wakati wa masika. Hivyo naomba barabara zitengenezwe kwani mazao ya wananchi yanashindwa kusombwa na wananchi wenyewe wanashindwa kufika makao makuu ya wilaya ya Kilwa Masoko. Barabara ya kutoka Kipatimu Ndundu ni fupi sana je, Serikali ina mpango gani wa kuiangalia barabara hiyo?

**MHE. ATHUMAN S. JANGUO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Kamati yako kwa kazi nzuri mnayoifanya na kwa taarifa nzuri iliyogusa maeneo yote muhimu ya shughuli zenu. Pamoja na hayo nina maoni yafuatayo ambayo Serikali haina budi iyafanyie kazi:-

1. **Kwa Kamati** - ingawa kwenye maoni na ushauri mmeeleza yote yanayohitaji kushughulikiwa, ingekuwa bora zaidi katika sehemu ya taarifa ya miradi mliyoitembelea mngeeleza kwa muhtasari mliyoyaona hasa matatizo, mafanikio na matarajio.

2. Nakubaliana na mapendekezo yenu yote hasa yafuatayo:-

**(**a) Kamati yenye *portifolio* ya Wizara ishughulikie taarifa za utendaji sawa, lakini kwa masuala ya kitaalamu, Kamati husika zishirikshwe.

(b) Uenyekiti wa wakala (*agencies*), nashauri kuwa kwa kuwa Makatibu Wakuu wana shughuli nyingi, wasiruhusiwe kabisa na kazi ambayo ni ya vikao tu.

(c) Gharama za kampuni za simu za mikononi ni kubwa. Wakizishusha mapato yao yataongezeka, gharama zao zitashuka na sisi wateja tutanufaika.

(d) Serikali ichukue hatua za kiuinusuru posta. Sawa, kama Serikali inabeba madeni ya mashirika kuyafanya yauzike, kwa nini isifanye hivyo ili kuwapatia wananchi huduma bora?

(e) Ufufuaji wa mradi wa Reli ya Tanga hadi Musoma, Serikali haina budi iuchukue ushauri wa Kamati kwa makini tena kwa haraka kwa sababu tukichelewa biashara itaendelea kuhamia Mombasa. Kwanza, bandari ya Tanga ina fursa *(opportunities)* zifuatazo:-

(i). Ipo karibu na Ziwa Victoria na nchi za jirani kuliko bandari yoyote Barani Afrika.

(ii). Uganda ipo tayari kushiriki katika utekelezaji wa mradi wa reli hiyo.

(iii). Mradi huu unaweza kuvutia uwekezaji wa kimataifa. Kwa mfano, barani Afrika, *NEPAD* inashabikia sana miradi inayogusa nchi zaidi ya moja. Benki ya Maendeleo ya Afrika na nyingine pia zinaweza kushawishika .

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza tena na ninaunga mkono.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi hii.

Awali ya yote naomba uniruhusu kwa niaba ya wanawake wa Kilimanjaro kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya marehemu Mbunge mwenzetu Salome Joseph Mbatia aliyepata ajali 24 Oktoba, 2007 na kupoteza maisha papo hapo. Ninawapa pole pia Wabunge wengine waliopata misukosuko mingine.

Pili, naipongeza CCM Chama Tawala kwa Mkutano Mkuu uliofana sana huko Kizota hivi karibuni. Naomba pia kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Miundombinu na Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naiomba sasa Kamati inifafanulie mambo machache yafuatayo:-

(1)**. Ukosefu wa fedha** - Hivi karibuni tulielezwa rasmi kuwa kila Kamati itapatiwa bajeti yake na isimamiwe na Kamati yenyewe; je, Kamati hii haikupewa fedha au hazikutosha? Pendekezo langu ni kuwa idadi ya wajumbe wa Kamati ipunguzwe kutoka 24 hadi 15 ili fedha wanazopewa ziwatoshe.

(2**. Kufufua *ATCL*** - Kwa vile Twiga amesharejea kwenye mkia wa Ndege, tunaomba jambo hilo lifanyike haraka.

(3). **Kufufua/Kujenga Viwanja vya Moshi na Kilimanjaro** - Naomba Kamati ichukue takwimu za ndege zinazotua Arusha na itambue umuhimu wa kujenga kiwanja cha Arusha na pia cha Moshi ili kuboresha usafiri wa Anga.

(4). Naomba pia nizungumzie suala la simu za mkononi, katika Nchi Zilizoendelea *handsets* za aina zote zina uhusiano na *credits* yaani *handsets* zinakopeshwa/au zinauzwa kwa bei ndogo lakini mtumiaji analipia kadri anavyoongeza *credits* kwenye simu yake. Vipi huku Tanzania zinauzwa kwa bei ya juu sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono asilimia mia moja, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita mtoa hoja, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Mohamed Missanga. Mheshimiwa Missanga karibu!

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukamilisha hoja yangu kwanza, kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii tena ili niweze kuhitimisha hoja hii ambayo niliiwasilisha asubuhi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwanza, sisi hatukutarajia kwamba tungepata wachangiaji wengi kama hivi kwa kutazamia tu kwamba hii ni taarifa ya Kamati na siyo mchakato wa bajeti kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Lakini kwa unyeti wa Kamati yetu na masuala ya Miundombinu ndio maana Waheshimiwa Wabunge wamevutika kutoa michango yao kwa kusema hapa Bungeni na wengi vilevile wametoa michango yao kwa maandishi. Kwa kweli mimi kwa niaba ya Kamati yangu ya Miundombinu naomba niwapongeze sana kwa michango yenu ambayo tumeizingatia.

Labda nianze kwanza kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kusema hapa Bungeni, wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Mohammed Mnyaa, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Rished, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Profesa Mtulia na mwisho Mheshimiwa Andrew Chenge Waziri wetu wa Miundombinu. Wale ambao wamechangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye.

Kwa hiyo, kama nilivyosema tumepata wachangiaji wengi na sisi kwa kifupi tunasema kwamba tumepokea ushauri wenu, tumepokea mawazo yenu ushauri mlioutoa, utatusaidia sisi kama Kamati . Lakini kwa vile Serikali nayo ipo imesikia, yuko Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na kwa ujumla Serikali ipo. Nina hakika yale yote ambayo yanaihusu Serikali ambayo baadhi yake yamefafanuliwa na Mheshimiwa Waziri wetu ingawa hakuyamaliza yote kwa sababu ya muda basi watakuwa wamesikia na tutakapokuwa tunakutana kwenye vikao vyetu katika Kamati na Wizara tutaendelea kuyafuatilia ili kuona kwamba yale yanayokusudiwa na yale yaliyosema yanaweza yakatekelezwa. Kama ambayo ilikuwa kwenye taarifa, hoja nyingi zimetolewa kuhusu barabara, bandari zetu, viwanja vya ndege, kuhusu reli kwa maana ya *TAZARA* na reli ya kati ambayo sasa imekabidhiwa mwekezaji chini ya Kampuni ya *Tanzania Railway Limited*. Limekuwepo pia suala la shilingi bilioni 10 zile ambazo zilikuwa zimeahidiwa na Serikali kwa ajili ya matengenezo ya barabara baada ya zile barabara kutokana na mvua nyingi.

Lipo suala la *ATCL*, simu za mikononi kama walivyoonyesha wajumbe wasiwasi kwamba gharama ni kubwa ukilinganisha na wenzetu nchi jirani za Afrika Mashariki. Lakini suala la wakandarasi nalo limejadiliwa kwa umuhimu wake kwamba baadhi yao kazi zao ni substandard na vile vile suala la vivuko hasa Busisi na kwa rafiki yangu Rished kule Kivuko cha Mto Pangani nilikwenda nimeona, nimepanda boti moja mimi mwenyewe nikawa na wasiwasi kama nitafika. Lakini kwa kudra za Mwenyezi Mungu tulikamilisha hiyo. Mheshimiwa Waziri, ametutolea maelezo sina sababu ya kurudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maeneo mengi ambayo yalitolewa pamoja na suala la posta ambalo limekuwa likikera kwa muda mrefu. Lakini nataka nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kuweza kutatua tatizo la posta na sasa kazi iwe kwao kama alivyosema, wamepata nafasi baada ya kufutiwa madeni vitabu vyao ni safi wanaweza wakakopa basi nadhani wanaweza kazi vizuri.

Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri amenipunguzia kazi, kwa hiyo, mimi yangu ambayo ninaweza nika-*comment* hapa ni machache kama ifuatavyo: Mheshimiwa Mwadini Jecha pamoja na Mheshimiwa Athumani Janguo walieleza wasiwasi wao kuhusu suala la kufadhiliwa na Wizara kwa kazi za Kamati, badala ya mfuko labda wa Bunge. Nadhani *concern* hiyo imesikika. Kwa bahati mbaya mimi siyo msemaji wa Ofisi ya Bunge, wala sikupewa *mandate* na Mheshimiwa Spika, kulielezea hili. Lakini kwa ufupi kama mnavyofahamu kwa mujibu wa taratibu zetu tulizonazo Kamati zote zimepewa muda wa wiki mbili kufanya kazi zetu kabla ya Bunge na wiki mbili zile zinatazamiwa kazi ya kwanza, ni kuangalia Miswada inayowasilishwa na Serikali kupitia Ofisi hii ya Mheshimiwa Spika. Hilo ndilo la msingi la kwanza ambalo lazima tulikamilishe katika wiki zile mbili. Wakati mwingine tunapata matatizo ndiyo sababu baadhi ya Miswada haikamiliki kwa sababu moja au nyingine lakini sina sababu ya kusemea hapa. La pili, ni kupitia taarifa za mashirika na taasisi ambazo ziko chini ya Wizara zinazohusika sisi kwetu ni nyingi, ndiyo kazi mbili ambazo wiki zile mbili kwa kweli ukizitumia vizuri unaweza ukakamilisha na wakati mwingine usikamilishe. Sasa ukitazamia wiki hizi mbili na ukafanya ile kazi ambayo tumeisema ya *value for money* kwenda kuangalia miradi mbalimbali kwa mfano, uende Sumbawanga uangalie barabara ile ya kutoka Tunduma mpaka Sumbawanga mpaka Bandari ya Kasanga, au ukague reli kutoka Dar es Salaam - Dodoma uende Tabora mpaka Kigoma, haiwezekani katika zile wiki mbili ukafanya kazi hii kwa kutegemea hiyo. Kwa hiyo, lazima utafute njia nyingine uwe *innovative.* Kamati iwe *innovative* ya kutafuta fedha nyingine, hakuna njia nyingine, hakuna mfadhili mzuri zaidi ya Serikali, ndiyo maana tumejikuta kwamba tumelazimika kuomba ufadhili wa Serikali na tumetumia neno ufadhili lakini nadhani ni haki ya Serikali ku-*finance* shughuli za Kamati kama vile shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa hili niseme tu kwamba Serikali imesikia kwamba kuna haja ya kutembelea miradi si Kamati hii tu, Kamati zote ili kuona *value for money* kuona kama kweli barabara inayohusika imetengenezwa kulingana na fedha zile ambazo tumetoa, kweli shule au zahanati imejengwa kulingana na fedha zilizotolewa. Kwa hiyo, Serikali imesikia, Waheshimiwa Mawaziri wapo hapa lakini pia

na Mheshimiwa Spika na Katibu wa Bunge, nao wamesikia. Kwa hiyo, katika *interruption* kati ya Serikali na Ofisi ya Bunge, wataangalia uwezekano wa kuwa na fedha za ziada ukiacha zile wiki mbili ambazo ndizo tunazifanyia kazi. Fedha za ziada za kuziwezesha Kamati zetu ikiwa ni pamoja na Kamati yangu ya Miundombinu kuweza kwenda kukagua miradi mbalimbali ambayo ikiwa ni pamoja na hiyo ambayo nimeitaja kwa umbali wake, ile ya Sumbawanga mpaka *Port* Kasanga na mingine ya Kigoma na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala ambalo limezungumzwa vilevile na Mheshimiwa Jecha, suala la usalama wa baadhi ya ndege za mashirika yetu. Ni kweli kwamba kuna matatizo. Sisi katika Kamati yetu tulikwishapata malalamiko na tulikwishapanga kikao kati ya Kamati ya Miundombinu na wenzetu wanaosimamia usalama hawa *TCCA* na wakati tunapanga hili tulipata malalamiko kwa upande wa *Precision Air*. Wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wao wenyewe wamepanda *Precision Air* hata wakitakiwa kueleza wataeleza jinsi ambavyo si mara mbili si mara tatu wameshindwa kwenda kunakohusika. Wameshindwa kutua, wamefanyaje acha zile taasisi ambazo zimeelezwa na Mheshimiwa Jecha pale. Kwa hiyo, tumepanga kikao kama Kamati kukutana na hao wenzetu ambao wamekabidhiwa kazi ya *TCCA* ili tuwaite hao wenye ndege umetuongezea Mheshimiwa Jecha hao wengine ambao umewataja tutawaita pamoja tuwaeleze *concern* ya wananchi wetu ya abiria hawa lakini vilevile na wao tuwasikilize na kisha ndiyo tutapata nafasi ya kuishauri Serikali inavyoonekana inafaa.

Vilevile Kamati yetu katika kuzingatia suala hili la gharama za simu za mkononi tumepanga kikao na kinafanyika hapa Dodoma tarehe 13 kati ya sisi na *TCRA* ili kusudi pamoja na mambo mengine lakini tuendelee kuwakumbusha suala la kuwadhibiti wenzetu hawa kuwabana wenzetu hawa. Haya tuliyosema ya kuchangia minara na kadhalika kwa maana ya kwamba kwa kweli bado bei ziko juu au gharama ziko juu ukilinganisha na wenzetu. Kwa hiyo, kikao kinafanyika hapa tarehe 13, ni vizuri mkajua tu hiyo katika kutekeleza hayo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamejaribu kuyasema.

Suala la Mheshimiwa Ndesamburo, kuhusu kuwa na *culture* ya kutunza barabara zetu, kama mnakumbuka ile sheria yetu ambayo tumeipitisha ya barabara kuna *component* ndani mle katika vifungu ambavyo vitasaidia kui-*force* kuona kwamba tunatunza barabara zetu na ziko adhabu kali zimetengwa au zimeelezwa katika sheria hii ambayo nadhani tunayo na kama tulivyosema imeshatiwa saini itaanza kutumika wakati wowote huu kwamba kuna vifungu vile ambavyo vitasaidia kuona kwamba tunatunza barabara hizi na wale watakaokiuka watachukuliwa hatua kali kadri itakavyoonekana inafaa. Nitumie nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri akamilishe kanuni zile zitakazosaidia utekelezaji wenye sheria kwa sababu sheria ikikamilika kama ulivyosaini na kanuni zikikamilika ndiyo itakuwa na uharaka zaidi wa kuitumia.

Ndugu yangu Ruth Msafiri ameshauri Kamati ipewe nguvu za kushauri Serikali dhidi ya watumishi wabovu au wanaodanganya Kamati zetu. Nadhani wazo ni zuri tumelisikia na Serikali imelisikia lakini, sisi kama Wabunge tuko katika mchakato wa kupitia kanuni zetu za Bunge, pengine ni nafasi nzuri kutumia fursa hiyo. Mheshimiwa

Spika, amekwishatamka kuwa kutakuwa na kikao maalumu cha kupitia kanuni zetu za Bunge. Hili linaweza likashughulikiwa katika kanuni zetu tukapata uwezo wa kuwashughulikia baadhi ya watendaji ambao ama wanapotosha au tukiwaita hawaji au hawaji *in time* na pengine kukwamishwa shughuli za Kamati. Kwa hiyo, tutakapokuwa tunapitia Kanuni zetu tunaweza tukaliangalia hili halafu Serikali itajua namna ya kulishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la makandarasi ambao wanaonekana *sub-standard.* Labda hili niliseme haraka haraka mawili. Moja, katika barabara hizi kubwa za kitaifa, imeanza kuonekana kwamba hii Sheria yetu ya *Procurement* nayo inaweza ikawa inachangia kupata wakandarasi ambao ni dhaifu kwa kigezo tu kwamba yule anayetenda kidogo ndiye anayechaguliwa kwenda kutengeneza barabara. Mimi sina hakika lakini kumbukumbu yangu inaniambia kwamba ndani ya Sheria ile kuna kipengele ambacho kinasema hata kama mtu ametenda *low*, lakini ukaangalia mazingira mbalimbali, wakaona kwamba huyu mtu hana uwezo sidhani kwamba lazima yule apewe. Hata kama ametenda *low,* sidhani kama kuna kipengele kinasema hivyo. *(Makofi)*

Lakini hapa ni mfano, nyinyi mnao ushahidi kwamba barabara zetu zingine baadhi ya barabara ambazo zimekwama ni kwa sababu makandarasi walitenda *very low,* matokeo yake hawakufanya kazi ile sawa sawa, matokeo yake baadaye wakaanza kuleta hizo *variation costs,* Serikali ikakaa muda mrefu kujadili ni sawa au siyo sawa, wakati mtu huyu alipewa nafasi ya kufanya *due deligency* katika barabara hizi. Sasa vipi tena aje nyuma aseme hii ilikuwa hivyo, kwa sababu alipaswa kuangalia gharama zake. Lakini wako wengine ambao naambiwa wanafanya hivyo makusudi a-*win* kazi halafu baadaye atatumia *technicalities* za kisheria na kadhalika ili kuona kwamba anaongezewa pesa lakini wakati ule alitenda *very low* kwa maana ya kumshawishi au kuishawishi Serikali iwape tenda na kadhalika.

Tatizo basi Serikali iangalie uwezekano wa kuleta marekebisho ya sheria tusikwamishe, tusiharibu kazi za barabara kwa sababu ya Sheria ambayo sisi tuko hapa kuzirekebisha na kuzitengeneza. Wito na ushauri wangu hapa kwa niaba ya Kamati, ni kwamba wenzetu wa Serikali waiangalie kama kweli ni lazima basi turekebishe vinginevyo wasing'ang'anie kutekeleza kifungu kwamba maadamu wametenda gharama ya chini basi huyu huyu ndiyo apewe, matokeo yake mimi sitaki kuwataja hapa au Taasisi zile, nyinyi mnawajua, lakini ni kweli watu wametukwamisha na wataendelea kutukwamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na taarifa nyingine sitaki kumtaja mtu, lakini yako mashirika mengine ya nchi za kimataifa, wanaogopa kuja kutenda barabara Tanzania. Wanasema ukienda Tanzania huwezi ukapata kazi, kwa sababu wako watu ambao maalumu, wanajulikana kwamba hawa wanatenda *very low*, kwa hiyo, wewe unajisumbua bure. Ni vizuri Serikali wakaliangalia. Sina uhakika wa ukweli kwake, lakini ndivyo wanavyosema, kwamba makampuni mengi ya kimataifa iwe ya kutoka Japan, Marekani au wapi, wanaogopa kutenda, hawatendi kwa sababu wanajua kabisa kwamba wao hawatapewa, wako watu wataalamu wa kutenda *very low* na wakapewa

hiyo kazi. Sasa kwa nini wapoteze shughuli zao, hasara zao. Naomba nitumie nafasi hii kuiomba Serikali kama kuna ukweli katika haya wayaangalie ili kusudi kuepukana na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, taarifa yetu ile ilikuwa imeishia Juni, lakini kweli ziko *developments* nyingi hapa katikati. Mheshimiwa Kaboyonga nimshukuru sana ameelezea vizuri sana habari za Sherika la Reli *TRC*. Lakini hata *ATCL* kama mnavyofahamu, imefika mahala pale kuanzia mkataba ule ulipomalizika na kuanzia Aprili mpaka Juni, Shirika lilikabidhiwa kwetu ingawa bado tulikuwa tunaendelea kufanya kazi na wenzetu wa *South African Airways* na tiketi zao ziliendelea kutumika mpaka Juni, 2007.

Kuanzia Julai 1, 2007 tumeanza kutumia tiketi zetu wenyewe za *ATC* na Shirika limeshikiliwa na wenzetu chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Mustafa Nyang'anyi, kama Mwenyekiti wetu na kijana wetu shupavu David Mataka ambao nina hakika kwamba wakipewa nafasi, na msaada na Serikali wanaweza wakalifanyia mambo mazuri shirika hili na likawa *competitive* kama ilivyokuwa imeshauriwa na Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa.

Vilevile kama mnavyofahamu sasa yule Twiga ambaye tulikuwa tunamlilia naye amekwisharejeshwa, uzinduzi ulifanyika tarehe 29 mwezi Septemba na kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2007 Twiga yule ameanza kutumika na katika mpango wao ambao hawataki kuutangaza ndege mpya zitakazokuja nina hakika zitakuwa na Twiga wetu akiwa amekaa mahala ambapo anaonekana mahala pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme mengi yalishasemwa na wenzangu wale. Lakini nisisitize suala moja la shilingi bilioni 10. Ni kweli liko tatizo kubwa la makandarasi hawa ambao hawajalipwa shilingi milioni 10 na sisi kama Kamati tulipolifuatia hili mwanzoni tulifika mahala tutakuta kwamba kwa sababu i*deally* au kiutawala ungetegemea fedha hizi zitoke Hazina zije Wizara ya Miundombinu ziende *TANROADS* lakini tukaambiwa kwamba haiwezekani, fedha hizi zinabaki Hazina. Makandarasi watakaomaliza wata-*raise certificates* na *certificates* zile zitakwenda Wizara ya Miundombinu zithibitishwe na halafu ndiyo ziende Hazina ili walipe. Sasa hilo ndilo tatizo.

Mmesikia lugha ambayo ameitumia Mheshimiwa Waziri wangu, nadhani ameshindwa kuji-*commit.* Lakini tatizo lipo, ni kwamba fedha zile ziko Hazina, haziko Wizara ya Miundombinu kwa mujibu wa taratibu zetu. Sasa kwa kweli mtu wa kusema hapa tuombe sana wenzetu, Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha au Hazina kwa kweli waliokoe jahazi la kulipa hizi fedha kama walivyoahidi.

Kama tuliahidi kuwalipa makandarasi wakafanya kazi, lakini sasa hatuwalipi ni jambo la kusikitisha sana. Mimi namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, hili mimi sitaki kumkabidhi Waziri wangu hapa, lakini sisi kama Kamati ya Miundombinu tulishakaa hapa, tukakaa Dar es Salaam na tumeazimia kumwita Waziri wa Fedha na Waziri wa Miundombinu watueleze ni lini watalipa fedha hizi na kama hawatapata jibu la

msingi tumeamua kwenda kumwona tena Mheshimiwa Waziri Mkuu ili aokoe jahazi la kuhakikisha kwamba anazikutanisha hizi Wizara mbili ili kusudi zile shilingi bilioni 10 ambazo zilikuwa zimeahidiwa zinalipwa mikoani kusudi makandarasi wale wapewe.

Tatizo litakalojitokeza ni kwamba barabara zitakazotengenezwa kwa bajeti ya 2007/2008 zitatengeneza zitalipwa, hizo barabara mpya. Barabara zile ambazo zilitengenezwa nyuma kwa mkandarasi ambazo tayari zimekwisha haziwezi kulipwa kwa sababu fedha hazipo. Sasa hapo mantiki ipo wapi?

Huyo aliyetengeneza jana kwa mkopo humlipi, huyu anayetengeneza leo unampa kwa sababu pesa unazo. Serikali hiyo hiyo moja! Ni jambo ambalo halieleweki. Kwa hiyo, kama alivyosema tutawaita Mawaziri hawa tuzungumze nao watueleze, lakini kama ikibidi kwamba hatutapata maelezo ya kuridhisha tutamwomba tena Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati ili kupata usuluhishi wa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kurudia kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kukamilisha hoja yangu hii. Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu, kwa ushauri wenu. Tumeuzingatia, utatusaidia sisi Kamati lakini pia utaisaidia sana Serikali katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha mwaka huu ambao umebakia na ni imani yangu kwamba tutayafuatilia kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru tena Kamati yangu kwa kazi nzuri ambayo imeifanya mpaka tumekamilisha taarifa yetu. *Inshallah* sasa tuko karibu mwisho wa kumaliza mwaka 2007 na sisi tumekwishaanza taarifa ya mwaka 2007 ambayo itakuwa na *informations* ambazo ziko kamilifu zinazokwenda na wakati. Tatizo ni kwamba taarifa hizi zilijadiliwa huko nyuma.

Sasa zimejadiliwa *very late*, nadhani huko mwakani Mheshimiwa Spika na Ofisi ya Katibu watapanga taarifa hizi zijadiliwe mapema zaidi ili ziende na wakati kuliko ilivyo sasa. Baada ya kusema hayo, kwa heshima na taadhima, naomba tena kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kwa mwaka 2006 ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mwenyekiti, hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, nilimwona Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Hadija Ngozi, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga na kadhalika, bila kumsahau Mheshimiwa James Msekela.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua tuliyofikia sasa naomba niwahoji kama tunaikubali na kuipokea ripoti hii ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Wote wameafiki. Kwa hiyo, Bunge limeipokea rasmi ripoti hii na itafanyiwa kazi kwa taratibu zilizopo. Nitoe tangazo moja tu ambalo lilitolewa asubuhi kwamba kuna, maonyesho ya asali, vimekuja vikundi mbalimbali vinavyojishughulisha na masuala yote ya asali katika nchi yetu. Wapo leo na watakuwepo pia kesho, wanaendelea kuwepo katika viwanja vyetu. Tunaombwa sana Waheshimiwa Wabunge kwa wakati wa mchana tukiwa na nafasi basi tuweze kuwatembelea na kuona jinsi ambavyo Watanzania hawa wanajitahidi katika kuboresha zao hili ili liwe ni sehemu ya mazao yanayoweza kutuletea biashara kubwa ya kimataifa. Wapo wajasiriamali kutoka Kigoma, Tabora maeneo ya Inyonga, Nzega, Sikonge, Uyui, wako kutoka Korogwe, Manyoni na maeneo mengine mengi na wengi wao wamelalamika kwamba hawajawaona Wabunge wao. *(Makofi)*

Wangependa sana mfike muweze kujionea wenyewe. Basi baada ya tangazo hilo Meza yangu hapa kwa shughuli za leo zilizopangwa katika *Order Paper* zote zimekamilika. Kwa hiyo, naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.40 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka siku ya Alhamisi,
Tarehe 8 Novemba, 2007, Saa 3.00 Asubuhi)*